# USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIUME KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LA HER*I NA NGUU ZA JADI

**KIEMA AGNES MWONGELI**

**Tasnifu Hii Imewasilishwa kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili Katika Idara ya Isimu na Lugha**

**Chuo Kikuu cha Machakos, Kenya**

**OCTOBA 2025**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe wala haijawasilishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

| | |
|---|---|
| _______________ | 30.10.2025 |
| Kiema Agnes Mwongeli | Tarehe |
| C50-6901-2020 | |

Idhini ya wasimamizi

Tasnifu hii imewasilishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Machakos.

| | |
|---|---|
| _______________ | 3-11-2025 |
| Dkt. John Mutua | Tarehe |
| Idara ya Isimu na Lugha | |
| Chuo Kikuu cha Machakos | |

| | |
|---|---|
| _______________ | 30/10/2025 |
| Dkt. Sarah Ndanu M. Ngesu | Tarehe |
| Idara ya Isimu, Lugha na Fasihi | |
| Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya | |

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa marehemu Kiema Kaloki na Tabitha Kiema kwa kunihamasisha kutia bidii maishani.

## SHUKURANI

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uaminifu wake kwangu. Amenijalia uhai na neema ya kuikamilisha kazi hii. Nawashukuru pia wasimamaizi wangu Dkt. John Mutua na Dkt. Sarah Ndanu M. Ngesu kwa kunielekeza hatua baada ya hatua hadi kuikamilisha kazi hii. Mola awabariki sana. Aidha, ninawashukuru wahadhiri wengine wa Chuo Kikuu cha Machakos, hususan wa Idara ya Isimu na Lugha walionifundisha, kunielekeza na kunitia moyo hadi kukamilisha kuandika tasnifu hii. Hawa ni Dkt. Vifu Makoti na Dkt. Charles Kebaya. Ninamshukuru pia mwanafunzi mwenzangu, Agnes N. Mwaniki tuliyesoma pamoja, kusaidiana na kutiana moyo katika safari hii ndefu ya kusoma shahada ya uzamili. Halikadhalika, shukurani maalum ni kwa familia yangu; mume wangu mpendwa Benson M. Kitema na watoto wetu Nehemiah na Mercy, kwa uvumilivu wao.

## YALIYOMO

**UNGAMO** ........................................ **ii**

**TABARUKU** ........................................ **iii**

**SHUKURANI** ........................................ **iv**

**YALIYOMO** ........................................ **v**

**UFAFANUZI WA ISTILAHI** ........................................ **ix**

**ORODHA YA VIFUPISHO** ........................................ **x**

**IKISIRI** ........................................ **xi**

**ABSTRACT** ........................................ **xii**

**SURA YA KWANZA** ........................................ 1

1.0 Utangulizi ........................................ 1

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ........................................ 1

1.2 Suala la Utafiti ........................................ 3

1.3 Malengo ya Utafiti ........................................ 4

1.4 Maswali ya Utafiti ........................................ 4

1.5 Sababu za Kuteua Mada ........................................ 4

1.6 Upeo wa Utafiti ........................................ 5

1.7 Hitimisho ........................................ 6

**SURA YA PILI:YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA NA MISINGI YA NADHARIA** ........................................ 7

2.0 Utangulizi ........................................ 7

2.1 Tasnifu ........................................ 7

2.2 Makala ........................................ 15

2.3 Vitabu ........................................ 17

2.4 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko ........................................ 18

2.5 Mtazamo wa kinadharia ........................................ 18

2.6 Hitimisho ........................................ 20

**SURA YA TATU:MBINU ZA UTAFITI** .......... 21
3.0 Utangulizi .......... 21
3.1 Eneo la Utafiti .......... 21
3.2 Muundo wa Utafiti .......... 21
3.3 Sampuli .......... 22
3.3.1 Uteuzi wa Sampuli .......... 22
3.4 Ukusanyaji wa Data .......... 22
3.5 Vifaa vya Kukusanyia Data .......... 23
3.6 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data .......... 23
3.7 Hitimisho .......... 24
**SURA YA NNE:UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA** .......... 25
4.0 Utangulizi .......... 25
4.1 Usawiri wa Mhusika wa Kiume katika Riwaya Teule .......... 25
4.1.1 Mwanamume aliyetelekezwa katika Jamii .......... 26
4.1.2 Mwanamume aliyekosa Matumaini .......... 28
4.1.3 Mwanamume Aliyekosa Nafasi katika Jamii .......... 29
4.1.4 Mwanamume kama Kiumbe Mvumilivu .......... 30
4.1.5 Mwanamume Amesawiriwa kama Kiumbe Mlevi .......... 33
4.1.6 Mwanamume kama Mwenye Msimamo Imara .......... 36
4.1.7 Mwanamume kama Mtetezi wa Haki .......... 38
4.1.8 Mwanamume kama Jasiri .......... 40
4.1.9 Mwanamume kama Mwenye Bidii .......... 42
4.1.10. Mwanamume kama Mlezi Mwema .......... 44
4.1.11 Mwanamume anayefanyiwa Ukatili .......... 46
4.1.12 Mwanamume kama Mwanamapinduzi .......... 47
4.1.13 Mwanamume kama Anayesalitiwa .......... 50
4.1.14. Mwanamume kama Kiumbe asiye na Hisia .......... 51

4.1.15 Anayebaguliwa kwa Misingi ya Kiukoo ........ 52
4.1.16 Mwanamume kama Anayempenda Mkewe ........ 53
4.1.17 Mwanamume kama Mwenye Tamaa na Ubinafsi ........ 54
4.1.18 Mwanamume kama Fisadi ........ 56
4.2 Changamoto Zinazomkabili Mhusika wa Kiume katika Riwaya Teule ........ 57
4.2.1 Mwanamume kukosa Kazi ........ 58
4.2.2 Kutelekezwa katika Jamii ........ 60
4.2.3 Mwanamume kukosa Matumaini ........ 62
4.2.4 Kulemewa na Ulevi ........ 64
4.2.5 Kusalitiwa kwa mwanamume ........ 66
4.2.6 Kutumikishwa katika Jamii ........ 67
4.2.7 Kutopewa Nafasi katika Jamii ........ 68
4.2.8 Kujeruhiwa kimwili na Kisaikolojia ........ 69
4.2.9 Ukosefu wa Elimu ........ 70
4.2.10 Umaskini ........ 72
4.2.11 Mwanamume anayetekwa Nyara ........ 73
4.2.12 Mwanamume kuwa na malezi mabaya ........ 74
4.3 Namna Changamoto zinazomkabili Mhusika wa Kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake katika Riwaya Teule ........ 75
4.3.1 Athari za Ukosefu wa Nafasi za Kazi ........ 75
4.3.2 Athari za Usaliti kwa Mhusika wa Kiume ........ 78
4.3.3 Athari za Ulevi ........ 80
4.3.4 Athari za Utelekezaji wa Mwanamume ........ 81
4.3.5 Athari za Mapigo na Dhiki za Kisaikolojia ........ 83
4.3.6 Athari za Ukosefu wa Elimu ........ 84
4.3.7 Athari za Ukosefu wa Matumaini ........ 85
4.3.8 Athari za Utekaji Nyara ........ 86

4.3.9 Athari za Malezi Mabaya ................................................................. 88

4.4 Hitimisho................................................................................................ 89

**SURA YA TANO**:**HITIMISO NA MAPENDEKEZO** ........................................ 90

5.0 Utangulizi............................................................................................ 90

5.1 Matokeo ya Utafiti ................................................................................ 90

5.2 Waathirika wa Mchango wa Utafiti Huu: ............................................. 94

5.3 Mapendekezo ........................................................................................ 94

**MAREJELEO** ............................................................................................ 96

KIAMBATISHO I ........................................................................................ 100

KIAMBATISHO II ....................................................................................... 101

KIAMBATISHO III....................................................................................... 102

KIAMBATISHO IV ...................................................................................... 103

# UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| **Jinsia**: | Hali ya kuwa mume au mke. |
| **Mhusika wa kiume:** | Wahusika wote wa kiume. |
| **Nadharia**: | Mwongozo unaotumiwa na msomaji kuhakiki kazi ya fasihi. |
| **Usawiri**: | Uchoraji au uumbaji wa mhusika au wahusika katika kazi ya fasihi. |
| **Wahusika**: | Ni watendaji au viumbe wanaomsaidia msanii kuwasilisha maudhui na dhamira. |

## ORODHA YA VIFUPISHO

**Dkt** - Daktari

**K.t.j** - Keshatajwa

**n.k** - Na kadhalika

**TUKI** - Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

**IKISIRI**

Katika karne ya ishirini na moja, mwanamke amewekwa mbele kinyume na ilivyokuwa wakati dunia ilikuwa imetawaliwa na ubabedume. Hali hii inasawiri mabadiliko katika jamii. Mabadiliko haya yamemwathiri mwanamume katika jamii. Utafiti huu ulichunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia ya uhalisia inadai kwamba, fasihi inalenga kutoa picha halisi ya jamii husika. Nadharia hii ilizuka huko Ulaya katika karne ya kumi na tisa. Miongoni mwa wataalamu waliohusishwa na nadharia hii ni Georg Lukacs (1972). Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi mhusika wa kiume anavyosawiriwa katika riwaya teule. Aidha, umebainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule. Halikadhalika, utafiti huu umeonyesha jinsi changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani ambapo riwaya ya *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi* zilisomwa na kuhakikiwa. Riwaya hizi zilichanguliwa kimakusudi. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo. Utafiti huu umeangazia masuala ya jinsia ya kiume, jambo ambalo linahusu jamii kwa jumla. Vilevile, kutokana na utafiti huu, jamii itaweza kubaini changamoto mbalimbali zinazoikabili jinsia ya kiume na athari ya changamoto hizo na hivyo, kuwa na uwezo wa kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo. Halikadhalika, utafiti huu utakuwa kichocheo na rejea muhimu kwa watafiti wa baadaye wa fasihi kuchunguza masuala yanayohusu jinsia ya kiume.

# ABSTRACT

In the 21st Century, women have been placed at the forefront, a stark contrast to past eras when patriarchy ruled society. This shift illustrates the societal transformations that have taken place. These changes have had a significant impact on the role and perception of men within the community. This study explored the representation of male characters in the novels *Chozi la Heri* and *Nguu za Jadi*, guided by the theory of realism. Realism advocates for literature to reflect the true nature of society. This theory originated in Europe during the 19th century, with Georg Lukács (1972) being among the key proponents. The main objective of this research was to examine how male characters are depicted in the selected literary texts. Additionally, the study identified the challenges these male figures face and demonstrated how these challenges influence both their personal lives and the wider society. This was a library-based study, where the two novels were critically read and analyzed. These novels were purposively chosen. The collected data was then interpreted and presented descriptively. This research focused on issues concerning the male gender, issues that are relevant to society at large. Moreover, the findings from this study will enable communities to recognize the struggles experienced by men and the resulting societal effects, ultimately guiding the development of strategies to address such challenges. This study will also serve as a valuable foundation and inspiration for future literary scholars interested in gender-focused literary analysis, particularly on masculinity.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ndiyo msingi wa utafiti huu. Utafiti huu unahusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Katika sura hii tumeshughulikia masuala ya kimsingi yanayojenga msingi wa utafiti. Masuala haya ni pamoja na; usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuteua mada na upeo wa utafiti.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Jinsia ni suala mtambuko ambalo linaendelea kuwashughulisha wataalamu wengi duniani. Bayyo (2020) anaeleza kuwa katika mjadala kuhusiana na masuala ya jinsia, fikira za watu wengi huelekezwa kwa jinsia ya kike. Jinsia ya kike hupewa kipaumbele katika mijadala inayolenga kuonesha namna inavyoonewa na kudhulumiwa.

Mhusika ni kiumbe ambaye hupatikana katika kazi za fasihi anayefanana na binadamu halisi kwa kiasi fulani (Njogu na Chimera 1999). Wahusika ni viumbe ambao hubuniwa na msanii kutokana na maisha ya jamii yake na pia kulingana na anachotaka kukifafanua (Mlacha 1985). Ili malengo ya mwandishi wa kazi ya fasihi yamfikie msomaji, kipengele cha wahusika lazima kitumike. Fasihi inahusiana na jamii naye mwandishi wa kazi ya fasihi ni zao la jamii. Hivyo, mwandishi wa kazi ya fasihi huandika mambo yanayohusiana na jamii na hutumia wahusika kuwasilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii husika.

Katika jamii ya mtafiti kuna watu wa jinsia zote, yaani wanaume na wanawake, ambayo ni hali halisi ya maisha ya binadamu. Wanaume na wanawake hawa hujitokeza katika

kazi ya fasihi kama wahusika. Kwa miaka mingi jamii imekuwa ikimzungumzia mwanamke na kumsahau mwanamume. Isitoshe, masuala mengi yamechunguzwa kuhusu jinsia ya kike katika fasihi huku wahusika wa kiume wakisahaulika na masuala yanayowahusu kutoangaziwa kikamilifu ikilinganishwa na wahusika wa kike (Kilonzo 2015). Wafeministi huamini kuwa, mwanamke hudhulumiwa na mwanamume katika jamii. Imani hii imekuwa kichocheo cha watafiti wengi kuchunguza usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili huku masuala ya wahusika wa kiume yakipuuzwa.

Kwa mujibu wa Katiba ya Kenya (2010) kifungu cha tisini na saba (97), kila eneo Bunge lina mwakilishi wa wanawake ilhali hakuna anayewawakilisha wanaume. Kanwa (2022) anasema ya kwamba, hali hii ya wanawake inaonekana katika siasa ulimwenguni kote kama njia ya kubadilisha hali ya makundi ya watu wanaodhaniwa kuwa wametelekezwa duniani.

Atieno (2019) anaeleza kuwa, jamii imepuuza jinsia ya kiume kutokana na fikra kuwa ina uwezo wa kujitetea na kukabiliana na changamoto inayokumbana nazo. Jambo hili limechangia hali ya upweke miongoni mwa wanaume kwa sababu hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Wafeministi wa Kiafrika wanaopigania ukombozi wa mwanamke, haki na usawa wa kijinsia, wamenuia kuwapa wanawake mwelekeo mbadala kwa msingi wa utamaduni wa kimapokeo ilhali wanaume wamesalia kufuata mwelekeo wa utamaduni wa kimapokeo kwa kukosa mwelekeo mbadala kama wanawake, jambo ambalo linaathiri uhusiano wao zaidi (Atieno 2019).

Hivyo, kwa kuwa masuala ya jinsia ya kike yamekuwa yakishughulikiwa kwa miaka mingi iliyopita, kuna haja ya kuchunguza masuala yanayohusujinsia ya kiume ili

kuonyesha inavyosawiriwa katika kazi za fasihi. Utafiti huu umechunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Riwaya hizi zimeteuliwa kimaksudi kwa sababu ni za karne ya ishirini na moja na zinamsawiri mhusika wa kiume katika nyanja mbalimbali za maisha. Aidha, riwaya hizi ziliteuliwa kwa kuwa zimeandikwa na waandishi wanawake ambao wanaangazia jinsia ya kiume katika miaka ya sasa.  Hivyo, riwaya hizi zilionekana zitaweza kuibua masuala ibuka kuhusiana na uhalisia uliopo katika usawiri wa jinsia ya kiume kwenye kazi za fasihi ya Kiswahili.

**1.2 Suala la Utafiti**

Jinsia ni suala ambalo limepewa kipaumbele miongoni mwa masuala yanayotafitiwa katika taaluma mbalimbali zinazohusu maisha ya binadamu. Hata hivyo, suala hili limeangaziwa na watafiti waliotangulia kwa kujiegemeza katika jinsia ya kike. Mohamed (2018) anasema kuwa, kuchunguza nafasi ya mwanamume katika fasihi ni suala geni kwa sababu watafiti wengi wamejikita katika kushughulikia masuala ya wanawake. Anaeleza kuwa, katika ulimwengu wa riwaya ya Kiswahili na fasihi, imekuwa kama jambo la kawaida kwa watafiti wengi kuchunguza masuala ya wanawake zaidi kuliko masuala yanayowahusu wanaume. Jambo hili huenda limetokana na ukweli kwamba, kumekuwa na mwamko wa kupigania haki za wanawake kwa lengo la kudumisha usawa miongoni mwa jamii na nyanja mbalimbali. Hali hii imesababisha kusahaulika kwa nafasi ya mwanaume katika jamii ya sasa. Watafiti wengi wamechunguza usawiri wa wahusika wa kike zaidi ikilinganishwa na usawiri wa wahusika wa kiume. Jambo hili limesababisha kupuuzwa na kutelekezwa kwa jinsia ya kiume katika jamii. Ni kutokana na hali hii ambapo, utafiti huu ulijikita

kuchunguza usawiri wa mhusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi* ili kiziba mapengo hayo.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

i. Kuchunguza jinsi mhusika wa kiume anavyosawiriwa katika riwaya teule.

ii. Kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule.

iii. Kuonyesha namna changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Je, mhusika wa kiume anasawiriwa vipi katika riwaya teule?

ii. Ni changamoto gani zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule?

iii. Changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinamwathiri vipi binafsi na jamii yake?

### 1.5 Sababu za Kuteua Mada

Wanaume na wanawake waliomo katika jamii halisi ya binadamu, hujitokeza katika kazi ya fasihi kama wahusika. Kwa miaka mingi masuala kuhusu wahusika wa kike yamekuwa yakishughulikiwa huku mhusika wa kiume akisahaulika. Watafiti wengi wa hapo awali wameegemea zaidi kwenye aina za dhuluma ambazo wanawake hukumbana nazo katika jamii za Kiafrika. Watafiti hao ni pamoja na; Materu (1982), Ndungo (1988), Momanyi (2000), Mnenuka (2011), Mavisi 2017), Mutua (2017) na wengine. Isitoshe, anga nzima imehanikiza vilio vya kumkinga mwanamke wala hakuna anayejali mustakabali wa jinsia ya kiume. Hali hii ilimchochea mtafiti kuichagua mada

hii. Msukumo wa kuichagua mada hii umetokana na kuwepo kwa pengo la kimaarifa kuhusu usawiri wa jinsia ya kiume katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Isitoshe, baadhi ya watafiti waliotangulia walipendekeza tafiti zifanywe ili kuchunguza masuala ya jinsia ya kiume kwa sababu mengi yametafitiwa kuhusiana na jinsia ya kike. Watafiti hawa ni kama Momanyi (1998), King'ei (2002), Wandera (2002) na Kimani (2003) ambao wanaeleza kuwa tafiti zinazoangazia masuala ya kijinsia katika fasihi ya Kiswahili zitaendelea kuwepo kwa sababu binadamu anaendelea kuwepo.

Kupuuzwa kwa jinsia ya kiume kumechangia hali yao ya upweke, kwa kuwa hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Utafiti huu ulinuia kuziba pengo hili la kimaarifa. Utafiti huu umetoa mwanga kuhusiana na masuala ya jinsia ya kiume. Aidha, tasnifu hii inatarajiwa kuwa kichocheo cha watafiti wa baadaye wa fasihi katika kuchunguza masuala yanayohusu jinsia ya kiume. Halikadhalika, kutokana na utafiti huu, jamii itaweza kubaini changamoto mbalimbali zinazoikabili jinsia ya kiume na athari ya changamoto hizo na kubuni mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Fasihi andishi ina tanzu mbalimbali ambazo ni; riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita kuchunguza usawiri wa jinsia ya kiume katika utanzu wa riwaya pekee. Hii ni kwa sababu, riwaya ina mawanda mapana yanayoweza kutosheleza malengo na kujibu maswali ya utafiti huu. Matei na Momanyi wameandika kazi mbalimbali za fasihi. Kazi zao zilizoteuliwa katika utafiti huu ni *Chozi la Heri* (2017) na *Nguu za Jadi* (2021). Ingawa Assumpta Matei ameandika riwaya moja tu ambayo iliteuliwa. Riwaya zingine zilizoandikwa na Clara Momanyi kama vile; *Tumaini* (2006), *Nakuruto* (2009) na nyingine, hazikushughulikiwa katika utafiti huu

kwa kuwa utafiti ulilenga riwaya inayomsawiri mhusika wa kiume kwa kina na pia riwaya iliyoandikwa katika karne hii. Masuala mengine kama vile usawiri wa wahusika wa kike, usawiri wa watoto na dhamira ya mwandishi, hayakushughulikiwa katika utafiti huu kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti huu umeshughulikia usawiri wa wahusika wa kiume katika jamii ya waandishi. Riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu ni *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi.* Riwaya hizi zinamsawiri mhusika wa kiume katika nyanja mbalimbali za maisha.

### 1.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia vipengele vya kimsingi kuhusu utangulizi. Vipengele hivyo ni; usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuteua mada na upeo wa utafiti.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mapitio ya maandiko yanayohusiana na mada ya utafiti huu na misingi ya nadharia. Mapitio ya maandishi yalihusisha maandiko kuhusu wahusika wa kiume na wa kike. Aidha, mapitio mengine yalihusu tafiti mbalimbali zilizofanywa katika fasihi. Maandiko yaliyorejelewa yaligawika katika sehemu tatu ambazo ni; tasnifu, makala na vitabu. Kazi hizi zilimwezesha mtafiti kubaini pengo la utafiti. Aidha, nadharia ambayo iliongoza utafiti huu imefafanuliwa.

## 2.1 Tasnifu

Tasnifu kadha zimeshughulikia suala la jinsia. Utafiti wa Katola (2006) ulihusu udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia nne za Kiswahili.Tamthilia hizi zimeandikwa na waandishi tofauti ambao ni Mwachofi *Mama Ee* (1987), Muhando *Hatia* (1972), Yahya na Mulwa, *Buriani* (1983) na Mohammed ameandika *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000). Katola ameonyesha kuwa mwanamke anakabiliana na dhuluma kutokana na mfumo wa kuumeni katika taasisi zinazojikita kwenye misingi ya ubabedume. Kulingana na Katola (k.t.j), baadhi ya dhuluma ambazo mwanamke hukabiliana nazo ni pamoja na; ndoa za lazima, kutusiwa, kutishwa, kupigwa, kutalikiwa, miongoni mwa zingine. Katola alichunguza utanzu wa tamthilia, tofauti na utafiti wetu ambao ulichunguza utanzu wa riwaya. Ingawa dhuluma dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia teule si lengo la utafiti wetu, utafiti wa Katola (k.t.j) una mchango na utafiti wetu kwa kuwa ulitusaidia kubaini dhuluma zinazofanyiwa wanawake na jinsi zinavyohamishiwa kwa wanaume huku wataalamu na wahakiki

wakilipuuza jambo hili. Utafiti huu unahusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya teule na ulitarajiwa kutoa matokeo tofauti kwa kuwa kila utanzu una sifa zake bainifu.

Maombe (2011) alifanya utafiti kuhusu ukombozi wa mwanamke katika riwaya za Habwe. Anasema kuwa, suala kuhusu ukombozi wa mwanamke dhidi ya ukandamizaji wa mwanaume limeshughulikiwa na watafiti wengi. Anaendelea kuhoji kuwa, watafiti hawa wameangazia jinsi mwanamke anavyokandamizwa na mwanaume kupitia vyombo vya utamaduni kama vile; asasi za ndoa, dini, taasisi za elimu, itikadi na mila za jamii. Hata hivyo, mada hii ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu hatukushughulikia masuala ya wanawake. Utafiti wa Maombe una mchango katika utafiti huu kwa kuwa unatoa mwanga kwamba masuala ya jinsia ya kike yameangaziwa huku ya jinsia ya kiume yakipuuzwa.

Utafiti wa Obure (2012) ulihusu dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya *Rosa Mistika* na *Tumaini.* Anasema kuwa, kila uchao waandishi wa riwaya, tamthilia, na tanzu zingine za fasihi wameangazia suala la dhuluma kwa vijana wa kike katika tungo zao. Ingawa hatukushughulikia masuala kuhusu wanawake, kazi ya Obure ilituwezesha kuelewa kuwa, tafiti tangulizi zina pengo kwa sababu zilishughulikia masuala kuhusu jinsia ya kike kwa upana na masuala kuhusu jinsia ya kiume yamesahaulika. Utafiti wetu unahusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya zilizoteuliwa.

Kipyegon (2013) alifanya utafiti kuhusu nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani.* Alibaini kuwa, masuala yanayowahusu wanawake ni muhimu na huibua hisia tofauti katika jamii hasa wakati huu ambapo wanawake wanaanza kujitambua na kushiriki kikamilifu katika ujenzi mpya wa jamii. Anaeleza kuwa, kuna kazi nyingi zilizotafitiwa kuhusu wanawake. Kazi hizi zimeguza kila utanzu, si riwaya,

si ushairi, si tamthilia, zote zimetafitiwa. Utafiti wa Kipyegon ni tofauti na wetu kwa sababu tulishughulikia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya teule. Hata hivyo, utafiti huu una mchango katika utafiti wetu kwa sababu ulishughulikia suala la jinsia. Utafiti huu ulitupa mwelekeo kubaini kuwa, masuala kuhusu wanawake yameshughulikiwa kwa upana na kuna umuhimu wa kuchunguza upande wa pili wa kijinsia.

Kilonzo (2015) alifanya utafiti kuhusu ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Anaeleza kuwa, suala la mwanamke limetafitiwa na watafiti wengi. Uchunguzi wa watafiti wengi umejikita katika nafasi ya mwanamke, utambulisho wa mwanamke, ukombozi wa mwanamke, taswira ya mwanamke miongoni mwa masuala mengine. Kilonzo (k.t.j) anasema kuwa tafiti tangulizi hazikushughulikia suala hili la usawiri wa wahusika wa kiume, bali zimeshughulikia jinsia ya kike kwa kiasi kikubwa na kuipuuza ile ya kiume. Japo utafiti wa Kilonzo ni tofauti na wetu kwa kuwa hatukushughulikia ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia, maelezo yake yana uhusiano na utafiti wetu. Aidha, utafiti wake ulikuwa wa manufaa kwetu kwa sababu ulidhihirisha kuwa jinsia ya kiume imepuuzwa kiutafiti.

Utafiti wa Suleimani (2015) ulihusu usawiri wa mwanamke katika muziki wa nyimbo za dansi: Mifano katika nyimbo za Mbaraka Mwinshehe. Anasema kuwa, taswira ya mwanamke imeshughulikiwa na wachunguzi na wataalamu mbalimbali katika vipengele vya fasihi hususan fasihi andishi. Utafiti wa Suleimani (k.t.j) unahitilafiana na wetu kwa njia kadhaa. Kwanza, mada yake inahusu usawiri wa mwanamke katika muziki wa nyimbo za dansi, tofauti na utafiti huu unaohusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya teule. Aidha, Sulemani alitumia nadharia ya ufeministi lakini tulitumia nadharia ya uhalisia. Hata hivyo, tafiti hizi zina uhusianao kwa sababu

yaliyoshughulikiwa ni masuala ya kijinsia. Utafiti wa Suleimani ulikuwa muhimu kwa kazi yetu kwa sababu ulitusaidia kuelewa kuwa nyingi za tafiti tangulizi zina pengo kwani zinashughulikia masuala ya wanawake pasi kuangalia upande wa jinsia ya kiume.

Utafiti wa Rymond (2016) ulihusu usawiri wa mwanamume katika methali za Kimeru nchini Kenya. Anaeleza kuwa, usawiri wa mwanamume katika methali za Kimeru haujawekwa bayana na tafiti tangulizi. Utafiti wa Rymond ni tofauti na wetu kwa kuwa, hatukushughulikia usawiri wa mwanamume katika methali za Kimeru. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa na mchango katika utafiti huu kwa kuonyesha kwamba kuna mambo ambayo hayajawekwa bayana kuhusu masuala ya jinsia ya kiume. Utafiti wa Rymond uliongozwa na nadharia ya Ubabedume ilhali utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Hata hivyo, utafiti wa Rymond una mchango katika utafiti wetu kwa kuwa alishughulikia usawiri wa jinsia ya kiume kama ilivyo katika utafiti wetu.

Fakih (2017) alishughulikia kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si Mbali Tena.* Utafiti huo unaonyesha kwamba, katika kazi za fasihi, mada ya usawiri na nafasi ya mwanamke imefanyiwa utafiti na wataalamu mbalimbali. Mfano wa kazi hizo ni; Chacha (1986), Nungo (1985), Momanyi (1998), Lughano (1989), Waruguru (2013), Jilala (2008) na wengineo. Fakih (k.t.j) anasema kuwa kwa upande wa fasihi ya Kiswahili, kuna umuhimu mkubwa wa kuchunguza usawiri wa mwanamke ingawaje watafiti wengi wamejitahidi kulitafitia suala hili katika tanzu kama fasihi simulizi, ushairi, tamthilia na riwaya. Utafiti wa Fakih una uhusiano na utafiti wetu kwa sababu alitumia utanzu wa riwaya na alishughulikia suala la jinsia. Hata hivyo, utafiti wa Fakih ni tofauti na wetu kwa sababu hatukushughulikia masuala ya wanawake. Utafiti huu una mchango katika utafiti wetu

kwa kuwa, unaonyesha kuwa masuala kuhusu wanawake yameshughulikiwa katika tafiti mbalimbali na yanaendelea kushughulikiwa hata sasa. Utafiti wa Fakih unaibua uhaba wa tafiti kuhusu uchunguzi wa wa wahusika wa kiume katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*.

Utafiti wa Saro (2017) ulihusu usawiri wa mwanamke katika riwaya: Mfano katika riwaya ya *Utengano* anaonyesha kuwa, uchunguzi wa taswira ya mwanamke katika kazi ya fasihi umejitokeza tangu pale tu mwanadamu alipoumbwa na kuanza kuandaa na kushiriki katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Saro (k.t.j) anasema kuwa, watafiti kadhaa wamehakiki kazi za fasihi na kueleza taswira ya mwanamke kwa jumla. Utafiti wa Saro ulihusishwa na riwaya na suala la jinsia kama ilivyo katika utafiti wetu. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu ilishughulikia usawiri wa mwanamke ambalo halikuwa lengo la utafiti wetu. Kazi ya Saro ilitupa kuelewa kuwa, masuala kuhusu wahusika wa kike yamekuwa yakishughulikiwa tangu mwanadamu alipoumbwa, na bado linaendelea kushughulikiwa. Usawiri wa wahusika wa kiume ndilo suala la msingi katika utafiti wetiu katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*.

Utafiti wa Samuel (2018) ulihusu ukandamizaji wa jamii unavyodhihirika katika uandishi wa Clara Momanyi na Sheila Ryanga. Anaeleza kuwa, matini za waandishi zinazoitetea nafasi ya mwanamke zimechapishwa kwa wingi. Mfano wa matini hizi ni; *Mama Eee!* (Ari Katini Mwachofi: 1987) *Nguzo Mama*, (Peninah Muhando: 1982) *Tumaini*, *Nakuruto*, (Clara Momanyi: 2006, 2009). Matini hizi zinajikita katika kupigania kazi za mwanamke na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutombagua mwanamke kwa misingi ya uana. Pia, tafiti nyingi zimefanywa kuhusu jinsi mwanamke

anavyosawiriwa katika jamii. Utafiti wa Samuel ni tofauti na wetu kwa sababu alitumia nadharia ya Jinsia - Hakiki ilhali utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Hata hivyo, kazi hii ulitufahamisha kuwa, masuala kuhusu jinsia ya kike yamepewa kipaumbele huku masuala kuhusu jinsia ya kiume yakikosa kushughulikiwa kwa kina. Utafiti wetu ulichunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi.*

Mohammed (2018) alichunguza usawiri wa mhusika mwanamume katika riwaya za Kiswahili: *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie.* Katika uchambuzi wake ameeleza nafasi ya mwanamume katika riwaya hizi na pia, kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika mwanamume katika riwaya hizo. Utafiti wa Mohammed una uhusiano na utafiti huu kwa sababu unahusu usawiri wa mhusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili na pia, unahusishwa na utanzu wa riwaya kama ilivyo katika utafiti wetu. Utafiti huu ulichangia katika kuonesha jinsi wahusika wa kiume wanavyosawiriwa. Mohammed (k.t.j) alitumia nadharia mbili ambazo ni; sosholojia na fasihi na saikolojia changanuzi ilhali, utafiti huu ulitumia nadharia ya uhalisia katika kuchunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Kwa hivyo, utafiti uliweza kuibua matokeo tofauti na ya utafiti wa Mohammed.

Mohammed (k.t.j), akimrejelea Mulokozi (1989, 1996 na 2002) anasema kuwa, katika ulimwengu wa riwaya ya Kiswahili na fasihi, limekuwa kama jambo la kawaida kuona watafiti wengi wakichunguza nafasi ya mwanamke zaidi kuliko nafasi ya mwanamume. Jambo hili huenda limetokana na ukweli kwamba, wanawake wamekuwa wakipiganiwa haki zao ili kuwafanya wawe sawa na wanaume katika nyanja mbalimbali. Nyanja hizo ni pamoja na, uongozi, elimu, kumiliki mali, ajira, n.k. Anasema kuwa hali hii imefanya ukweli uliokuwa wazi kusahaulika. Ukweli huo ni

nafasi ya mwanamume katika riwaya ya Kiswahili. Maneno haya yalimchochea mtafiti kutaka kuchunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi.*

Utafiti wa Wanjiku (2018) ulihusu mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya za Said. A. Mohamed *Utengano* (1980) na *Dunia Yao* (2006).” Anaeleza kuwa, wahusika ni nguzo muhimu sana katika kazi yoyote ile, iwe fasihi au matini ambazo ziliandikwa na wasanii.

Ijapokuwa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu usawiri wa wahusika katika fasihi ya Kiswahili, watafiti wengi zaidi wamejikita katika wahusika wa kike. Maandiko haya yanadhihirisha pengo la maarifa ambalo utafiti huu umeweza kulishughulikia. Utafiti wa Wanjiku (k.t.j) una mchango katika utafiti wetu kwa sababu alitumia nadharia ya uhalisia na utanzu wa riwaya kama ilivyo katika utafiti huu. Aidha, utafiti wa Wanjiku unatofautiana na utafiti huu kwa sababu mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya za Said. A. Mohamed halikuwa lengo la utafiti wetu. Hata hivyo, kazi hii ilimsaidia mtafiti wa kazi hii kubaini jinsi ambavyo tafiti zilizofanywa kuhusu mhusika mwanamke zinavyomchora mwanamume. Utafiti wetu ulijikita katika kuchunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*.

Utafiti wa Atieno (2019) ulishughulikia utambulisho wa jinsia katika *Maumbile si Huja* na *Paradiso.* Anaeleza kuwa, tafiti kadha za hapo awali zimeshughulikia masuala ya wanawake ya ukombozi, unyanyaswaji na dhuluma wanazopitia katika jamii za kiafrika na kupuuza masuala ya wanaume. Anasema kuwa, tafiti hizi zina pengo ambalo linastahili kujazwa na watafiti wengine wa fasihi ya Kiswahili. Atieno (k.t.j) anasema kuwa, jamii imepuuza jinsia ya kiume kutokana na fikra kuwa ina, uwezo wa kujitetea

pamoja na kukabiliana na changamoto inayokumbana nazo. Hata ingawa mada ya Atieno ni tofauti na yetu, maelezo yake yana uhusiano wa karibu na utafiti wetu. Utafiti huu ulitupa mwelekeo wa kuchunguza jinsia ya kiume ambayo inaonekana kupuuzwa katika jamii. Utafiti wetu unahusu, usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya teule.

Utafiti wa Bayyo (2020) ulihusu usawiri wa jinsi ya kiume katika riwaya za Shafi Adam Shafi. Amebaini kuwa, jinsia ya kiume inasawiriwa kama jinsia yenye ujasiri, uvumilivu, msimamo, uongozi, wanamapinduzi na katili. Aidha, amebaini kuwa, jinsia ya kiume inakabiliwa na matatizo kama vile; kukosa elimu, hali ngumu ya maisha, usaliti, kukosa haki na kutenganishwa na familia zao. Kadhalika imebainika kuwa, kuna mbinu zinazotumika na jinsia ya kiume kukabiliana na matatizo hayo. Ingawa mbinu za kukabiliana na changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume si lengo la utafiti wetu na pia hatukutumia riwaya za Shafi Adam Shafi, kazi hii ina mchango katika utafiti wetu kwa sababu inahusu usawiri wa jinsia ya kiume. Kazi hii pia, iliongozwa na nadharia ya uhalisia kama ilivyo katika utafiti wetu. Utafiti wa Bayyo (k.t.j) ulituangazia jinsi jinsia ya kiume inavyosawiriwa katika riwaya za Kiswahili. Hata hivyo, tofauti na utafiti wake, utafiti wetu unahusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*.

Utafiti wa Kanwa (2022) ulihusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Anasema kuwa, baadhi ya wasomi walipendekeza tafiti nyingi zifanywe ili kuangalia upande wa pili wa masuala ya kijinsia kwa sababu mengi yameshatafitiwa kuhusiana na jinsia ya kike. Wasomi hawa ni kama vile; Momanyi, (1998), Kimani, (2003), King'ei, (2002) na Wandera, (2002). Jambo hili limeweka wazi kabisa pengo lililopo ambalo limezibwa na utafiti huu. Kanwa (k.t.j) amechunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya kama ilivyo

katika utafiti wetu. Tofauti ni kwamba, utafiti wake ni linganishi na alitumia nadharia tatu ambazo ni; Ujifuzaji wa Kijamii, Mwanamume Mpya na Uhalisia. Utafiti huu ulichunguza usawiri wa mhusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Kanwa (k.t.j) anaendelea kusema kuwa, tafiti zinazohusu jinsia katika fasihi ya Kiswahili zitaendelea kuwepo katika maisha ya mwanadamu. Hii ni kwa sababu binadamu anaendelea kuwepo.

## 2.2 Makala

Makala ya Mboya (2018) ilihusu dhuluma kama kichocheo cha mzinduko wa wanawake katika riwaya za Kiswahili. Utafiti wake unaonyesha kuwa, wasomi na wahakiki wa kazi za fasihi wameshughulikia suala la dhuluma kwa wanawake na athari zake kwa muda mrefu bila kutoa suluhu. Tafiti za wataalamu hawa ni kama vile Freeman (1975), Lugano (1985 na 1998), Muindi (1990), Rowbotham (1992), Matteru (1992), Wegesa (1994), Corrin (1996), Momanyi (1998), Kimani (2003), Rai (2003), Welchman (2007), Dish (2009). Utafiti wetu ni tofauti na makala ya Mboya kwa sababu masuala kuhusu wanawake si lengo la utafiti wetu. Hata hivyo, Makala hii ina uhusiano na utafiti wetu kwa sababu tulishughulikia masuala ya kijinsia. Makala hii ilikuwa ya manufaa kwetu kwa kuwa kuwa, ilitufahamisha masuala kuhusu wanawake yameshughulikiwa kwa muda mrefu. Hivyo basi, ni wakati wa kuangalia upande wa pili wa masuala ya kijinsia.

Makala ya Mavisi (2018) ilihusu usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya za Zainabu Burhan. Riwaya hizo ni *Mali ya Maskini* (1981), *Mwisho wa Kosa* (1981) na *Kipimo cha Mizani* (2004). Makala hii liongozwa na nadharia ya Unisai wa Kiafrika inayoeleza matatizo yanayowakabili wanawake wa Kiafrika, kinachosababisha matatizo hayo, na jinsi wanavyoweza kujiepusha nayo. Mavisi (k.t.j) anasema kuwa,

jamii imewaweka wanawake katika nafasi ya pili baada ya wanaume, jambo ambalo limesababishwa na mfumo dume, mazingira na malezi yanayowafanya wanawake hawa kuikubali hali yao. Utafiti wetu unatofautiana na makala ya Mavisi kwa sababu, alitumia nadharia ya Unisai wa Kiafrika ila katika utafiti wetu tuliongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo inachangia kuibua mambo tofauti. Ingawa usawiri wa wahusika wa kike si lengo la utafiti wetu, makala ya Mavisi ilitufahamisha kuwa, jinsia ya kiume hulaumiwa kwa matatizo yanayowakabili wanawake. Suala la msingi katika utafiti huu ni kuchunguza jinsi wahusika wa kiume wanavyosawiriwa katika riwaya teule.

Makala ya Wasike (2020) ilihusu mwanamke wa kisasa katika insha za kifasihi Magazetini: Mtazamo wa nadharia ya Upalizi. Amebaini kuwa, mkabala wa kuumeni umetawala jamii nyingi za kilimwengu kwa muda mrefu. Wasike (k.t.j) anasema kuwa suala hili limesababisha kupuuzwa kwa haki za wanawake kama viumbe kamili. Wasike akimrejelea Momanyi (1998) anasema kuwa, ukandamizaji wa wanawake katika jamii unatokana na mfumo unaodhibitiwa na wanaume. Ingawa masuala kuhusu wahusika wa kike si lengo la utafiti wetu, maelezo ya Wasike yana tija katika utafiti wetu kwani yalituongoza kuelewa kuwa, tafiti nyingi zimeegemea kwenye aina za dhuluma na matatizo yanayowakumba wahusika wa kike. Jambo hili linaathiri jamii kwa kuipa mtazamo kuwa jinsia ya kiume haikabiliwi na matatizo, bali ndiyo inayosababisha matatizo kwa jinsia ya kike. Maneno haya yalimtia ari mtafiti kuchunguza zaidi kuhusiana na namna wahusika wa kiume wanavyosawiriwa katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*.

Katika makala ya Mwita (2021) usawiri wa wahusika wa jinsia ya kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* anaeleza kuwa, kujikita katika tafiti kuhusu wanawake pekee kumekashifiwa na wataalamu wengi waliobainisha kuwa, kuzungumzia nafasi ya

mwanamke tu kana kwamba ni wanawake peke yao waishio duniani ni upotoshi mkubwa. Makala hii ilitupa mwanga kuhusiana na masuala ya jinsia ya kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Aidha, makala hii ilikuwa ya faida kwetu kwa sababu ilitupa kuelewa jinsi ambavyo wahusika wa kiume wanavyosawiriwa katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Makala hii ina uhusiano na mada ya utafiti huu kwa sababu inashughulikia riwaya ya *Chozi la Heri* kama ilivyo katika utafiti wetu. Isitoshe, makala ya Mwita iliongozwa na nadharia ya uhalisia kama ilivyo katika utafiti wetu, ambapoilitufahamisha zaidi kuhusu nadharia hii. Hata hivyo, makala hii inatofautiana na utafiti wetu kwa kuwa, tunashughulikia riwaya mbili ambazo ni *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*.

**2.3 Vitabu**

Kwa mujibu wa Ndungo na Wafula (1993), kuchunguza nafasi ya mwanamke zaidi kuliko mwanamume kumetokana na ukweli kuwa, kumekuwa na mwamko wa kupigania haki za wanawake kwa lengo la kukuza usawa dhidi ya utawala wa wanamume katika nyanja za uongozi, kumiliki mali, elimu, ajira n.k. Ingawa masuala kuhusu wanawake si lengo la utafiti wetu, maelezo ya Ndungo na Wafula yana mchango katika utafiti huu kwa kuwa yanaonyesha kuwa, nafasi ya mwanamke imechunguzwa sana kuliko nafasi ya mwanaume katika fasihi ya Kiswahili. Hali hii ilimchochea mtafiti kufanya utafiti huu.

Kulingana na Ntarangwi (2004), wanawake kupiganiwa haki zao ili kuwafanya sawa na wanaume ni njia nzuri ya kumkomboa mwanamke kutokana na hali ngumu ya maisha inayomkabili kutokana na mfumo dume ulipokithiri katika jamii. Ingawa utafiti wetu haukulenga masuala ya wanawake kwa jumla, utafiti wa Ntarangwi ulikuwa na mchango katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu yalitufahamisha kuwa, mwanamke

anaendelea kupiganiwa ili kukombolewa kutokana na hali ngumu ya maisha huku mwanamume akisahaulika.

## 2.4 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Kutokana na mapitio ya maandiko, inabainika kwamba kuna ukosefu wa maarifa kuhusu usawiri wa jinsia ya kiume katika fasihi ya Kiswahili. Kwanza, masuala kuhusu jinsia ya kiume hayajashughulikiwa kwa wingi ilhali masuala kuhusu jinsia ya kike yamechunguzwa kwa wingi. Pili, changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume hazijachunguzwa kwa wingi. Mwisho, athari za changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume na jamii yake hazijachunguzwa kwa wingi. Mapengo haya yalizibwa na utafiti huu. Utafiti huu ulichunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya teule. Aidha, tulibainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule. Halikadhalika tulionyesha namna changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake.

## 2.5 Mtazamo wa kinadharia

Kulingana na maelezo ya Njogu na Chimera (1999), nadharia za uhakiki wa fasihi ni miongozo inayomsaidia msomaji na mhakiki wa kazi ya fasihi kuifafanua kazi ile kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na uchunguzi wa kifasihi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia hii ilianza huko Ufaransa ambako walitumia dhana ya uhalisia kuelezea kazi ya sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu jinsi walivyo na uigaji wa mazingira wanamopatikana wanadamu (*Encyclopedia Britannica Volume 9*). Katika karne ya 19, istilahi uhalisia huelekezwa kwa sanaa za mchoraji Mfaransa ajulikanaye kama Gustave Flaubert ambaye michoro yake iliwatia kiwewe Wafaransa. Alisema kuwa, uhalisia ni kuondoa ufaraguzi na

kuangalia dunia kwa uamilifu na usawa kutokana na tajriba na uzoefu wa kibinafsi. Tapo la uhalisia lilizuka kama vuguvugu la kuupinga mtazamo wa kilimbwende ambao ulishindwa kutatua matatizo ya wanajamii kwa sababu uliishia kwenye fikra za kinjozi. Ulimbwende ulihusu mambo yasiyowezekana katika ulimwengu halisi. Hata hivyo, uhalisia katika kazi za sanaa ulipendekezwa na Plato takriban miaka mia nne (400) kabla ya Masihi. Plato alisema kwamba, msanii aandike au kuchora yale mambo halisi yanayopatikana katika jamii (Gilbert, 1962).

Ilipendekezwa matumizi ya "uhalisia" yaeleze kazi ya kifasihi inayouwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inavyochochewa waziwazi na hali aliyomo, (Wamitila, 2002).

Nadharia hii inadai ya kwamba, matukio yanayosimuliwa yanakaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Tapo hili linapingana na aina yoyote ya majaribio, hivyo basi mwandishi analazimika kuuteua mtazamo wa kisimulizi ambao utamwezesha kuyawasilisha maisha kwa "usahihi". Mulokozi (2017) anasema ya kwamba fasihi iyasawiri maisha kama yalivyo bila kupotosha wala kutia chumvi huku ikijikita katika kuonyesha mahusiano na migongano ya kijamii, matatizo na pia matamanio ya mtu wa kawaida ndani ya jamii.

Georg Lukacs (1972) ni mmoja kati ya wataalamu wanaohusishwa na dhana hii. Kulingana na maelezo ya Wamitila (2003), Njogu na Wafula (2007), lengo kuu la nadharia ya uhalisia lilikuwa ni kuupinga mtazamo wa kiulimbwende ambao ulishindwa kutatua matatizo ya watu kwa sababu ulikuwa ukiishia kwenye fikra za kinjozi. Kulingana na maelezo ya wataalamu hawa, nadharia ya uhalisia hakiki inahusishwa na mihimili ifuatayo;

i) Fasihi inalenga kuisawiri picha halisi ya jamii.

ii) Fasihi inalenga kueleza mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha.

iii) Fasihi iwaonyeshe wahusika kama walivyo katika muktadha wa historia ya jamii.

iv) Fasihi iweze kuonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu, yaani mwanadamu atakuwa mshindi wa matatizo yanayomkabili.

Mihimili hii ilitumika katika ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Aidha, mihimili hiyo ilitumika katika lengo la kuchunguza jinsi mhusika wa kiume anavyosawiriwa katika riwaya teule. Pia tuliitumia mihimili hiyo katika lengo la kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule. Mwisho, tuliitumia mihimili hiyo katika kuonyesha namna changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake.

**2.6 Hitimisho**

Sura hii, imebainisha maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti huu. Tumepitia kazi tangulizi zinazohusu masuala ya kijinsia katika fasihi ya Kiswahili. Kazi hizi zimegawanywa kwa mujibu wa tasnifu na makala na vitabu. Sura hii pia, imefafanua nadharia ya uhalisia ambayo ilitumika katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Utafiti huu unahusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Sura hii ya tatu imeshughulikia vipengele saba vya kiutangulizi. Vipengele hivyo ni pamoja na; eneo la utafiti, muundo wa utafiti, usampuli, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

## 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na mtandaoni, ambapo mtafiti alisoma matini ambazo zinahusu riwaya zilizoteuliwa, ili kuchunguza jinsi wahusika wa kiume wanavyosawiriwa katika riwaya za Kiswahili. Uchambuzi huu ulihusisha riwaya za *Chozi la Heri* (2017) na *Nguu za Jadi* (2021). Halikadhalika, maandishi yoyote yanayohusiana na mada ya utafiti yalisomwa ili kupata data ya kutosha kuhusiana na usawiri wa wahusika wa kiume.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Kama anavyopendekeza Kothari (2016) kuwa, utafiti wa kimaelezo ni mtazamo unaochunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa. Data ilikusanywa, ikachanganuliwa na mwisho kuwasilishwa kimaelezo.

### 3.3 Sampuli

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003) katika kitabu chao cha *Research Methods,* sampuli ni vijisehemu vidogo vya idadi jumla ya utafiti. Kimalu na Marimba (2014) katika kitabu chao cha *Research Methods* wanaeleza kuwa, sampuli ni kundi dogo la watu binafsi, matukio na vitu vinavyopatikana katika idadi halisi ya utafiti.

#### 3.3.1 Uteuzi wa Sampuli

Fasihi andishi ina tanzu mbalimbali ambazo ni; riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Hata hivyo, utafiti huu ulishughulikia utanzu wa riwaya pekee. Senkoro (1982) anasema ya kwamba, riwaya ni kisa changamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui. Utanzu wa riwaya ulichanguliwa kwa sababu una mawanda mapana yaliyoweza kutosheleza malengo na kujibu maswali ya utafiti huu. Kuna riwaya nyingi zilizoandikwa ulimwenguni. Aidha, Assumpta Matei na Clara Momanyi wameandika kazi nyingi za fasihi. Riwaya zingine zilizoandikwa na Clara Momanyi na Assumpta Matei kama vile *Tumaini* (2006) na *Nakuruto* (2009) hazikushughulikiwa katika utafiti huu. Riwaya zilizotumika katika utafiti huu ni *Chozi la Heri* (2017) na *Nguu za Jadi* (2021). Riwaya hizi mbili ziliteuliwa kimaksudi kwa sababu tulihitaji riwaya za kuanzia miaka ya 2017 na kuendelea zilizoandikwa na mwandishi yeyote awe wa kiume au wa kike, ambazo zinamsawiri mhusika wa kiume katika nyanja mbalimbali za maisha.

### 3.4 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Tafiti za kitaaluma huwa na data za aina mbili, data ya msingi na ya pili. Furlong (2000), Taherdoost (2021) na Sardana na wenzie (2023) wanaeleza kuwa, data ya msingi ni ile inayokusanywa kwa mara ya kwanza na

haijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kwa matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza. Katika utafiti wetu, tulikusanya data ya msingi katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi.*

Kulingana na maelezo ya Bryaman (2004), data ya pili ni ile iliyokwisha kukusanywa na watafiti wengine kwa kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti, majarida, makala, vitabu na tovuti kwa ajili ya kutumika kama marejeleo katika maktaba mbalimbali. Katika utafiti huu, mtafiti alikusanya data ya upili kwa kusoma maandishi yoyote yanayohusiana na mada kwa mfano vitabu, majarida, Makala, tasnifu na kadhalika. Tuliyoyapata tuliyarekodi katika kitabu kabla ya uchanganuzi.

### 3.5 Vifaa vya Kukusanyia Data

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na ulitumia vifaa mbalimbali katika ukusanyaji wa data. Daftari na kalamu zilitumika kuandika data zinazohusiana na mada ya utafiti huu. Vifaa hivi viliufaa utafiti huu kwa sababu ni vyepesi, hubebwa kwa urahisi na havihitaji utaalamu wa kuhifadhi.  Kompyuta ilitumika kwa kiwango kikubwa kuchapa kazi ya utafiti huu kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

### 3.6 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data

Baada data kukusanywa, ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo. Data hiyo ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Kwanza, mtafiti alisoma riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*, na kuchunguza jinsi mhusika wa kiume anavyosawiriwa. Aidha, mtafiti alibainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule. Mwisho, mtafiti alionyesha namna changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake. Mtafiti

alidondoa na kuyanakili maelezo hayo kwenye kompyuta. Baada ya kudondoa data iliwasilishwa kimaelezo.

### 3.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia vipengele mbalimbali vya mbinu za utafiti. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni pamoja na; eneo la utafiti, muundo wa utafiti, sampuli, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, vifaa vya kukusanyia data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

## 4.0 Utangulizi

Utafiti huu unahusu usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Utafiti huu ulinuia kutimiza malengo matatu ambayo ni; kwanza, kuchunguza jinsi mhusika wa kiume anavyosawiriwa katika riwaya teule. Pili, kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule na mwisho, kuonyesha namna changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake. Hivyo, sura hii inawasilisha data ya utafiti huu pamoja na kufanya mjadala kulingana na malengo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Sura hii imegawanywa katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa sura hii. Sehemu ya pili inahusu ubainishaji wa usawiri wa mhusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Sehemu ya tatu imebainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule. Sehemu ya nne inahusu ubainishaji wa namna changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake katika riwaya zinazohusika. Sehemu ya mwisho ni muhtasari wa sura ya nne.

## 4.1 Usawiri wa Mhusika wa Kiume katika Riwaya Teule

Riwaya teule zimemjadili mhusika wa kiume kama mhusika mkuu na wa kihalisia katika masimulizi yake. Katika riwaya hizi, mhusika wa kiume amesawiriwa katika namna tofauti tofauti kama vile; aliyetelekezwa katika jamii, aliyekosa matumaini, aliyekosa nafasi katika jamii, mvumilivu, mlevi, mwenye msimamo imara, mtetezi wa haki, jasiri, mwenye bidii n.k.

### 4.1.1 Mwanamume aliyetelekezwa katika Jamii

Katika riwaya zinazotafitiwa, mhusika wa kiume amepuuzwa na kutelekezwa katika jamii. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya *Chozi la Heri* kupitia kinywa cha Tetei, ambapo mwandishi anasema kuwa, jamii ya Wahafidhina inaipa kipaumbele pamoja na kuitetea jinsia ya kike, huku hukumu ya kifo ikipitishwa dhidi ya mwanamume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake. Inaelezwa kuwa, hata haki ya mtu kuhusiana kimapenzi na mkewe imebatilishwa na siasa hii ya usawa wa jinsia. Kupitia kinywa cha mwanaharakati Tetei, mwandishi anadhihirisha utelekezaji kwa jinsia ya kiume anaposema:

> "Almuradi anga nzima imehanikiza vilio vya kumkinga mwanamke. Lakini ni wangapi wanaokumbuka kuwa hata maghulamu wanalawitiwa? Ni wangapi wanaowatetea mamia ya wanaume ambao wanateseka katika ndoa kutokana na mapigo na dhiki za kisaikolojia kutoka kwa wake zao?" (uk. 17).

Kutokana na dondoo hili, tunakubaliana na kauli ya Mohammed (2018) kuwa, wanawake wamekuwa wakipiganiwa haki zao ili watendewe sawa na wanaume katika nyanja mbalimbali. Jambo hili limesababisha kusahaulika kwa jinsia ya kiume katika jamii ya sasa.

Halikadhalika, katika riwaya ya *Nguu za Jadi,* mhusika wa kiume amechorwa kama mtu aliyetelekezwa na kutothaminiwa na yeyote. Mhusika Mangwasha katika riwaya ya *Nguu za Jadi* anasema kuwa, amedurusu maandiko mengi ambayo yanamfunza mtoto wa kike jinsi ya kuwa mwanamke na jinsi ya kutangamana na mazingira yake. Hata hivyo, amegundua kuwa kuna machache mno yanayomfunza mtoto wa kiume jinsi ya kuwa mwanaume. Kauli hii inadhihirisha kuwa, mtoto wa kiume amepuuzwa na kutelekezwa na jamii yake katika malezi kwa kuwa, baba hayupo kumwelekeza jinsi

ya kuishi na kukabiliana na changamoto anazokumbana nazo katika maisha. Hali hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Mangwasha alitambua kuwa katika jamii yake, hakuna dira mahususi ya kumwongoza mtoto wa kiume. Dira hiyo ni mzazi wake wa kiume. Aghalabu huyu hayuko au hata hajulikani. Hivyo, hapati mafunzo yoyote kutoka kwake. Hata akiwepo, hana wasaa wa kumfunza lolote la maana (uk. 138).

Vilevile, Mangwasha anaonekana kuhuzunishwa na hali ya mwanamume anayeishi leo. Kupitia mawazo ya Mangwasha mwandishi anasema kuwa, jamii ilimshika mkono mtoto wa kike, ikapiga mbio na mtoto wa kike na kusahau kwamba hata mtoto wa kiume anastahili kushikwa mkono. Kutelekezwa kwa jinsia ya kiume kunadhihirika kupitia mawazo ya Mangwasha anaposema:

> "Ole wako ewe mwanamume uishiye leo. Unayechakura mapipa ili kuizima njaa. Uliikosea nini jamii hata usalie kuwa ombaomba? Umevaa koti kuukuu na umesalia kuwa nyuma kama koti hilo mwanetu. Yu wapi baba aliyekutelekeza? I wapi jamii isiyothamini elimu na utu wako? (uk. 138).

Kwa kurejelea dondoo hapo juu, mawazo haya ambayo yalimjia Mangwasha akilini alipowatazama vijana hao wakihangaika hapa na pale, magunia ya taka za kila aina yakiwa migongoni mwao, ni dhihirisho la kutelekezwa kwa wahusika wa kiume. Isitoshe, kupitia kauli ya Lonare inadhihirika wazi kuwa, jamii imemtelekeza mhusika mwanamume. Mwandishi anasema:

> Jamii hii imewatenga sana vijana wa kiume. Je, familia zitajengwaje ikiwa mume haonekani kuwa mume ndani ya nyumba? (uk.180).

Kwa mujibu wa dondoo hili, mhusika wa kiume ametelekezwa. Aidha, waandishi wameonyesha ukweli wa kauli kuwa, fasihi inatakiwa kutoa picha halisi ya jamii husika. Hii ni kwa sababu kupitia riwaya teule, wametoa picha halisi ya jamii. Inapoelezwa kuwa kunayo maandiko mengi kuhusu jinsia ya kike ila yanayohusu jinsia

ya kiume ni machache, inasadifu hali ilivyo katika jamii ya sasa. Masuala mengi yametafitiwa kuhusu jinsia ya kike huku yanayohusu jinsia ya kiume yakipuuzwa. Mohammed (2018) anaeleza kuwa, kuchunguza nafasi ya mwanamume katika fasihi ni suala geni. Msimamo wetu ni kwamba, mengi yachunguzwe kuhusiana na jinsia ya kiume.

### 4.1.2 Mwanamume aliyekosa Matumaini

Mhusika wa kiume katika riwaya teule anaonekana kukosa matumaini katika maisha. Haya yanadhihirika katika riwaya ya *Chozi la Heri*, ambapo baada ya familia ya Ridhaa kuangamia kwa moto na kufukuzwa kwao, anaingiwa na huzuni na kukosa matumaini. Mwandishi anasema kuwa, baada ya kufukuzwa kutoka katika Msitu wa Heri, Ridhaa, Kaizari na familia yake waliishi katika Msitu wa Mamba kwa miezi sita. Baada ya kipindi hicho, walibahatika kurudi nyumbani kufuatia mradi ulioitwa na wanaharakati wa kupigania haki za kibinadamu: *Operesheni Rudi Edeni*. Hata hivyo, siku hii ya kurudishwa kwao ilikuwa siku ya hisia mseto kwa Ridhaa kwa kuwa hakuwa na familia ya kuendea kwani, wote isipokuwa Mwangeka walikuwa wamekwisha kuangamia. Mwandishi anadhihirisha hali ya ukosefu wa matumaini kwa Ridhaa anaposema:

> Asubuhi hiyo ya kuhawilishwa kutoka Msitu wa Mamba, Ridhaa alihisi kama anayetoka Kanaani kwenda Misri. Hakuwa na matumaini ya maisha bora, hasa alipokumbuka kuwa hakuwa na mwenzi wala mtoto wa kuendea (uk. 34).

Kauli hii ya mwandishi inadhihirisha ukosefu wa matumaini. Vilevile, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume amekosa matumaini. Kwa mfano, idadi kubwa ya vijana wa kiume inaonekana kuzurura mjini bila kufanya lolote la maana. Vijana hawa wanaonekana kupoteza muda wao katika viambaza vya maduka kwa kukosa matumaini. Mwandishi anasema:

> Ukosefu wa matumaini ya kuishi ulianza kuhasiri mifumo ya kijamii (uk. 47).

Dondoo hili linadhihirisha ukosefu wa matumaini. Mwandishi anaeleza ya kwamba, mara nyingi Mangwasha alipotembea mjini alikuwa anatafuta muda wa kuwahutubia vijana wa mtaani na kuwapa matumaini. Inaelezwa kuwa, Mangwasha aliwaona, vijana hao wa kiume kama kizazi kilichopotea. Wengi wa vijana hawa wamekosa matumaini maishani kwa sababu hakuna dira mahususi ya kuwaongoza. Mwandishi anadhihirisha ukosefu wa matumaini anaposema:

> Mara nyingi alipotembea mjini hakusahau kuwahutubia vijana wa mtaani na kuwapa matumaini (uk.137).

Dondoo hili linadhihirisha kukosa matumaini kwa jinsia ya kiume katika riwaya teule. Riwaya teule inaakisi hali halisi ya jamii ya sasa. Nadharia ya uhalisia inadai kuwa, fasihi hulenga kueleza mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Hali ilivyo ndani ya riwaya hii ndivyo inavyoonekana katika jamii ya sasa. Mhusika wa kiume katika jamii amekosa matumaini kwa kuwa, hakuna anayemjali au kumtetea jinsi inavyofanyiwa jinsia ya kike. Tunakubaliana na Atieno (2019) anapoeleza kuwa, kuupuzwa kwa jinsia ya kiume kumechangia hali yao ya upweke kwani hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Mtafiti amegudua kuwa, mwanaume katika jamii amekosa matumaini ya kuishi kwa sababu hakuna anayemjali wala kumtetea. Msimamo wetu ni kuwa, mwanamume atetewe kama ambavyo mwanamke hutetewa katika jamii.

### 4.1.3 Mwanamume Aliyekosa Nafasi katika Jamii

Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, mhusika wa kiume amechorwa kama asiye na nafasi katika jamii ya Wahafidhina. Inaelezwa kuwa, vyombo vya habari na vikao vya wapigania haki vinapigania elimu ya mtoto wa kike, haja ya kuwainua akina mama

kiuchumi huku hukumu ya kifo ikipitishwa dhidi ya mwanaume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake. Isitoshe, wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* hawana nafasi ya kupitisha lolote hata katika vikao vya kitawala. Hali hii inadhihirika kupitia kinywa cha mhusika Tetei:

> Hakuna tuliloweza kulipitisha hata katika vikao vya kitawala bila kusikia kidumtu akisema "Fikiria suala la jinsia" na usidhani ni jinsia nyingine, ni dada zetu tu (uk. 17).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, inadhihirika kuwa, riwaya teule inamsawiri mhusika wa kiume kama asiye na nafasi katika jamii. Hali ilivyo ndani ya riwaya ya *Chozi la Heri*, ndivyo inavyoonekana ndani ya riwaya ya *Nguu za Jadi*. Lonare, mhusika katika riwaya ya *Nguu za Jadi* anapochaguliwa kuwa Mtemi wa Nchi ya Matuo, ana lengo la kubadilisha maisha ya vijana wa kiume ambao anawaona kuwa wametengwa na jamii. Mhusika Lonare anasema:

> Jamii hii imewatenga sana vijana wa kiume. Je, familia zitajengwaje ikiwa mume haonekani kuwa mume kwa nyumba? (uk. 180).

Kwa mujibu wa dondoo hili, mhusika wa kiume amekosa nafasi katika riwaya teule. Nadharia ya uhalisia inadai kuwa, fasihi hulenga kueleza mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Riwaya teule inasadifu uhalisia katika maisha ya sasa, ambapo jamii imemshika mkono mtoto wa kike na kusahau nafasi ya mwanaume. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, jinsia ya kike na ya kiume wapewe nafasi sawa katika jamii

### 4.1.4 Mwanamume kama Kiumbe Mvumilivu

Kwa mujibu wa BAKITA (2017), uvumilivu ni ustahimilivu katika shida, tabu au matatizo fulani. Katika riwaya teule, mhusika wa kiume ameonyeshwa kuwa ni mwenye uvumilivu. Hali hii inaonekana kupitia misukosuko mbalimbali ya kimaisha wanayopitia wahusika wa jinsia hii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Chozi la Heri*,

tunamuona Ridhaa anavyokabiliwa na matatizo mengi na kuyavumilia. Mhusika huyu anaonekana kuvumilia matukio yanayomkumba kijijini mwake, yakiwemo kutotakikana huko, mali yake kuharibiwa, familia yake kuangamizwa huku wakifukuzwa kwao. Halikadhalika, Ridhaa anapofukuzwa kwao anaishi katika hali ya kudhalilika kambini, anapoteza majumba yake katika mikasa tofauti tofauti. Hata hivyo anaikubali hali hii. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Moyo wa Ridhaa ulipiga kidoko, ukataka kumwonya dhidi ya tabia hii ya kulia pindi mtu akabiliwapo na vizingiti (uk.3).

Uvumilivu unaonekana pia wakati Lunga anafutwa kazi katika shirika la Maghala ya Fanaka kwa sababu ya kupinga kitendo cha raia kuuziwa mahindi ya manjano kutoka ughaibuni. Mwandishi anasema:

> Lunga alisoma barua hii mara mbili, alishangazwa na ukosefu wa fadhila wa waajira wake. Licha ya kujitolea kwake usiku na mchana kulijenga shirika hili anasindikizwa kwenda nyumbani kwa mistari michache ya maandishi. Hata hivyo hakujuta kwani alijua alikuwa ametenda wajibu wake (uk.73).

Dondoo hili linadhihirisha sifa ya uvumilivu. Aidha, baada ya mhusika Lunga kufutwa kazi, maisha yake yanabadilika na Naomi anashindwa kuvumilia hali hii ambapo anaondoka na kumwachia watoto. Tunaona Lunga akivumilia maisha ya kuwa baba na mama wa watoto wake kwa muda kabla ya kifo chake. Mwandishi anadhihirisha hili anaposema:

> Lunga alilazimika kuwa baba na mama wa watoto wake na hili usilione kuwa jepesi (uk. 81).

Dondoo hili linadhihirisha uvumilivu wa Lunga. Hata hivyo, yote wanayopitia wahusika wa kiume katika riwaya teule, wanayavumilia wakiamini kuwa maisha yatabadilika na kuwa mazuri. Kwa mujibu wa wafuasi wa nadharia ya uhalisia, fasihi hulenga kutoa picha halisi ya jamii. Kama kawaida, binadamu katika jamii halisi

kukumbwa na matatizo na kuyavumilia akiamini kuwa kuna njia zinazoweza kufanyika kusudi aweze kuyashinda.

Kwa upande wa riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika Lonare anajitahidi kuvumilia na kukabiliana na vitisho vya uongozi wa Mtemi Lesulia anayetaka kuwaangamiza na pia kuangamiza biashara yake. Mwandishi anaeleza kuwa, Lonare hakuwa mfanyakazi katika serikali ya Mtemi Lesulia, lakini alikuwa mfanya biashara hodari na alisifika sana katika biashara ya usafiri. Mara nyingi polisi walimuhangaisha kwa makosa madogo madogo, na wakati mwingine magari yake kuzuiliwa katika vituo vya polisi pasipo na makosa yoyote. Hali hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Siku haikupita bila tatizo kutokea kuhusu magari ya Lonare. Lonare alivumilia yote huku akiamini kwamba fanaka hutokea palipo na ari, bidii na nidhamu (uk.50).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, sifa ya uvumilivu inadhihirika. Isitoshe, Lonare anatekwa nyara, kuteswa na pia maisha yake yanakuwa hatarini. Hata hivyo anayavumilia yote haya na kutia juhudi awezavyo, aghalau aweze kuikomboa nchi yake kutokana na uongozi mbaya wa Mtemi Lesulia. Mwandishi anaeleza kuwa, uchaguzi unapokaribia, Lonare anatekwa nyara na kutoweka ghafla. Habari za kutoweka kwake zinawatia kiwewe wanajamii ya Waketwa. Siku ya uchaguzi inapofika ndipo Lonare anapatikana kando ya nyumba ya Mangwasha akiwa hajijui hajitambui. Mwandishi anaeleza kuwa, Lonare hangeweza kusimama kwa sababu alikuwa amedhoofika na mwili wake ulikuwa na maumivu. Hapo anapelekwa hospitalini na kupata matibabu. Hata hivyo, katika uchaguzi huo ndiye anayeibuka mshindi kama mtemi wa Matuo. Anasindikizwa na wafuasi wake kutoka hospitalini. Ijapokuwa alidhoofika mno, uso wake unajawa na furaha anapopata habari hizo za ushindi. Mhusika huyu anaonyesha uvumilivu wa hali ya juu licha ya kukumbwa na matatizo magumu. Hili linadhihirishwa na maelezo ya mwandishi kuhusu mhusika huyu anaposema:

> Lonare alisaidiwa na Lombo Pamoja na Mashauri kusimama jukwaani kutokana na udhaifu wa mwili (uk. 178).

Kwa kurejelea dondoo hili, inadhihirika kuwa ingawa Lonare alikuwa na maumivu na kukosa nguvu mwilini, anavumilia na kuhutubia umati. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, fasihi inalenga kuitoa picha halisi ya jamii. Ijapokuwa mwanadamu atakumbana na matatizo magumu katika maisha yake, bado kuna njia zinazoweza kufanyika aweze kushinda matatizo haya. Hivyo basi, yanayomkumba mhusika Lonare anakuwa na matumaini kuwa ipo siku atayashinda matatizo hayo. Hali ilivyo ndani ya riwaya teule ndivyo ilivyo katika jamii ya mtafiti. Mwanaume huonekana na kuchukuliwa kuwa mvumilivu. Ingawa mwanamume anakabiliana na changamoto nyingi katika maisha, anastahimili.

**4.1.5 Mwanamume Amesawiriwa kama Kiumbe Mlevi**

Waandishi wa riwaya zinazorejelewa, wamemchora mhusika wa kiume kuwa ni mlevi. Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* hali hii inadhihirika wakati wanaume waliosomea taaluma mbalimbali na ambao wamekosa nafasi za kazi wanaingilia matumizi mabaya ya vileo. Shamsi ambaye ana jina la msimbo Delengua, anaishi katika mtaa wa Kazikeni ambao ni jirani wa mtaa wa Afueni anakoishi Ridhaa. Shamsi amesoma hadi Chuo Kikuu lakini amekosa nafasi ya kazi katika taaluma aliyoisomea, jambo ambalo linamkatisha tamaa na kusababisha kuingilia matumizi mabaya ya pombe. Akawa mlevi wa kupindukia. Unywaji huu wa pombe wa kupindukia unamlazimisha mkewe kumwandama siku ya mshahara ili ajichukulie pesa za matumizi. Mwandishi anasema:

> Anayetazama anamwona mja aliyevaa koti kuukuu lililoning'inia upande mmoja kwa mawe yaliyo mfukoni. Anaimba huku ameshika chupa mkononi (uk. 129).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, inabainika kuwa, Shamsi ni mlevi. Aidha, anaonekana kutembea kurudi nyumbani usiku wa manane akiwa amelewa chakari. Shamsi anaimba wimbo ambao unasikika kama ngonjera. Wimbo huu ni wa kilevi. Ili kudhihirisha hili, mwandishi anasema:

> Ewe chupa wangu ninakuenzi kama mboni ya jicho langu, Mwendani wangu tazama ulivyo shujaa. Asohisi shinikizo la majabali mahangaiko, Ola jinsi unavyonizingira, Maji matamu kunipa yakawa dawa mujarabu… (uk. 129-130).

Kwa kurejelea dondoo hili, inabainika kuwa mhusika wa kiume katika riwaya teule ni mlevi. Vilevile, mwanafunzi wa uzamili ananusurika kifo kutokana na kulewa pombe haramu. Mwandishi anaeleza kuwa, yeye na wenzake wanalewa ili kujisahaulisha changamoto wanazokabiliana nazo kama vile kutopata ruzuku au mikopo. Vijana hawa badala ya kutafuta mbinu nyingine za kujisaidia wamejiingiza katika matumizi mabaya ya pombe haramu, kama ambavyo mwandishi anaonyesha Selume anaposema:

> Na usidhani wanaotumia vileo vibaya ni wale tu wanaotaka kujipurukusha na hali duni chuoni. Wapo wanaovitumia ili kujisahaulisha kusambaratika kwa familia zao. Kuna huyo ghulamu, kipanga anayepokea huduma za ushauri nasaha hapa petu. Yeye alinusurika kifo kutokana na kangara iliyowaua watu sabini mwezi uliopita. Huyu anasema kwamba alianza kuchovya kidogo kidogo akiwa kidato cha pili baada ya aliyemdhania kuwa baba yake kumkana… (uk.142-143).

Dondoo hili linadhihirisha sifa ya ulevi kwa mhusika wa kiume katika riwaya teule. Kwa upande wa riwaya ya *Nguu za Jadi*, Mwandishi amemsawiri mhusika wa kiume kuwa ni mpenda anasa na ulevi. Inaelezwa kuwa, Mrima alikuwa mwanamume mzuri wakati alioana na Mangwasha. Baadaye, alianza kushirikiana na Sagilu huku akipewa pesa za kujistarehesha. Baada ya muda, Mrima anapotelea Ponda Mali na Majaani mahali ambapo palikuwa na walevi wa kila aina kujihusisha na ulevi. Kama inavyoelezwa, Mrima alianza kushiriki ulevi akawa hata anakesha katika vilabu vya

pombe. Watoto wake Sayore na Kajewa, walishinda wakimsumbua mama yao wakitaka kujua aliko baba yao. Mrima anaonekana kushiriki ulevi mpaka anaanza kuhepa kazi na kupotelea ulevini. Mwandishi anasema:

> Alipofika nyumbani, alikuwa hatazamiki. Nguo zilikuwa chafu. Zilinuka uvundo wa pombe. Nywele zake zilitimka. Macho yake daima sasa yalikuwa mekundu kama ya mvuta bangi. Haya yalimshangaza Mangwasha. (uk. 27).

Isitoshe, Mrima anaonekana kufanya usuhuba na wanawake nje ya ndoa, jambo ambalo mkewe anakuja kugundua anapoipata barua ambayo Mrima alikuwa ameandikiwa na mwanamke. Hii ni thibitisho kuwa, Mrima alikuwa tayari ameingia katika anasa. Mwandishi anasema:

> Mangwasha aliisoma tena na tena. Alijua barua hiyo ilitoka kwa mwanamke (uk.77).

Hata hivyo, Mrima anakataa kuuacha ulevi hata anaposhauriwa na mkewe, hadi anapigwa kalamu. Kutokana na ulevi wake, Mrima anaonekana kuokotwa Majaani na wenziwe huku hali yake ikiwa mbaya zaidi. Ilimbidi kupelekwa hospitalini. Mwandishi anasema:

> Waliamua kumwinua. Walimbeba hobelahobela hadi kwenye gari. Alikuwa hatazamiki. Uchafu wa siku nyingi ulimfanya kunuka kama kisonzo (uk. 100).

Tunaelezwa kuwa Majaani palikuwa mahali pa walevi wengi ambao, walishindwa na maisha na kupotelea ulevini na kusahau jamaa zao:

> Hapa pia palikuwa na walevi waliolewa chakari. Baadhi yao walikuwa wanavuta sigara. Wengine waliendelea kubugia pombe katika chupa walizobeba. Wengine tayari walikuwa wametekwa na usingizi (uk.99).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, inaonekana kwamba,riwaya teule inaakisi hali halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu, inamsawiri mhusika wa kiume namna ambavyo anaonekana katika jamii halisi. Katika jamii halisi, wapo walevi ambao matendo yao yanaenda

sambamba na matendo ya wahusika walevi katika riwaya hii. Maoni yetu ni kwamba, hatua ichukuliwe ili kuiokoa jinsia ya kiume inayopotelea ulevini kwa kukosa matumaini.

### 4.1.6 Mwanamume kama Mwenye Msimamo Imara

Msimamo ni hali ya mtu kutetea jambo fulani pasipo kutetereka (BAKITA, 2017). Kuwa na msimamo imara ni mojawapo ya sifa ya jinsia ya kiume ambayo imesawiriwa katika riwaya teule. Wahusika wa kiume wanaonekana kuwa na masimamo katika kupambana na changamoto zinazowakabili. Mhusika Lunga katika riwaya ya *Chozi la heri* ambaye ni mkurugenzi wa kitengo kinachoshughulikia uhifadhi wa nafaka katika Shirika la Maghala ya Fanaka, anasimama imara kupiga kitendo cha raia kuuziwa mahindi ambayo yalikuwa yameagizwa kutoka ughaibuni. Mahindi hayo, licha ya kuwa na rangi ya manjano, kulikuwa na hofu kuwa yameharibika. Huko ughaibuni yalikotolewa mahindi haya, yalisemekana kuwa hatari kwa usalama hata wa panya. Wataalamu wa masuala ya lishe bora walitia sahihi kuidhinisha uuzaji wa mahindi haya baada ya kushinikizwa na vigogo wenye shehena za mahindi haya. Kama inavyoelezwa, Lunga alikuwa na msimamao imara kulipinga tendo hili, ili kuyaokoa maisha ya wanyonge wasio na hatia, jambo ambalo lilisababisha kupoteza kazi yake. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Rai ya wakubwa hata hivyo, haikumnyamazisha Lunga. Aliendelea kulipinga tendo hili kwa jino na ukucha. Alimkabili Mkurugezi wa kitengo cha Uhakikishaji wa Viwango na Ubora wa Bidhaa (uk. 71).

Aidha, mhusika Kang’ata naye anaonekana kuwa na msimamo imara kupinga ubaguzi wa kinasaba. Hili linadhihirika wakati ambapo anaridhia bintiye kuolewa katika ukoo ambao ni hasidi wa ukoo wake, jambo ambalo linajenga uhusiano bora kati ya koo hizi. Inaelezwa kuwa, Waombwe awali walikuwa maadui sugu wa ukoo Anyamvua. Hii

ndiyo sababu ukoo mzima wa Anyamvua ulipinga ndoa ya Lucia kwa jino na ukucha. Ami zake Lucia walikuwa wamekataa katakata kuridhia ndoa yake. Kang'ata naye ambaye ndiye baba yake Lucia anaonekana kuwa na msimamo imara na kuridhia bintiye kuolewa katika ukoo ambao ni hasidi wa ukoo wake. Mwandishi anasema:

> Isingekuwa kwa msimamo wa Kang'ata usiotetereka, Lucia angebakia kuozea kwao bila mume. Ami zake walikuwa wamekataa katakata (uk. 66).

Kwa kurejelea dondoo hili, ni kawaida wanaume kuwa na msimamo usiotetereka katika jamii wanapotaka jambo fulani kufanyika. Aidha, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, sifa ya mhusika wa kiume kuwa na msimamo imara imejidhihirisha kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Ngoswe ambaye ni mwanawe Mtemi Lesulia anakataa katakata kujiunga na kundi la vijana ambao Mtemi Lesulia anawataka kuzua fujo kubwa ili kuharibu zoezi la upigaji kura. Mwandishi anasema kuwa, Mtemi Lesulia alijawa na wahaka mwingi wakati uchaguzi wa mchunjo ulipokaribia. Kwa hivyo, aliamua kucheza karata ambayo ingefisha umaarufu wa Lonare, aliyekuwa mpinzani wa Sagilu.

Inaelezwa kuwa, Mtemi Lesulia aliwaita vijana wachache aliowaamini, wakafika nyumbani kwake. Ngoswe pia alikuwa miongoni mwa vijana hao. Mtemi Lesulia ambaye alikuwa kiongozi katili, aliwapa vifurushi vya pesa na kuwataka wavuruge shughuli ya upigaji kura katika vituo ambavyo vilikuwa na idadi kubwa ya wafuasi wa Lonare. Inaelezwa kuwa, Ngoswe anasimama imara na kutokubaliana na baba yake kuhusu jambo hili. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Ngoswe alisimama na kusema, "Samahani, lakini hii si haki." Kisha alimgeukia babake na kumwambia, "Una hiari kuwatoa mhanga wezangu wakapigwe au hata kuuawa ati kwa sababu mnataka uongozi. Mimi sikubaliani nanyi kamwe (uk. 129).

Kwa mujibu wa dondoo hili, imebainika kuwa, msimamo imara ni mojawapo ya sifa zinazohusishwa na mhusika wa kiume katika riwaya teule. Halikadhalika, Mashauri

anadhihirisha kuwa na msimamo imara kwa kutojihusisha na baba yake anayetenda maovu nchini Matuo. Mwandishi anasema kuwa, miezi minne iliyosalia kabla ya uchaguzi mkuu, haikukosa vitimbi hasa kwa wale waliopoteza viti vyao baada ya uteuzi. Inaelezwa kuwa, kichaa kilimvaa Sagilu akaanza kujizungumzia, kupiga makofi na kucheka peke yake. Watoto walimcheka huku wakimfuata na kumtania. Hata hivyo, Ngoswe anapojulishwa kuwa baba yake ni mgonjwa, anaonyesha msimamo wake kwa kutomjali na hata kumkana baba yake. Mwandishi anadhihirisha hili anaposema:

> Mangwasha alipomjulisha Mashauri kuhusu hali ya babake, huyu alimjibu, “astahili yake. Mkewe akamtafute aliko. Sina baba mie.” (uk. 147).

Kwa mujibu wa dondoo hili, imebainika kuwa, mhusika wa kiume katika riwaya teule ni mwenye msimamo imara. Hata hivyo, ni kawaida wanaume kuwa na msimamo imara wanapotaka jambo fulani kufanyika au kutofanyika.

### 4.1.7 Mwanamume kama Mtetezi wa Haki

Shamsi ambaye ni mmoja kati ya wasimulizi wa hadithi ya *Chozi la Heri*, anaonekana kuwa mtetezi wa haki. Shamsi na wenzake wanalalamikia mishahara duni. Isitoshe, wanalalamikia kutwaliwa kwa shamba lao na kukosekana kwa dawa katika hospitali za wanyonge jambo linalosababisha kifo cha baba yake Shamsi. Mwandishi anaeleza kupitia wimbo wa Shamsi anaposema:

> Kwani hata hakuwepo
> Hospitali ilipokosekana
> Dawa zilipokosekana
> Baba asipate matibabu ya dharura? (uk. 135).

Kwa kurejelea dondoo hili, Wimbo huu unatetea haki za wanajamii. Aidha, yule mja aliyekuwa amevaa shati lililoandikwa “Hitman” mgongoni anaonekana kuwa mtetezi wa haki. Mja huyu alalamikia ukosefu wa ajira, changamoto ambayo imeikumba nchi ya Wahafidhina. Mwandishi anadhihirisha hayo kupitia kinywa cha mja anaposema:

> “Nyamaza wewe! Nyinyi ndio mlioturudisha nyuma miaka yote hii. Mnatuhadaa kwa vishahada mnavyotupa vyuoni; vishahada ambavyo ni laana kwetu, tanuri hasa linalouchoma uwepo wetu. Mtu anahitimu haha digrii tatau kisha anapiga lami kwa miaka kumi…” (uk. 21).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, ni jambo la kawaida wanaume kuwa watetezi wa haki katika jamii halisi. Riwaya ya *Nguu za Jadi* halikadhalika, imemchora mhusika wa kiume kama anayetetea haki za wanajamii. Kwa mfano, Lonare ambaye ni kiongozi wa jamii ya Waketwa na mpinzani wa Mtemi Lesulia, anaonekana kutia juhudi kutetea haki za wananchi wote wa Matuo. Lonare anaonekana kupigania haki za vijana na kuwasomesha watoto wake wote bila ubaguzi wa kijinsia. Aidha, wanajamii wa waketwa wanapochomewa makazi yao na kufurushwa kutoka Matango, Lonare anasimama kidete kuwapigania hata anapeleka kesi mahakamani. Mwandishi anasema:

> Lonare na wenzake walikwenda mbio kuharakisha kesi ya ardhi ya Matango. Mwanasheria Bwana Mwamba sasa alikuwa na ushahidi wa kutosha kuwasilisha mahakama (uk. 93).

Lonare anapochaguliwa kuwa Mtemi wa Matuo, anawahakikishia wanajamii kuwa mashamba na mali yotote ile iliyomilikiwa na watu binafsi kinyume na sheria, watapokonywa na mali hiyo kurudishwa kwa serikali. Maneno haya yanadhihirisha utetezi wa haki kwa wanajamii. Mwandishi anatueleza kupitia kwa maneno ya Lonare anaposema:

> Mafisadi wote waliopora mali ya umma na kukimbilia ugenini tutahakikisha wamekamatwa huko na kurudishwa nchini ili wahukumiwe (uk. 179).

Sauni na Sagura ambao ni marafiki wa karibu wa Lonare, wanaonekana kutetea haki za Waketwa wenzao pale kanisani baada ya kuchomewa nyumba zao na kufukuzwa kutoka Matango. Sauni anauliza ni wapi watapiga kura iwapo hawana makao. Baada ya Waketwa kugundua kuwa Mtemi alitaka kunyakua ardhi yao, Sagura anawahimiza

wenzake na kusema kuwa watapigania haki yao kwa jino na ukucha. Mwandishi anatuonyesha haya kupitia Sagura:

> Tuliamini kwamba tulikuwa tumepata makazi yetu yale kwa njia halali. Mtemi sasa anataka kutumia njia za mkato kutopoka haki yetu. Tunahitaji kumzuia kwa jino na ukucha (uk. 92).

Kwa mujibu wa nukuu hili, riwaya teule inaakisi hali halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu, katika jamii kuna wanaume ambao husimama kidete kutetea wanajamii wenzao dhidi ya dhuluma na mateso wanayoyapata kutokana na uongozi mbaya. Ingawa wanaume wanadhulumiwa na kutelekezwa katika jamii, wanaonekana kutetea haki zao.

### 4.1.8 Mwanamume kama Jasiri

Utafiti huu umebaini kuwa, mhusika wa kiume amehusishwa na sifa ya ujasiri katika maisha. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, Lunga anadhihirisha ujasiri wa kipekee anapomkabili mkurugenzi wa kitengo cha Uhakikishaji wa Viwango na Ubora wa Bidhaa na kupinga uamuzi wa kuwauzia raia mahindi ambayo yangekuwa na athari hasi kwa maisha ya jamii. Lunga hajali matokeo ya tendo lake ambalo linamsababishia kuachishwa kazi. Mwandishi anasema:

> Rai ya wakubwa hata hivyo haikumnyamazisha Lunga. Aliendelea kulipinga tendo hili kwa jino na ukucha. Alimkabili Mkurugenzi wa kitengo cha Uhakikishaji wa Viwango na Ubora wa bidhaa (uk. 71).

Dondoo hili linadhihirisha wazi kwamba, Lunga hakuogopa kutenda wajibu wake hata kama utachangia kufutwa kazi. Aidha, tunamuona Dick ambaye baada ya baba yake kuaga dunia, anatoroshwa na kijakazi Sauna na kupelekwa kumsaidia Buda katika kazi yake ya ulanguzi wa dawa za kulevya. Wakati huu Dick alikuwa mtoto wa miaka kumi aliposhirikishwa katika biashara hii haramu, ambayo ilikuwa imewaingiza wengi

kwenye nyavu na madema ya polisi wakatiwa mbaroni. Mwandishi anadhihirisha hali hii anaposema:

> Kila mara alipopatwa na kiwewe alijiambia “Dickson, wewe jikaze. Mzee wako hayupo hapa, amejipumzikia ahera. Na mama yako hakuwapo tangu hapo” (uk. 119).

Halikadhalika, inaelezwa kuwa, ingawa hapo awali kisa cha kuchomwa kwa Lemi rafikiye na umati uliomdhania kuwa alikuwa mwizi, kinamtia woga na kumfanya kukubali kumlangulia dawa Buda, baadaye anakuja kuwa jasiri na kukabiliana na hali ya ulanguzi. Mwandishi anatuonyesha hili Dick anaposema:

> “Sijawahi kuona maafisa wa usalama kwenye jumba la Buda wakija kuuliza kinachoendelezwa humu. Hata wanaofika humo huingia kwa tabasamu na kutoka kwa vicheko.” Mawazo haya yalimtia Dick ujasiri zaidi akapiga mbizi kwenye biashara hii kwa hamasa na ujana (uk. 123).

Dondoo hili linadhihirisha ujasiri wa Dick. Hata hivyo, Dick aliendelea kukua na kupata nguvu za kukabiliana na ushawishi na vitisho vya mwajiri wake bila kuogopa. Akajifunza mbinu za kujiokoa. Ujasiri wa Dick unaonekana wakati anajinasua kutoka mikononi mwa Buda na kuanzisha biashara yake. Mwandishi anasema:

> Mawazo haya yalimsukuma Dick kufikia uamuzi wa mkataa akajinasua kutokana na kucha za mwajiri wake huyu. Aliacha biashara hii haramu na kuanzisha biashara ya kuuza vifaa vya umeme (uk. 124).

Kwa kurejelea dondoo hili, inadhihirika kuwa, wahusika wa kiume katika riwaya teule wanahusishwa na sifa ya ujasiri. Hali kadhalika, kwa upande wa riwaya ya *Nguu za Jadi*, sifa ya ujasiri inadhihirika wakati ambapo Mashauri anamkabili baba yake bila woga na kumtisha kwamba, angeuanika uovu wake wote kwenye magazeti ambapo umma ungemhukumu. Kama inavyoelezwa, mzee Sagilu ambaye ni baba yake Mashauri, anaendeleza uovu nchini Matuo kwa kuwaharibu wasichana wadogo ambao alifanya uhusiano wa kimapenzi nao. Mwandishi anaeleza kuwa, Mashauri, Lonare

pamoja na wahusika wengine walifanya mpango wa kukomesha uovu huu. Inaelezwa kuwa, Mashauri alifululiza hadi nyumbani kwa baba yake ambapo alimpata sebuleni akifuatilia matukio ya kampeni za uteuzi kwenye runinga. Mzee anapomwona Mashauri anashtuka, kisha anasimama na kumkaribisha kwa furaha. Ujasiri wa Mashauri unadhihirika anaposema:

> "Sikiliza mzee, sikuja hapa kwa wema ndiposa unikunjulie mikono ili kunisahaulisha yaliyopita. Nimekuja kwa shari," Mashauri alitamka bila hata salamu (uk. 144).

Dondoo hili linadhihirisha ujasiri wa Mashauri, kumkabili baba yake mzazi bila kuogopa. Vilevile, ujasiri unadhihirika pale ambapo, Mashauri anaonyesha kutoogopa laana kutoka kwa baba yake. Baba yake anamwambia:

> "Kijana chunga kinywa chako! Nitakulaani."
> "Wewe ndiwe uliyelaaniwa na umma wote wa Matuo."
> (uk. 144).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, imebainika kuwa, mhusika wa kiume katika riwaya teule, amehusishwa na sifa ya ujasiri. Mwanamume katika jamii ya mtafiti hutumainiwa kuwa mtu jasiri. Hali ilivyo ndani ya jamii, ndivyo inavyoonekana katika riwaya teule. Katika maisha ya kawaida ndani ya jamii, mwanamume hutumainiwa kama mtu jasiri ambaye hahusishwi na sifa ya woga hata mbele ya majabali ya maisha. Riwaya teule zimeonyesha wazi ukweli wa kauli kuwa, fasihi ni zao la jamii. Hii ni kwa sababu zimemchora mhusika wa kiume kama ambavyo mwanamume huonekana na anavyotakiwa kuwa machoni mwa jamii.

### 4.1.9 Mwanamume kama Mwenye Bidii

Assumpta katika riwaya ya *Chozi la Heri*, anamsawiri mhusika wa kiume kama binadamu halisi na mwenye bidii katika mambo anayoyafanya. Mzee Mwimo Msubili ni baba yake Ridhaa na babu yake Mwangemi na Mwangeka. Huyu ni mmoja wa

Waafrika waliolazimika kuwa vibarua katika mashamba yao baada ya vishamba kunyakuliwa na wakawa maskwota ambao maisha yao yalitegemea utashi wa Mzungu.

Inaelezwa kuwa, zama hizo hali ilikuwa tofauti. Mzee mwenye wake na wana wengi alihesabiwa kuwa tajiri kweli kweli. Kama anavyoeleza mwandishi, Mzee Mwimo Msubili alikuwa na wake kumi na wawili. Wake hawa hawakuchelea kutimiza amri ya maumbile, walipania kuujaza ulimwengu. Ardhi yake mzee huyu ilikuwa haitoshi kuyalea madume yake ishirini. Mwandishi anasema kuwa, ardhi hii iligawanywa hadi ikawa vikataa, ikalimwa na kupaliliwa hadi ikachoka. Kauli hii inadhihirisha bidii aliyokuwa nayo mzee Mwimo Msubili ili kuhakikisha kuwa, familia yake haijakosa mahitaji ya kimsingi. Inaelezwa kuwa, mzee huyu aliamua kuwahamishia wake wawili wa mwisho katika Msitu wa Heri. Mwandishi anasema:

> Siku hizo ilikuwa rahisi kwa mtu kuwa na mashamba kokote katika eneo lililomilikiwa na kabila lake kwani umiliki wa mashamba ulitegemea bidii ya mtu (uk. 9).

Kauli hii ya mwandishi inadhihirisha kuwa, mzee Mwimo Msubii alikuwa na bidii ya kulima mashamba ili kuhakikisha kuwa familia yake ina chakula cha kutosha. Isitoshe, Ridhaa ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya hii anaonekana kuwa na bidii. Inaelezwa kuwa, anafanya bidii masomoni na kuwashinda wenzake katika shule ya msingi na mwishowe kuhitimu kama daktari. Vilevile, Ridhaa amewekeza katika miradi kama vile ujenzi wa kituo cha afya cha Mwanzo Mpya. Hali kadhalika, amenunua shamba katika Msitu wa Heri akajenga jumba ambalo lilichomwa wakati wa vurugu za kisiasa. Hali hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Alikuwa amesafiri kwa shughuli za ujenzi wa taifa, kama alivyoziita safari zake za kikazi (uk. 14).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, inabainika kwamba, Ridhaa ni mwenye bidii za mchwa katika kazi yake ya kila siku anayoitia “Ujenzi wa taifa”.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume amesawiriwa kuwa mwenye bidii kwa kila analofanya. Inaelezwa kuwa, ingawa Lonare hakuwa mfanyakazi katika serikali ya Mtemi Lesulia, alitia juhudi katika biashara zake, akawa mfanyabiashara mashuhuri. Sifa hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Alisifika sana katika biashara ya usafiri. Mara nyingi alihangaishwa na polisi kwa makosa madogo madogo. Lonare alivumilia yote huku akiamini kwamba, fanaka hutokea palipo na ari, bidii na nidhamu (uk. 50).

Dondoo hili linadhihirisha sifa ya bidii kwa wahusika wa kiume katika riwaya teule. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, mhimili usemao; fasihi iwaonyeshe wahusika kama walivyo katika muktadha wa historia ya jamii, tunaona riwaya teule ikisadifu uhalisi katika maisha. Hii ni kwa sababu, imemsawiri mhusika wa kiume kama kiumbe halisi mwenye tabia halisi za binadamu wa kawaida. Ni kawaida ya mwanamume kuonyesha juhudi katika kufanya mambo fulani. Ingawa mwanamume katika jamii anakabiliwa na vizingiti maishani, anaonekana kutia juhudi ili kujiokoa pamoja na kizazi chake.

### 4.1.10. Mwanamume kama Mlezi Mwema

Waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi* wamemchora mhusika mwanamume kama mlezi mwema. Mfano wa kwanza unaonekana katika riwaya ya *Chozi la Heri* ambapo, licha ya shughuli za kikazi, Ridhaa akiwa nyumbani anatenga muda kucheza na wanawe na pia mjukuu wake Becky. Mwandishi anasema kuwa, Mwangeka alikuwa akimwangukia baba yake akiigiza jinsi ya kupigana masumbwi. Hali hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Mwangeka kwa utundu wake wa kitoto angemnyang'anya stethoskopu yake na kutia kwenye shingo yake yeye Mwangeka kisha anamlaza baba yake juu ya kochi; baba ni mgonjwa wa Dkt. Mwangeka! (uk. 48).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa, Ridhaa ni mlezi mwema. Aidha, Ridhaa anaonekana kucheza na kijukuu chake Becky ambacho kinamwita Babuu, naye Ridhaa anacheka. Mwandishi anaonyesha hali hii anaposema:

> Anawaona wote mbele ya macho yake yaliyojaa mavune. Anamshika mjukuu wake Becky, akimwita, "Babuuu!" (uk. 5).

Isitoshe, Ridhaa anaonekana kuwa mlezi mwema wakati anarudi nyumbani kutoka kazini na kuwapata watoto wake wakiigiza mazishi ya marehemu ndugu yao. Jambo hili linamkasirisha sana na akawaonya. Inaelezwa kuwa, baada ya onyo hili la babake Mwangeka aliapa kuwajibika zaidi, akainamia cha mvunguni katika masomo hadi chuo kikuu ambako alisomea uhandisi. Lunga naye anaonekana kuwa mlezi mwema anapoachwa na mkewe na kuachiwa watoto watatu kuwalea mpaka pale anapougua na kufariki. Inaelezwa kuwa:

> Lunga alilazimika kuwa baba na mama wa watoto wake, na hilo usilione kuwa jepesi (uk. 81).

Mwandishi anasema kuwa, Lunga alikuwa anawalea watoto wake kwa njia nzuri huku akiwahimiza kujiamini. Anawaonya dhidi ya kujishika tama. Mwandishi anatuonyesha haya Mwaliko anaposema:

> Baba alitukataza kushika tama; akisema kuwa kushika tama hukaribisha umaskini (uk. 169)

Kauli hii ya mwandishi inadhihirisha kuwa, mhusika wa kiume katika riwaya teule ni mlezi mwema.

Vilevile, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume amechorwa kama mlezi mwema. Mwandishi anasema kuwa, ingawa Lonare alikuwa mjane, aliwalea watoto wake vizuri na kuwapa elimu bora. Isitoshe, aliwalea watoto katika jamii yake. Mwandishi anasema kuwa, hata Lonare alipoona vitimbi vya mtemi Lesulia kutowaajiri

Waketwa, aliamua kuwapeleka ng'ambo ambako walisomea taaluma mbalimbali. Mwandishi anadhihirisha hili anaposema:

> Lonare alifanya kila juhudi kuona kwamba watoto wa kike na wa kiume hasa katika jamii yake wamesoma. Yeye mwenyewe alizaa watoto watatu, binti mmoja na wavulana wawili. Wote aliwapa elimu sawa. Hakubagua hata mmoja (uk. 50).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, ni dhahiri kuwa mhusika wa kiume katika riwaya teule ni mlezi mwema. Riwaya teule inaakisi hali halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu inamchora mhusika wa kiume kama jinsi ambavyo mwanamume huonekana katika jamii. Mwanamume katika jamii huwa na jukumu la kutunza na kulea familia yake kwa njia inayofaa licha ya changamoto anazokumbana nazo.

### 4.1.11 Mwanamume anayefanyiwa Ukatili

Waandishi wa riwaya teule wamemsawiri mhusika wa kiume kama anayefanyiwa ukatili. Hili linadhihirika katika riwaya ya *Chozi la Heri* wakati ambapo mzee Kedi anasababisha mauaji kwa aila ya Ridhaa. Inaelezwa kuwa, mzee Kedi na Ridhaa walikuwa majirani na marafiki pia. Walikula na kunywa pamoja. Mwandishi anasema kuwa, Ridhaa hakuelewa ni kipi kilichosababisha rafikiye kumfanyia ukatili namna ile. Mwandishi anadhihirisha ukatili anaofanyiwa Ridhaa anaposema:

> Uuuui! Uuuui! Jamani tusaidieni! Uuuui! Uuuui! Mzee Kedi usituue, sisi tu majirani! Maskini wanangu! Maskini mume wangu!" (uk. 3).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, maneno haya yanadhihirisha ukatili mkubwa wa jirani yake Ridhaa, mzee Kedi.

Kwa upande wa riwaya ya *Nguu za Jadi*, Sagilu anawafanyia hila wahusika wa kiume waliomshinda kwa werevu na hata kuwafilisi kabisa kibiashara. Isitoshe, Sagilu

anawaua washindani wake katika biashara, jambo ambalo ni la kushangaza mno. Mwandishi anaonyesha hili anaposema:

> Alikuwa katili kwa wale waliokinzana naye kibiashara. Alijaa ukiritimba na hakutaka wengine wampiku kwa lolote (uk.16).

Dondoo hili ni dhihirisho la ukatili wa hali ya juu. Isitoshe, Sagilu anaendeleza ukatili kwa kuvunja ndoa za wanaume wengine. Ukatili huu unadhihirika wakati anapompokonya mwanawe Mashauri mpenzi wake na kuuvunja uchumba wao bila kujali. Tendo hili linamkasirisha sana Mashauri ambapo anamchukia baba yake maisha yake yote. Mwandishi anadhihirisha hayo anaposema:

> Alimwona babake akishuka kutoka orofa ya juu. Mkononi ameshika cheiya kama mkoba. Walikumbatiana na kunong'onezana maneno ambayo ni wao tu waliyafahamu. (uk. 121).

Hali kadhalika, Sagilu Pamoja na Mtemi Lesulia wanawadhulumu Lonare kupitia kwa vitendo vya kikatili ili kujinufaisha kisiasa. Wawili hawa wanampangia Lonare mauti ili wanufaike kisiasa. Mwandishi anasema:

> Walituma magaidi kumkatizia maisha lakini watu hawa wakamjia Lonare na kumwonyesha malaki ya pesa waliyopewa kumwagamiza (uk. 51).

Nukuu hii inadhihirisha ukatili wa hali ya juu sana, kwa mhusika wa kiume. Katika maisha ya kawaida ndani ya jamii, kuna wanaume ambao hufanyiwa hila na ukatili hata na wanaume wenzao. Hivyo basi, mhusika wa kiume katika riwaya teule amesawiriwa jinsi alivyo mwanamume katika jamii.

### 4.1.12 Mwanamume kama Mwanamapinduzi

Kulinga na TUKI (2013), mapinduzi ni mabadiliko ya haraka ya hali fulani. Mwanamapinduzi au mwanamabadiliko ni mtu yeyote anayetaka kufanyike mabadiliko ya haraka ya hali fulani. Ridhaa ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Chozi la*

*Heri,* anaonekana kuwa mwanamapinduzi. Kama anavyoeleza mwandishi, Ridhaa anapohamia Msitu wa Heri, mzee Kedi anamsaidia kupata shamba ambapo, mwanawe Mzee Kedi kwa jina Mhandisi Kombo anasimamia ujenzi wa jumba la Ridhaa. Inadhihirika kwamba, mkewe Ridhaa na mkewe Mzee Kedi wanakuwa kama ndugu wa toka nitoke. Aidha, Ridhaa anayathamini masomo ya wapwa zake wawili. Tunaona kuwa wakati alipewa shamba hili lilikuwa kama jangwa yaani, eneo hili lilikuwa kame. Ridhaa kama mwanamapinduzi, anahakikisha kwamba kijiji kizima kina maji ya mabomba. Inaelezwa kuwa, eneo hilo ambalo hapo awali lilikuwa kame, anahakikisha kuwa mazingira yameboreshwa kwa kupanda miti, hali ambayo inafanya mvua kunyesha msimu baada ya mwingine. Mwandishi anaonyesha hili kupitia Ridhaa:

> “Mimi binafsi nimefanya juu chini kuhakikisha kijiji kizima kimepata maji ya mabomba. Kalahari sasa imetwaa rangi ya chanikiwiti. Mibambakofi, mivule na miti mingine mingi imepandwa. Mvua inanyesha majira baada ya mengine (uk. 12).

Kwa kurejelea nukuu hii, inadhihirika kwamba, mhusika wa kiume katika riwaya teule ni mwanamapinduzi. Aidha, Ridhaa anajenga kituo cha afya cha Mwanzo Mpya ambacho kinakuwa afueni kwa wahusika mbalimbali. Mwandishi anasema kuwa, Selume anakiona kituo hiki kuwa afadhali mara mia akilinganisha na hospitali ya umma ambako alikuwa akifanya kazi. Kutokana na maelezo haya inaeleweka kuwa, mhusika Ridhaa ni mwanamabadiliko. Mwandishi anaeleza kupitia kinywa cha Ridhaa anaposema:

> “Kwa sasa azma yangu kuu ni kumalizia ujenzi wa kituo cha afya cha Mwanzo Mpya nilichokijenga kwenye lile ganjo letu. Haidhuru kwamba humo ndimo mlimoangamia familia yangu. La muhimu ni kwamba kituo hiki kikikamilika kitawafaa raia wengi ambao hawamudu gharama ya matibabu katika hospitali za kibinafsi na wengine hata hospitali za umma” (uk. 139).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, inadhihirika kuwa mhusika wa kiume katika riwaya teule ni mwanamabadiliko.

Aidha, kwa upande wa riwaya ya *Nguu za Jadi,* Lonare na wanaume wenzake wanaonekana kuleta mapinduzi ya haraka kwa wananchi wa Matuo dhidi ya uongozi mbaya wa Mtemi Lesulia. Akishirikiana na wafuasi wake, Lonare anaingia katika kampeni za kisiasa bila kujali vitisho na matusi ya wapinzani wake ili kuikomboa nchi yake na kuleta mapinduzi kwa Waketwa, ambao waliishi kwa kudhulumiwa na viongozi wa Matuo. Juhudi za Lonare na wafuasi wake zinafua dafu, ambapo licha ya vizingiti vingi vinavyomkumba Lonare, anachaguliwa kuwa Mtemi wa Matuo na kuleta mapinduzi nchini matuo kama ambavyo mwandishi anatuonyesha kupitia Lonare:

> Nitatumia mamlaka mliyonipa kuhimili zao la taifa na kubatili nakisi ya bajeti. Kwa miaka mingi uchumi wa nchi umekuwa ukifisidiwa na walafi wasiojali maisha ya wengi. Wezi na walaghai wamekuwa wakichukua kibubusa rasilimali za nchi kujinufaisha. Nitabadilisha hali hii (uk. 178).

Dondoo hili linadhihirisha mabadiliko yanayopatikana nchini Matuo baada ya Lonare kuchaguliwa kuwa Mtemi. Lonare anaendelea kusema kuwa, mashamba ya serikali ambayo yalikuwa yamenyakuliwa na watu binafsi yatarudishwa serikalini. Anaahidi kuwa, waliopora mali ya umma na kukimbilia ugenini atahakikisha kuwa wamekamatwa huko na kurudishwa nchini ili wahukumiwe. Huyu ni mwanamapinduzi. Mwandishi anasema:

> Sasa watu walisimama na kumshangilia, walijua waliobekua mali ya umma sasa siku zao zimehesabiwa. (uk. 179).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa, mhusika wa kiume katika riwaya teule ni mwanamapinduzi. Aidha, mabadiliko ya haraka yanaonekana kupitia juhudi za Lonare na wenzake. Nadharia ya uhalisia inadai kuwa kazi ya fasihi inaonyesha matumaini juu

ya kizazi cha binadamu yaani binadamu aonyeshwe kama mshindi wa matatizo yanayomkabili. Lonare na wafuasi wake wanaonekana wakisherehekea ushindi baada ya kupitia matatizo mengi katika mazingira yao. Mwanamume katika jamii hupenda mabadiliko.

### 4.1.13 Mwanamume kama Anayesalitiwa

Mhusika wa kiume katika riwaya teule amesawiriwa kama anayefanyiwa usaliti. Kwa mfano, katika riwaya ya *Chozi la Heri*, mzee Kedi anamsaliti Ridhaa kwa kuangamiza familia yake. Kama mwandishi anavyosema, mzee Kedi alimsaidia Ridhaa kupata shamba alilokuwa akiishi pamoja na familia yake kabala ya kuagamizwa. Isitoshe, aliyeusimamia ujenzi wa jumba la Ridhaa ni mwanawe mzee Kedi aliyeitwa Lombo. Vilevile, mke wa mzee Kedi na mke wa Ridhaa walikuwa marafiki wa toka nitoke. Usaliti wa mzee Kedi kwa Ridhaa unadhihirika kupitia kinywa cha Ridhaa:

> "Kweli jaza ya hisani ni madhila? Vipi watu wawa hawa walioniita 'Ndugu' na 'Mzee', tukala na kunywa pamoja, tukazungumza ya kupwa na kujaa, wananilipulia aila na kuyasambaratisha maisha yangu?" (uk. 12).

Nukuu hii inaonyesha kuwa mhusika wa kiume anasalitiwa.

Riwaya ya *Nguu za Jadi* hali kadhalika, inamchora mhusika mwanamume kama mtu anayewasaliti wengine. Mwanasheria Mafamba anaonekana kusalitiwa na Mtemi Lesulia wakati anapomnyang'anya cheti cha uanasheria na kumfuta kazi licha ya kuifanyia serikali yake kazi na kumfichia uovu wake katika kesi za ufisadi. Utafiti unaonyesha ya kwamba, Mafamba anafanyiwa tendo hili wakati alishindwa kutatua kesi ya ardhi ya Matango kwa njia ambayo Mtemi alitaka. Mwandishi anasema:

> Shoka lililomwangukia hakimu halikumwacha Mafamba. Huyu alinyang'anywa leseni yake ya uanasheria pia akatimuliwa katika afisi za serikali (uk. 96).

Maelezo haya yanasadifu namna jinsia ya kiume ilivyo katika jamii halisi na maisha ya kila siku. Usaliti ni jambo la kawaida katika jamii zetu.

### 4.1.14. Mwanamume kama Kiumbe asiye na Hisia

Mhusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* anasawiriwa kama kiumbe asiye na hisia. Ridhaa anatatizika sana na milio ya kereng'ende usiku wa kuamkia siku ile ya kiyama. Kama anavyosema mwandishi, milio hii ilionekana kumtia Ridhaa kiwewe zaidi, kwani bundi hawakuwa wageni wa kikaida katika janibu hizi. Aidha, Ridhaa alijaribu kumjuza mkewe ila alipuuza na kumwambia kuwa, atakuja kujitia fadhaa bure kwa kujishughulisha na mambo ya ushirikina. Haya yanadhihirika mkewe anaposema:

> "We nawe huishi kufanya tumbo moto! Kila jambo kwako lazima liwe na kiini! Utakuja kujitia fadhaa bure. Nashangaa vipi daktari mzima hapo ulipo unajishughulisha na mambo ya ushirikina" (uk. 2).

Mazungumzo haya baina ya Ridhaa na mkewe Terry, yalikuwa ya mwisho kabisa kutokea Terry akiwa hai. Ridhaa anatamani kuwa angekuwa na muda zaidi wa kumuuliza mkewe maswali ambayo sasa yameivamia akili yake. Kama anavyoeleza mwandishi, moyo wa Ridhaa ulipiga kidoko, ukataka kumwonya dhidi ya tabia hii ya kike ya kulia pindi mtu akabiliwapo na vizingiti ambavyo ni kawaida ya maisha, ukamkumbusha maneno ya marehemu mama yake siku za ujana wake.

> "Ridhaa mwanangu, mwanamume hufumbika hisia. Machozi ya Mwanamume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majambali ya maisha. Huku ni kujiumbua hasa. Unyonge haukuumbiwa majimbi; ulitunukiwa makoo (uk. 3).

Kwa kurejelea dondoo hili, mwandishi anaonyesha mitazamo potovu waliyonayo watu kuhusu jinsia ya kiume. Msimamo wetu ni kwamba, iwapo wanawake wanaruhusiwa kulia, basi hata majimbi wana hisia na wanapaswa kulia ili kuondoa uchungu na masikitiko.

### 4.1.15 Anayebaguliwa kwa Misingi ya Kiukoo

Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, Ridhaa anabaguliwa kwa sababu ametoka ukoo tofauti na watu wa ukoo wa Msitu wa Heri. Tunaelezwa kuwa, Ridhaa alitazamana ana kwa ana na tanuri la moto ambalo liliteketeza jumba lake la kifahari. Katika mkasa huu, familia yake iliangamia. Inaelezwa kuwa, Ridhaa hakuwa mkaazi asilia wa Msitu wa Heri. Alikuwa 'mfuata mvua' kama walivyoitwa walowezi na wenyeji kindakindaki walionunua na kuhamia sehemu tofauti. Kama tunavyoarifiwa, baba yake Ridhaa alikuwa na wake kumi na wawili. Wake hawa walijaliwa na wana wa kiume ishirini na ndipo ardhi ya mzee Mwimo Msubili ikawa haitoshi kuwalea. Mzee Mwimo aliwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu wa Heri. Mama yake Ridhaa alikuwa mke wa mwisho wa Mzee Mwimo. Wakati huo, Ridhaa alikuwa na umri wa miaka kumi na alikuwa bado hajaanza shule. Walipowasili humu, hamkuwa na wakaazi wengi na ilimchukua muda kuzoeana na watoto wa majirani ambao walimuona kama aliyekuja kuvuruga utulivu wao. Ridhaa alitengwa na wenzake siku ya kwanza shuleni katika michezo mbalimbali. Mwandishi anaonyesha hali hii kupitia mwanafunzi mmoja:

> "Wewe ni Mfuata Mvua, hatutaki kucheza nawe. Umekuja hapa kutushinda katika mitihani yote. Wewe ndiwe unatuibia kalamu." (uk.10).

Kwa kurejelea dondoo hili, inaonekana kuwa watoto hawa wamejifunza kutoka kwa wazazi wao kutoshirikiana na watu ambao si wa jamii zao. Isitoshe, katika riwaya ya *Chozi la Heri*, wanajamii wana chuki na watu mbalimbali ambao wamehamia sehemu zao kwa njia ya kununua ile ardhi. Watu hawa huonekana kama maadui kwa wanajamii asilia. Inaonekana kuwa, Ridhaa ameyafanya mengi mazuri kijijini mpaka kikaacha kuitwa Kalahari. Hata hivyo, mke wa jirani anakuja kulalamika kuhusu kuuzwa kwa mashamba ya wenyeji kwa wageni, ambapo Ridhaa anagundua kuwa alikuwa mgeni

wala si mwenyeji, hata baada ya kuishi pale kwa miongo mitano. Halikadhalika, watu waliokula na kunywa pamoja naye, wanamlipulia aila na kusambaratisha maisha yake.

### 4.1.16 Mwanamume kama Anayempenda Mkewe

Mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* amemchora mhusika mwanamume kama mtu mwenye mapenzi ya dhati kwa mkewe. Kwa mfano, Lunga anampenda sana na kumtunza mkewe Naomi. Anajitolea kumridhia lakini mwanamke huyu haridhiki. Mwandishi anaeleza kuwa, Naomi ni miongoni mwa wale ahali ambao hata wanapoolewa hawasahau uhusiano wao na nasaba zao, hawatulii kuyapalilia maisha ya unyumba. Inaelezwa kuwa, Lunga aliamshwa asubuhi moja na mlio wa rununu yake kuashiria kuwa kuna ujumbe mfupi. Ujumbe huo ulitoka kwa mkewe akimfahamisha kuwa ameenda kutamba na ulimwengu. Mwandishi anasema:

> Lunga alihisi kama aliyechomwa kwa joto la tanuri. Hili ni pigo la tatu kutoka kwa walimwengu. Tofauti ni kwamba hili linauma na kudhalilisha zaidi. Kwani Lunga alijisabilia kwa hali na mali kumpendeza mkewe. Kwamba analilipia penzi lake kwa kumwachia adha za malezi ni jambo ambalo Lunga hakuweza kulistahimili (uk. 81).

Kwa kurejelea dondoo hili, inadhihirika kwamba, Lunga alikuwa na mapenzi ya dhati kwa mkewe hata ingawa alimsaliti. Kwa sababu ya kuachwa na mkewe, Lunga aliingiwa na wahka ambao ulimsababishia Kihoro, na kuugua ugonjwa wa shinikizo la damu na mwishowe kufariki akiwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao.

Vilevile, tunamuona Kaizari ambaye ana mapenzi ya dhati kwa mkewe. Tukio hili linaonyesha kuwa, Subira mkewe Kaizari na mavyaa wake hawahusiani vyema. Jambo hili linamfanya Subira kuondoka na kumuacha Kaizari pamoja na watoto wake Lime na Mwanaheri. Mapenzi ya dhati yanaonekana pale ambapo Kaizari anajitolea

kumtafuta mkewe huku akijawa na majuto makuu. Hali hii inadhihirika kupitia Mwanaheri:

> Baba alienda kumtafuta mama kwao, asimpate. Alijuzwa kuwa mama alikuwa ameenda mjini kuzumbua riziki. Baba alifululiza mjini kumtafuta mama, majuto yamemjaa kifuani (uk. 96).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, maelezo haya yanasadifu na kuakisi hali halisi ya jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, fasihi inapaswa kuwasawiri wahusika kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Kihistoria mwanamume huwa na jukumu la kumpenda na kumtunza mkewe na akipotea jamii inamlaumu mwanamume kwa sababu alikabidhiwa jukumu la kumlinda. Ingawa mwanamume katika jamii anaonekana kukabiliwa na vizingiti, anaonyesha upendo kwa mkewe.

#### 4.1.17 Mwanamume kama Mwenye Tamaa na Ubinafsi

Tamaa ni ile hali ya kutaka sana kitu au matamanio ya kitu au jambo fulani. Hamu ya kufaidi kitu huwa mbaya iwapo itafaidi mtu mmoja kutokana na ubinafsi wake. Ubinafsi ni ile hali ya mtu kujipendelea yeye mwenyewe pasipo kuwajali watu wengine.

Mwandishi wa riwaya ya *Nguu za Jadi* amemsawiri mhusika wa kiume kama mtu mwenye tamaa na ubinafsi. Mwandishi anaeleza kuwa nchini Matuo, mtaa wa Majuu ulikuwa umeshiba ubinafsi na ubaguzi. Hili linadhihirika kutokana na jinsi Mtemi Lesulia anavyojawa na tamaa ya uongozi na kutokana na tamaa hii yuko tayari kuendeleza dhuluma au hata mauaji kwa wapinzani wake. Mtemi Lesulia anamteka nyara Lonare mpinzani wake, ili asiweze kuwa katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu. Hii ni kwa sababu Mtemi anahisi kuwa Lonare huenda akamshinda na kuwa mtemi. Mwandishi anasema:

> Mtemi Lesula na Sagilu walikuwa tutu kwa ufu. Isitoshe, wote walimchukia Lonare. Walijua kwamba alitaka kugombea kiti katika uchaguzi ujao. Walimpangia njama ili awe muflisi, lakini vigwena hao wakatibuliwa na wale waliompenda Lonare. Walituma magaidi kumkatizia maisha, lakini watu hawa wakamjia Lonare na kumonyesha malaki ya pesa waliyopewa kumwagamiza. (uk. 51).

Aidha, Mtemi Lesulia na wenzake kama vile Sagilu wanahujumu pato la nchi kutokana na tamaa ya kujilimbikizia mali. Mwandishi anatudhihirishia ubinafsi wa Mtemi Lesulia pale ambapo anaonekana kumiliki raslimali za serikali kupitia kwa unyakuzi unaoendelezwa na Mkewe Nanzia. Mwandishi anaonyesha hili anaposema:

> Walihangaika ili kusitiri pato la nchi ambalo kiasi kikubwa pato hilo liliwaendea wenye hali na vyeo nchini. Mtemi kama mjusi kafiri juu ya kuchunguu, aliingia katika shimo moja hadi jingine akiotea vyakula vya mchwa au hata kuwala mchwa wenyewe (uk. 93).

Dondoo hili linadhihirisha sifa ya tamaa na ubinafsi kwa wahusika wa kiume. Vilevile, Sagilu ambaye ni mshauri mkuu wa Mtemi Lesulia, anaonekana kuwa mwenye tamaa na ubinafsi pale ambapo anahodhi bidhaa kama vile ngano kwa njia za kimagendo bila kulipia ushuru na kuiuza kwa bei ghali. Isitoshe, anaagiza maziwa yenye sumu kutoka ughaibuni. Inaelezwa kuwa, maziwa haya yalihatarisha maisha ya watoto wote nchini. Mwandishi anasema:

> Waliokunywa maziwa hayo walitapika na kuendesha kiasi cha kutia nchi nzima taharuki (uk. 17).

Dondoo hili linaonyesha ubinafsi uliokithiri. Mrima naye kwa sababu ya tamaa ya pesa, anadanganywa na Sagilu na kupewa pesa mpaka anaitelekeza familia yake na kupotelea ulevini. Ubinafsi unamfanya kukaidi masharti ya ndoa na uwajibikaji. Tamaa ya pesa inasababisha kusahau kuwa Sagilu alikuwa adui mkubwa wa Waketwa. Mwandishi anatuonyesha hili kupitia Mangwasha anaposema:

> “Hizo pesa ambazo unapewa na mahasidi wetu mbona unazikubali? Hata kama unazikubali mbona huzileti nyumbani tukazitumia sote? Kumbuka tuna watoto wanaotutegemea Mrima” (uk. 41).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu ni dhahiri kwamba wahusika katika riwaya ya *Nguu za Jadi* ni wenye tamaa na ubinafsi. Nadharia ya uhalisia inadai ya kwamba katika kazi ya fasihi wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na jamii. Katika hali halisi, jamii hudhihirisha watu wenye tamaa na ubinafsi. Hali ilivyo katika jamii halisi ndivyo inavyosawiriwa katika riwaya ya *Nguu za Jadi.* Mwanaume katika ulimwengu halisi, huwa na sifa hasi na chanya.

### 4.1.18 Mwanamume kama Fisadi

Hali ya kuamua kudanganya na kunufaika kwa kutoa au kupokea mali kama fedha ni ufisadi. Riwaya ya *Nguu za Jadi* imemchora mhusika mwanamume kama mtu anayepokea au kutoa hongo ili afaidike. Inaelezwa kuwa, kutokana na urafiki wake wa karibu wa wahusika, Mtemi Lesulia, Sagilu anajiingiza katika vitendo vya ufisadi. Hili linadhihirika wakati anaposhirikiana na mwanawe Mashauri kufisidi nchi kwa kuuza vipusa na meno ya ndovu kama ambavyo mwandishi anatuonyesha kupitia Sauni:

> Kijana aliyeshirikiana na mzazi wake kufisidi vipusa na meno ya ndovu. Kijana aliyetajirika kwa kuuza maliasili za nchi ng’ambo hadi kuathiri utalii wa nchi (uk. 127).

Isitoshe, Sagilu anaficha bidhaa na kuziuza kwa faida. Inaelezwa kuwa, anazuia meli baharini isitie nanga bandarini na kupakua ngano, mpaka anafaulu kuuza kwa bei ya juu ngano nchini. Vilevile, anaagiza ngano hiyo kimagendo pamoja na bidhaa nyingine ambazo hakulipia ushuru. Aidha, malori yake yanaposhikwa na polisi yakisafirisha bidhaa gushi, anatoa mlungula na maroli hayo kuachiliwa kusambaza bidhaa zinazohatarisha maisha ya watu. Mwandishi anasema:

> Kila wakati malori yake yaliposhikwa yakisafirisha bidhaa ghushi nchini, alitoa hongo kisha yaliachiliwa kusambaza bidhaa zilizohatarisha afya ya umma (uk. 17).

Halidhalika, Sagilu anaimarisha mtandao wa mafisadi ambao hata polisi hawakuweza kukabiliana nao. Sagilu anaonekana kumuhonga Mangwasha pesa ili afaidi penzi lake. Tendo hili linaashiria ufisadi wake. Sagilu anaungana na Mtemi Lesulia na wengine kuwanyang'anya ardhi yao wenyeji wa Matango. Kama inavyoelezwa, Sagilu na Mtemi Lesusia wanashirikiana kuwahonga rafiki wa Ngoswe ili kwenda kusambaratisha zoezi la upigaji kura. Huu ni ufisadi. Mwandishi anaeleza:

> Kwanza aliwapa vifurushi vya pesa kisha akawaeleza kwamba siku ya uchaguzi wa mchujo wahonge watu kinyemela kuharibu zoezi la upigaji kura (uk. 128).

Dondoo hili ni dhihirisho la ufisadi katika riwaya hii.

Riwaya ya *Nguu za Jadi* inaakisi hali halisi ya jamii ya sasa. Ni kweli kuwa fasihi ni kioo cha jamii kwa sababu tunayoyaona katika jamii yanaonekana pia katika riwaya hii. Ingawa mwanamume ametelekezwa na kukosa nafasi katika jamii, sifa zake ni hasi na chanya kwa kuwa hakuna aliye mkamilifu. Ufisadi ni jambo la kawaida katika jamii ya sasa.

## 4.2 Changamoto Zinazomkabili Mhusika wa Kiume katika Riwaya Teule

Mtafiti anaonelea kuwa, jinsia ya kiume inahitaji kupewa msaada kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Hii ni kwa sababu, inakumbana na changamoto mbalimbali katika maisha zikiwemo za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kifikra. Kwa mujibu wa riwaya zinazorejelewa katika utafiti huu, changamoto mbalimbali zinazomkabili mhusika wa kiume zimebainika. Changamoto hizo ni pamoja na; ukosefu wa nafasi za kazi, kutelekezwa, ukosefu wa matumaini, usaliti, ulevi, kutopewa nafasi katika jamii, kutumikishwa, jeraha la mwili na la kisaikolojia.

### 4.2.1 Mwanamume kukosa Kazi

Ukosefu wa nafasi za kazi unadhihirika katika riwaya ya *Chozi la Heri* wakati ambapo, vijana wa kiume hata wale ambao wamehitimu katika taaluma mbalimbali wanaonekana kukosa ajira. Kupitia mja mmoja ambaye alikuwa amevaa shati lililoandikwa 'Hitman', mwandishi anatuonyesha kuwa, wakati wa uchaguzi vijana hawa uhaidiwa nafasi za kazi lakini baada ya viongozi hao kuingia mamlakani, haya yote husahaulika. Mwandishi anadhihirisha hili kupitia mja aliyekuwa amevaa shati lililoandikwa 'Hitman':

> Nashangaa ni vipi mtu aliye na shahada ya uzamifu katika masuala ya elimu na mitaala hajaweza kuwaziwa nafasi kama hizi zinapotokea! Mara wewe tutakuteua kama Waziri wa masilahi ya kijamii katika jimbo…haya yote husahaulika mara tu baada ya uchaguzi na kuvyazwa kwa serikali mpya (uk. 23).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, ni dhahiri kwamba, mhusika wa kiume katika riwaya teule amekosa nafasi ya kazi. Hata hivyo, vijana wa kiume wakikosa ajira serikalini wanaweza kulima mashamba na kuzalisha mali. Mwandishi anaeleza kuwa, vijana hawa na familia zao wanaishi kwa msaada wa wale waliotoka mbali kule walikotoka, wakapewa maelfu ya ekari na kujenga viwanda na maduka ya biashara. Wengine wanalima mashamba makubwa wakidai kuwa, wanawasaidia wenyeji kupata mazao mengi. Kumbe wanawasababishia ufukara zaidi. Hili linadhihirika kupitia kinywa cha mja huyu:

> Vijana wenzetu ni vyema kumpigia kura kiongozi anayejali mustakabali wa maisha yenu, kiongozi atakayesaidia kuangamiza tatizo sugu la uhaba wa nafasi za kazi (uk. 22).

Hali kadhalika, mhusika Shamsi anadhihirisha ukosefu wa nafasi ya kazi kupitia wimbo wake anaouimba akiwa mlevi chakari. Mwandishi anaeleza:

> … kwani hawakunikabidhi kazi walizoahidi kweye mabuku (uk. 132).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, inadhihirika kuwa, mhusika wa kiume amekumbwa na changamoto ya ukosefu wa nafasi za kazi. Changamoto hii inayowakumba wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* ni akiso la hali halisi katika jamii. Wanaume katika jamii ya sasa wamekosa nafasi za kazi jambo ambalo linawafanya kutoyamudu maisha yao. Vilevile, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, vijana wengi wa jamii ya Waketwa hata waliosoma, wanaonekana kukosa ajira. Inaelezwa kuwa, kutokana na uongozi mbaya wa Mtemi Lesulia uliojaa ufisadi na ukabila, vijana wengi wa kiume hata wale waliohitimu katika taaluma mbalimbali walikosa ajira. Baadhi yao walianza kushikilia kwamba, elimu haikuwa na thamani kwao. Mwandishi anaeleza:

> Ukosefu wa ajira hasa kwa vijana waliohitimu katika taaluma mbalimbali ulikuwa sasa ni mazoea (uk. 44).

Mwandishi anasema kuwa, nchi ya Matuo ilishindwa kupanua uchumi ili kuwaajiri vijana wa kiume, na haikuweza kuanzisha miradi ya kuwawezesha kujiinua kiuchumi. Mwandishi anasema kuwa, kazi zilizopatikana zilipewa watu wasiokuwa na ujuzi wala maarifa, jambo ambalo linasababisha maendeleo ya nchi kukwama na maafa mengi kutokea. Inaelezwa kuwa, kazi zilizokuwepo zilipeanwa kwa kujuana hata kama mtu hakuhitimu ipasavyo. Hivyo basi, vijana wa kiume wa jamii ya Waketwa wakabaki kuhangaika mijini. Mwandishi anasema:

> Vijana wengi Waketwa waliohitimu shahada za vyuo vikuu walihangaika mjini kutafuta kazi bila mafanikio katika majopo ya uajiri, utawala ulihakikisha kwamba hawa hawaajiriwi katika kazi zilizokuwa na mamlaka ya uongozi (uk. 44).

Kwa kurejelea dondoo hili, mtunzi amefanikiwa kuonyesha hali halisi ilivyo katika jamii ya sasa. Changamoto hii ya ukosefu wa ajira imewakumba vijana wengi wa kiume katika jamii ya sasa. Hivyo, mwandishi kupitia riwaya hii ameeleza mambo kwa

kuzingatia uyakinifu wa maisha. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, vijana wa kiume wapewe nafasi za kazi ili waweze kuyamudu maisha yao pamoja na familia zao.

### 4.2.2 Kutelekezwa katika Jamii

Katika riwaya zinazohusika, mhusika wa kiume ametelekezwa. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya *Chozi la Heri* kupitia mhusika Tetei, mwandishi anaposema kuwa, jamii ya Wahafidhina inaipa kipaumbele pamoja na kuitetea jinsia ya kike, huku hukumu ya kifo ikipitishwa dhidi ya mwanamume. Inaelezwa kuwa, anga nzima imehanikiza vilio vya kumkinga mwanamke ila, hakuna anayewatetea mamia ya wanaume ambao wanateseka katika ndoa kutokana na mapigo na dhiki za kisaikolojia kutoka kwa wake zao. Vilevile, hakuna anayeshuhudia majeraha ya kudhalilisha wanayopagazwa wanaume mashavuni, na hasa moyoni. Kupitia kinywa cha mwanaharakati Tetei, mwandishi anadhihirisha changamoto ya kutelekezwa kwa jinsia ya kiume anaposema:

> "Vyombo vya habari na vikao vya wapigania haki vinapigania elimu ya mtoto wa kike, haja ya kuwainua akina mama kiuchumi, hukumu ya kifo ikipitishwa dhidi ya mwanamume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake. Hata haki ya mtu kuhusiana kimapenzi na mkewe imebatilishwa na siasa hii ya usawa wa kijinsia! (uk. 17).

Kutokana na dondoo hili, ni dhahiri kuwa, utelekezaji ni mojawapo ya changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule.

Hali kadhalika, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume anaonekana kutopewa kipaumbele kama ilivyo kwa jinsia ya kike. Mwandishi anaeleza kuwa Mangwasha amekuwa akipitia maandiko mengi ambayo yanamfunza mtoto wa kike jinsi ya kuwa mwanamke, lakini amegundua kuwa, maandiko yanayomuelekeza mtoto wa kiume jinsi ya kuishi ni machache mno. Inadhihirika kuwa, vijana wengi wa kiume

hukumbana na changamoto za aina nyingi na hata mauti katika kujaribu kuwa wanaume. Utafiti unaonyesha kuwa, mtoto wa kiume amekosa dira ya kumwongoza na ambapo ni dhihirisho kuwa, mhusika wa kiume ametelekezwa katika jamii ya Matuo. Mwandishi anasema:

> Hakuna dira mahususi ya kumwongoza mtoto wa kiume. Dira hiyo ni mzazi wake wa kiume. Aghalabu huyu hayuko au hata hajulikani. Hivyo hapati mafunzo yoyote kutoka kwake (uk. 138).

Kwa mujibu wa nukuu hapo juu, imebainika kuwa, mhusika wa kiume katika riwaya hii hana mtu wa kumwelekeza. Ametelekezwa. Inaelezwa kuwa, mwanamume katika familia ndiye dira inayofaa kumwelekeza mtoto wake wa kiume ila hayupo, au hata akiwepo, ana kazi nyingine za kufanya. Aidha,Mangwasha anasema kuwa jinsia ya kiume imetelekezwa huku jinsia ya kike ikipewa kipaumbele na kujadiliwa namna inavyoonewa na kudhulumiwa. Mwandishi anasema:

> Jamii ilimshika mkono mtoto wa kike, ikapiga mbio na mtoto wa kike na kusahau kwamba hata wewe unahitaji kushikwa mkono (uk. 138).

Kupitia nukuu hii, changamoto ya utelekezaji wa jinsia ya kiume unadhihirika. Aidha, Lonare anapochaguliwa kuwa Mtemi wa Nchi ya Matuo, ana lengo la kubadilisha maisha ya vijana wa kiume ambao anawaona kuwa wametengwa na jamii na wanapitia changamoto za aina mbalimbali. Kupitia kinywa cha Lonare yanadhihirika haya:

> Aidha serikali yangu itadhibiti ujasiriamali miongoni mwao kwa njia mbalimbali. Hii ni kwa sababu tegemeo la vijana ndio tegemeo la Matuo la baadaye. Jamii hii imewatenga sana vijana wa kiume. Je, familia zitajengwaje ikiwa mume haonekani kuwa mume ndani ya nyumba? (uk. 180).

Kwa kurejelea dondoo hili, hali ilivyo ndani ya riwaya teule, ndivyo inavyoonekana katika jamii halisi. Nadharia ya uhalisia inadai ya kwamba, fasihi ieleze mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Katika jamii mwanamume ametelekezwa, amepuuzwa

na kutengwa huku mwanamke akipewa kipaumbele katika jamii. Kulingana na Katiba ya Kenya (2010) kifungu cha tisini na saba (97), kila eneo Bunge lina mwakilishi wa wanawake ilhali hakuna anayewakilisha wanaume. Atieno (2019) anasema kuwa, tafiti kadha za hapo awali zimeshughulikia masuala ya wanawake na kupuuzwa kwa masuala ya wanaume. Anasema kuwa, hali ya wanaume imekuwa ya upweke kwa sababu hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Mtafiti anaonelea kwamba, pawe na dira mahususi ya kumuongoza mtoto wa kiume. Aidha, mengi yaandikwe yanayomuelekeza mtoto wa kiume jinsi ya kuishi na pia, mtoto wa kiume apewe nafasi sawa na mtoto wa kike katika jamii ili kukiokoa kizazi hiki kinachopotelea nyikani.

### 4.2.3 Mwanamume kukosa Matumaini

Mhusika wa kiume katika riwaya teule anaonekana kukosa matumaini katika maisha. Haya yanadhihirika katika riwaya ya *Chozi la Heri*, ambapo baada ya familia ya Ridhaa kuangamia kwa moto na baadaye anafukuzwa kwao, anaingiwa na wasiwasi na kukosa matumaini katika maisha. Mwandishi anasema kuwa, baada ya kufukuzwa katika Msitu wa Heri, Ridhaa, Kaizari na familia yake waliishi katika Msitu wa Mamba kwa miezi sita. Baada ya kipindi hicho, walibahatika kurudi nyumbani. Ridhaa hakuwa na familia ya kuendea kwa sababu wote isipokuwa Mwangeka walikuwa wamekwisha kuangamia. Jambo hili lilimkosesha matumaini ya kuishi. Mwandishi anadhihirisha changamoto ya ukosefu wa matumaini anaposema:

> Ridhaa alihisi kama anayetoka Kanaani kwenda Misri. Hakuwa na matumaini ya maisha bora, hasa alipokumbuka kuwa, hakuwa na mwenzi wala mtoto wa kuendea. Siku walipoambiwa kuwa watarudishwa kwao, ilikuwa siku ya hisia mseto kwa wengi. (uk. 34).

Kauli hii ya mwandishi inadhihirisha kuwa, mhusika wa kiume katika riwaya ya teule amekumbwa na changamoto ya ukosefu wa matumaini. Kwa upande wa riwaya ya *Nguu za Jadi*, Ukosefu wa matumaini unabainika pale ambapo, idadi kubwa ya vijana wa kiume inaonekana kuzurura mjini na kupoteza wakati wao katika viambaza vya maduka. Mwandishi anasema:

> Ukosefu wa matumaini ya kuishi ulianza kuhasiri mifumo ya kijamii. Asasi ya familia ikaathirika sana pale mizozano ya kifamilia ilipokithiri (uk. 47).

Isitoshe, Mangwasha alikuwa akiwaonea huruma vijana hawa ambao aliwaona kama kizazi kilichopotea kama anavyoeleza mwandishi kuwa:

> Mangwasha aliwaona kama kizazi kilichopotea. Je, hawa wangeweza kuwa raia wa kuaminiwa kesho kweli? (uk. 34).

Inaelezwa kuwa, vijana wengine walizurura tu katika barabara za mji wasijue wafanyalo. Maneno ya mwandishi yanadhihirisha wazi ukosefu wa matumani kwa vijana wa kiume. Mwandishi anaonyesha kupitia Mangwasha:

> "Hawa watakuwa wanaume wenye kutunza jamaa zao kweli? (uk. 49).

Aidha, mwandishi anaonyesha kuwa, changamoto ya ukosefu wa matumaini miongoni mwa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Nguu za Jadi,* imetokana na kutelekezwa kwa jinsia ya kiume. Mangwasha anasema kuwa, kuna maandiko mengi yanayomwelekeza mtoto wa kike jinsi ya kuishi ilhali ni machache yanayomfunza mtoto wa kiume. Anasema kuwa, vijana wengi wa kiume hukumbana na mauti katika harakati za kujaribu kuwa wanaume. Kama inavyoelezwa, hakuna dira ya kumuongoza mtoto wa kiume jambo ambalo linampelekea kukosa matumaini maishani. Mwandishi anadhihirisha haya anaposema:

> Mangwasha aliwaona vijana hao kama kizazi kilichopotea (uk. 137).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, imedhihirika kuwa, ukosefu wa matumaini ni changamoto ambayo huikumba jinsia ya kiume katika maisha ya kila siku, katika jamii halisi. Kupitia riwaya teule, waandishi wameonyesha uhalisia uliopo katika jamii. Katika jamii halisi, mwanamume amekosa matumaini ya kuishi, wengi wao wameingilia matumizi mabaya ya dawa za kulevya ili kujisahaulisha wanayopitia. Maoni yetu ni kwamba, hatua isipochukuliwa huenda hali hii ikaathiri pakubwa kizazi cha kiume kijacho.

### 4.2.4 Kulemewa na Ulevi

Imebainika kuwa, ulevi ni mojawapo ya changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya zinazohusika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Chozi la Heri*, changamoto ya ulevi inadhihirika pale ambapo wahusika wa kiume baada ya kukosa ajira, wanaingilia matumizi mabaya ya vileo. Mwandishi anasema kupitia kinywa cha Selume kuwa:

> Na ushidhani wanaotumia vileo vibaya ni wale tu wanaotaka kujipurukusha na hali duni vyuoni. Wapo wanaovitumia ili kujisahaulisha kusambaratika kwa familia zao (uk. 142).

Aidha, changamoto ya ulevi inadhihirika kupitia mhusika Shamsi ambaye anakata tamaa maishani na kuingilia matumizi mabaya ya pombe, akawa mlevi wa kupindukia. Kwa kurejelea dondoo hili, riwaya teule inaweza kutumika kama kioo cha kumulika yanayotendeka katika jamii halisi. Hii ni kwa sababu ulevi ni mojawapo ya changamoto zinazowakumba wanaume katika jamii ya sasa.

Kwa upande mwingine, Riwaya ya *Nguu za Jadi* inaonyesha kuwa, ulevi wa pombe ni mojawapo ya changamoto inayopelekea kutofaulu kwa mhusika wa kiume, na kukosa maendeleo katika jamii zao. Changamoto ya ulevi inadhihirishwa na mhusika Mrima

anayeiacha familia yake na kushiriki ulevi kupitia kwa Sagilu. Mwandishi anaonyesha haya kupitia mhusika Mangwasha:

> Mrima haonekani kujitwika majukumu yake ya unyumba tena. Anakesha na kuamkia ulevini. Hana Habari tena kuhusu familia yake. (uk. 29).

Aidha, mwandishi anaeleza kuwa, wakati Mangwasha anaondoka kuelekea Ponda Mali kumtafuta mumewe aliyepotelea ulevini, anajionea jinsi changamoto hii ya ulevi ilivyowalemea wanaume katika jamii yao. Mwandishi anasema:

> Njiani alikumbana na walevi waliozua vitimbi vya kila aina. Wengine waliimba nyimbo zisizokuwa na mahadhi ilhali wengine walibaki kutoa vicheko vilivyowaudhi wapita njia. Hapa na pale aliwaona wengine wakitapika ovyo baada ya nishai za ulevi kunoga. (uk. 34).

Dondoo hili ni dhihirisho kuwa, changamoto ya ulevi imemlemea mhusika wa kiume katika riwaya teule. Isitoshe, pale Majaani ambapo Mrima aliokotwa, palijaa walevi waliolewa chakari. Mwandishi anadhihirisha hali hii anaposema:

> Hapa palikuwa na walevi waliolewa chakari. Baadhi yao walikuwa wanavuta sigara. Wengine waliendelea kubugia pombe katika chupa walizobeba. Wengine tayari walikuwa wametekwa na usingizi. Walilala vinywa wazi bila kujali nzi waliong’ong’a nyuso zao (uk. 99).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, riwaya teule inaonekana kuakisi hali halisi ya jamii ya sasa. Hii ni kwa sababu, kunao walevi katika jamii ya sasa, na matendo yao yanalingana na matendo ya wahusika walevi katika riwaya hii. Riwaya hii inaweza kutumika kama kioo cha kumulika yanayotendeka katika jamii ya sasa. Kulingana na maoni ya mtafiti, hatua ichukuliwe ili kukabiliana na changamoto hii inayowakumba wanaume wengi katika jamii, kwani tusipoziba ufa tutajenga ukuta.

### 4.2.5 Kusalitiwa kwa mwanamume

Usaliti ni changamoto kubwa inayomkumba mhusika wa kiume katika kupigania maslahi yake kwa pamoja ndani ya riwaya teule. Kwa mfano, katika riwaya ya *Chozi la Heri*, changamoto hii imetokea kwa Lunga ambaye anafutwa kazi na shirika la Maghala ya Fanaka, kwa sababu ya kupinga kitendo cha raia kuuziwa mahindi ya manjano kutoka ughaibuni. Inadhihirika kwamba, baada ya usaliti huu, Lunga anapatwa na matatizo ambapo maisha yake yanabadilika na mkewe kumtoroka. Mwandishi anasema:

> Alijiona kama mfa maji ambaye anakabiliwa na mtutumo wa mawimbi ya misiba, mmoja baada ya mwingine alikumbuka kazi yake. Yeye alikuwa mtu mwenye chake. Alikuwa mwenye heba zama zile alizokuwa kinara wa kitengo katika shirika… mlimwengu aliyang'wafua haya kutoka kinywani, akamfuta kazi! (uk. 79).

Ingawa Lunga anatumikia shirika hili kwa kujitolea linamfuta kazi kwa kuwa mtetezi wa haki. Huu ni usaliti. Aidha, Naomi anaonekana kumsaliti mumewe Lunga licha ya mapenzi anayompa. Mwandishi anaeleza kuwa, Lunga anapopoteza kazi yake na maisha yake kubadilika, mkewe anatoroka na kumwachia watoto. Mhusika Lunga analazimika kuwa baba na mama wa watoto wake. Changamoto hii ya usaliti inamsababishia Lunga kihoro na hatimaye uwele wa shinikizo la damu na mwishowe anafariki. Hali hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao (uk. 82).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, inadhihirika kuwa, usaliti ni jambo la kawaida katika jamii halisi. Hivyo maelezo haya yanasadifu uhalisi katika jamii. Aidha, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume anakumbwa na changamoto ya usaliti. Hali hii inadhihirika wakati Sagilu anamnyemelea Cheiya ambaye ni mkazamwanawe na

kufanya uhusiano wa kimapenzi naye. Inaelezwa kuwa, Mashauri mwanawe Sagilu, na ambaye ni mumewe Cheiya, hakuamini kuwa jambo kama hili lingeweza kutendeka. Ngoswe alimpa habari Mashauri kuwa, alikuwa amewaona Sagilu na Cheiya katika hoteli ya Saturn huku wameshikana mikono kwa njia isiyoeleweka. Mwandishi anasema kuwa, Mashauri hakuyaamini kamwe maneno ya Ngoswe, lakini alifanya uchunguzi ili kujua ukweli uliokuwepo. Usaliti unadhihirika mwandishi anaposema:

> Mashauri aliona asiyotaka katu kuyaona. Alimwona babake akishuka kutoka orofa ya juu. Mkononi ameshika Cheiya kama mkoba. Wawili hao walishika ngazi taratibu. Walikumbatiana na kunong'onezana maneno ambayo ni wao tu waliyafahamu (uk. 121).

Dondoo hili linadhihirisha usaliti wa baba kwa mwanawe. Hali kadhalika, Cheiya pia anamsaliti mumewe kwa kufanya mapenzi na bavyaa wake.

Vilevile, Mrima anawasaliti wahusika wa kiume wenzake kama vile; Lonare, Sagura, Sauni na wengine. Hii inadhihirika wakati Mrima anapokubali wito wa Sagilu kuendesha kampeni za Mtemi Lesulia, ambaye alikuwa mpinzani wa Lonare. Inaelezwa kuwa, Mrima alipokea pesa shilingi elfu mia nane kutoka kwa mtemi na akakubali wito wao. Mwandishi anadhihirisha usaliti kupitia Sagura:

> "Mrima dunia yote inajua aliyemsaliti Yesu Kristo. Unajua mtu huyo aliishia wapi?" Sagura alitamka huku akimkazia Mrima macho (uk. 114).

Dondoo hili linadhihirisha usaliti wa Mrima kwa wanaume wenzake. Hii ni kwa sababu, anakubali hongo na kumuunga mkono Mtemi Lesulia. Usaliti ni jambo la kawaida katika jamii.

### 4.2.6 Kutumikishwa katika Jamii

Utafiti huu umebaini kuwa, mojawapo ya changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya hii ni kutumikishwa katika jamii. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*,

mhusika wa kiume amedhalilishwa katika jamii ya Wahafidhina na nafasi yake haitambuliki. Anatumikishwa na kukadamizwa. Inaelezwa kuwa, katika jamii ya wahafidhina kuna wakati ambapo wanaume walitumikishwa sana na wanawake waliokuwa mamlakani. Mwandishi anatuonyesha hayo kupitia mwanaharakati Tetei:

> Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike yule anayesimuliwa katika visakale vya majirani zetu. Kumbuka jinsi katika enzi hiyo ya Kisitimari wanaume walivyotumikishwa! Si sisi tuliokuwa tukitifua udongo mashambani huku, wanawake kama majeta, wanakaa na kutumikisha? (uk. 17).

Kwa kurejelea nukuu hii, mwanaharakati Tetei anasema maneno haya baada ya kutawazwa kwa kiongozi mwanamke ambapo, wengi waliamini hafai kuongoza. Wanaume wanaonekana kushika silaha kupigania uhuru wao wakidai kuwa, watatumikishwa kama walivyofanywa enzi hizo. Wanatoa kauli kuwa, kiongozi mwanamke atawarudisha kule walikotoka. Mwandishi anatudhihirishia hili kupitia Tetei:

> Sasa wanataka kuturudisha palepale. Kwa miongo mitatu sasa, hawa watu wamekuwa wakitusumbua na *affirmative action* na *a third should be women*. (uk. 17).

Kwa kurejelea dondoo hili, ni uhalisia mtupu kwamba, wanawake wanapoingia mamlakani hutumia nafasi hiyo kuwadhulumu wanaume.

### 4.2.7 Kutopewa Nafasi katika Jamii

Jamii ya wahafidhina katika riwaya ya *Chozi la Heri* inaonekana kuipa kipaumbele jinsia ya kike huku wahusika wa kiume wakiipuuzwa. Kupitia kinywa cha mwanaharakati Tetei mwandishi anaonyesha kuwa, hakuna anayewafikiria wanaume wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsi ya kike. Tetei anasema:

> Fikiria suala la jinsia. Na usidhani ni jinsia nyingine. Ni dada zetu tu (uk. 17).

Hali kadhalika, changamoto ya mhusika mwanamume kutopewa nafasi katika jamii inadhihirika pale ambapo kupitia Tetei mwandishi anasema:

> Hakuna tuliloweza kulipitisha hata katika vikao vya kitawala bila kusikia kidumtu akisema “Fikiria suala la jinsia” na usidhani ni jinsia nyingine, ni dada zetu tu (uk. 17).

Nadharia ya uhalisia inadai kuwa, fasihi hulenga kueleza mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Kwa mujibu wa nadharia hii, riwaya hii inasadifu uhalisia katika maisha ya sasa. Mwanamume hana nafasi katika jamii ya sasa. Jamii imeshika mkono mtoto wa kike na kupiga mbio na mtoto wa kike ikasahau kwamba hata mtoto wa kiume anahitaji kushikwa mkono. Mohamed (2018) anasema kuwa, wanawake wamekuwa wakipiganiwa haki zao ili kuwafanya sawa na wanamume katika nyanja mbalimbali, hali ambayo imefanya nafasi ya mwanaume kusahaulika. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, mtoto wa kiume anahitaji kushikwa mkono jinsi inavyofanyiwa jinsia ya kike.

### 4.2.8 Kujeruhiwa kimwili na Kisaikolojia

Utafiti huu umebaini kuwa, kupigwa na kupagazwa dhiki za kisaikolojia ni mojawapo ya changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Changamoto hii inasababisha mhusika wa kiume kushindwa kuyamudu maisha yake. Kupitia mwanaharakati Tetei. Mwandishi anaeleza kuwa kuwa, jamii ya Wahafidhina inamtetea mwanamke dhidi ya dhuluma na manyanyaso na kusahau kuwa mamia ya wanaume wanateseka katika ndoa zao kutokana na dhuluma wanazopata kutoka kwa wake zao. Mwandishi anasema:

> Ni wangapi wanaotetea mamia ya wanaume ambao wanateseka katika ndoa kutokana na mapigo na dhiki za kisaikolojia kutoka kwa wake zao? Je ni nani asiyeshuhudia majeraha ya kudhalilisha wanayopagazwa wanaume mashavuni, na hasa moyoni. (uk. 17).

Aidha, Lunga anapoachwa na mkewe Naomi na kuachiwa watoto awalee mwenyewe, anakumbwa na changamoto na dhiki za kisakolojia. Mwaandishi anaeleza kuwa, Lunga hakuweza kustahimili jambo hili ambalo lilimuumiza moyo na kumdhalilisha zaidi. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya mkewe kutoroka, Lunga alilazimika kuwa baba na mama wa watoto wake, jambo ambalo lilikuwa nguvu kwake. Alishindwa kukabiliana na ukiwa wa kuachwa na mkewe. Mwandhisi anasema:

> Katika hali hii Lunga aliingiwa na wahka ambao ulimsababishia kihoro na hatimaye uwele wa shinikizo la damu. Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao (uk. 82).

Vilevile, inaelezwa kuwa, Annette anamwacha mumewe Kiriri na kuhamia ng'ambo bila kujali ukiwa na dhiki ya kuachwa katika upweke wa hali ya juu. Anamnyima haki za unyumba na kumwachwa kwenye simanzi kuu. Mwandishi anasema kupitia kinywa cha Kiriri:

> "Kipi kinachowavutia raia kuhamia ughaibuni?" Angeiuliza nafsi yake pale ambapo mzigo wa simanzi na ukiwa ulipokilemea kifua chake. (uk. 65).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, maelezo haya yanaakisi hali halisi ya jamii. Jinsia ya kiume hukumbana na changamoto ya kupigwa, kudhulumiwa na kupagazwa dhiki za kisaikolojia katika maisha ya kila siku. Hivyo basi, mwanamume anahitaji kutetewa jinsi ambavyo mwanamke hutetewa katika jamii.

### 4.2.9 Ukosefu wa Elimu

Elimu ni mafunzo ambayo hutolewa na jamii kwa watu wake, darasani au pengine pale kulingana na maelezo ya TUKI (2013), elimu ni mafunzo maalum ambayo mtu hupata kutoka shule au vyuoni. Mafunzo haya yanaweza kupatikana kupitia njia rasmi au zisizo rasmi. Elimu rasmi hupatikana kupitia mitaala mbalimbali ya elimu ilhali elimu

isiyo rasmi, hupatikana pasipokuwa na mitaala maalum. Katika riwaya hii, ukosefu wa elimu ni changamoto mojawapo ambayo inaonekana kumfanya mhusika wa kiume kutoyafikia malengo ya kupata maisha bora. Katika jamii ya sasa, elimu ni msingi wa maisha ya binadamu yeyote. Jamii inapokosa elimu hukumbwa na changamoto nyingi katika maisha. Mwandishi anadhihirisha hali hii anaposema:

> Wengi wa vibarua hao walikuwa watoto na vijana wa kiume waliomaliza shule. Hawakubahatika kuendelea na masomo kutokana na ukosefu wa karo (uk. 46).

Mwandishi anaeleza kuwa, ukosefu wa elimu uliwafanya vijana wa kiume kuzurura huku na kule na wengine kujiingiza katika matumizi mabaya ya madawa ya kulevya. Wengine walionekana kumfuata na kumcheka mlevi aliyebwabwaja kwa sauti ya kilevi. Vijana hawa walionekana kama kizazi kilichopotea. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Kila dalili ilionyesha kwamba hawajaona mlango wa darasa la shule. Walivaa mararu. Wengine walikuwa wakivuta vipande vya sigara vilivyotupwa na wapita njia. Mangwasha aliwaona kama kizazi kilichopotea (uk. 34).

Aidha, mwandishi anasema kuwa, katika serikali ya Mtemi Lesulia, wengi walifanya kazi ambazo hawana umahiri na ujuzi wazo. Mwandishi anasema:

> Marubani wengi wa kijeshi waliangusha ndege kila wakati kutokana na mafunzo duni ya urubaini. Nao manahodha wa kijeshi baharini wakapasua vyombo kwenye miamba kwa sababu ya kutindikiwa kitaaluma (uk. 44).

Dondoo hili linadhihirisha ukosefu wa elimu. Nadharia ya uhalisia inadai kuwa, fasihi hulenga kuisawiri picha halisi ya jamii. Mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* ameonyesha hali halisi ya maisha ya sasa. Ukosefu wa elimu ni changamoto inayokwamisha harakati za kujikomboa kwa wanaume dhidi ya manyanyaso na dhuluma wanazofanyiwa. Maoni ya mtafiti ni kuwa, ikiwa jinsia ya kiume itapata

maarifa na ujuzi, jamii itasonga mbele na kuleta mabadiliko ya kiuchumi, kifikra, kijamii na kitamaduni.

### 4.2.10 Umaskini

Mwandishi wa riwaya *Nguu za Jadi* anaonyesha kuwa, miongoni mwa changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume ni umaskini. Changamoto hii inaonekana kuchangia kutofaulu kwa mhusika wa kiume kupata maendeleo ndani ya jamii au taasisi wanazofanyia kazi. Mwandishi anasema kuwa, umaskini nchini Matuo unachochewa na sera mbovu za uongozi wa Mtemi Lesulia. Uongozi wake unatawaliwa na ubaguzi ambao unatokana na jamii mbili hasimu, jambo ambalo linasababisha hali ya umaskini kwa jamii ya Waketwa. Mwandishi anasema:

> Wakule wanafaidi pato la nchi zaidi kutokana na utawala wa Mtemi Lesulia ambaye ni Mkule. Waketwa wanafukarishwa na ubaguzi huo (uk. 50).

Inadhihirika kuwa, kutokana na changamoto ya umaskini vijana wengi wa kiume wanakosa elimu, hali ambayo inasababisha kuzururura mitaani na kujikusanya kwenye viambaza vya maduka wasijue wafanyalo. Mwandishi anasema:

> Wengi walikuwa wamemaliza shule kidato cha nne au darasa la nane. Lakini kutokana na hali ngumu ya maisha ya wazazi wao vijana hao hawakuendeleza elimu yao. Huo ukawa mwisho wao wa kubukua mabuku (uk. 48).

Katika jamii halisi, umaskini ni mojawapo ya changamoto zinazowakabili wanaume. Hivyo, maelezo haya yanaakisi hali halisi ya maisha katika jamii ya leo. Mtafiti anaonelea kuwa, jinsi umaskini unavyosababishwa na ukosefu wa maarifa na ujuzi, jinsia ya kiume isaidiwe kupata elimu ili kuondoa hali ya umaskini na kusonga mbele kiuchumi.

### 4.2.11 Mwanamume anayetekwa Nyara

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, Lonare ambaye Waketwa walimdhani kuwa kiongozi wao amekuwa akipitia mitego mingi na ya hatari sana, anayotegewa na Wakule. Mara nyingi, Lonare ananusurika kifo kutokana na mashambulizi ya watu wanaotumwa kumwangamiza. Lonare anaonekana kuwa shupavu kisiasa na mwenye hekima, jambo ambalo linawatia Wakule wahka. Lonare ana ruwaza njema ya kuwasaidia wenyeji wote wa Matuo bila ubaguzi. Mwandishi anaeleza kuwa, katika uchaguzi wa miaka minne iliyopita, Lonare aliandaa maazimio yaliyowavutia wengi. Maazimio haya yakapigiwa mfano hata na mataifa ya nje. Kutokana na umaarufu na ushupavu wake, wafuasi wake waliamua kumteua ili agombee kiti cha Mtemi, jambo ambalo linasababisha kutekwa nyara na kutoonekana tena mpaka baada ya uchaguzi. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Wakati wa uchaguzi ulipowadia, alitekwa nyara pamoja na vinara wakuu wa chama chake cha kisiasa. (uk. 10).

Kipindi cha uongozi wa Mtemi Lesulia kinapokwisha, uchaguzi mwingine unatangazwa kufanyika ambapo siku chache tu kabla ya uchaguzi huu, Lonare anatoweka kama moshi. Jambo hili linaonekana kuwavunja moyo zaidi wafuasi wa Lonare. Inaelezwa kuwa, mara ya mwisho kuonekana alikuwa akifanya mazoezi ya viungo, mazoezi yaliyohusisha kukimbia akiwa karibu na nyumbani kwake. Mwandishi anasema:

> Habari za kutoweka kwa Lonare na kutoonekana katika hadhara za kisiasa ziliwafadhaisha wafuasi wake. Zilifadhaisha taifa zima. Watu wakaingia katika msako mkubwa. Walisaka kila mahali hata hospitalini na kwenye makafani (uk. 164).

Kwa kurejelea dondoo hili, riwaya ya *Nguu za Jadi* inaakisi halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu, inaeleza mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Ni jambo la kawaida

katika jamii ya sasa kuwa, mtu anapoonekana kuwa shupavu katika jambo fulani kuliko wenzake, wanaweza kumfanyia hila au hata kumwagamiza. Utekaji nyara aghalabu ukithiri wakati wa siasa.

### 4.2.12 Mwanamume kuwa na malezi mabaya

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, kuna wahusika wa kiume ambao wamekosa malezi mazuri. Mwandishi anasema kuwa, mwanawe Mtemi Lesulia, kwa jina Ngoswe, alilelewa kwa kuengwaengwa na kudekezwa pamoja na kuhusishwa na ulanguzi wa dawa za kulevya. Kama inavyoelezwa, Ngoswe aliishi maisha ya faiwashii katika kasri kubwa peke yake mtaani Majuu. Ngoswe hakushughulika kujisulubisha na kazi, kwani ndiye aliyekabidhiwa mamlaka ya kukusanya kodi za majumba mengi aliyomiliki Mtemi Lesulia. Vilevile, alifuja pesa hizo kwa raha na anasa mbalimbali na zilizomfikia mzazi wake ni chache mno. Aidha, tunaona kuwa marafiki zake Ngoswe walikuwa wamekataa shule na kuingilia ulanguzi wa dawa za kulevya. Maneno haya yanathibitisha kuwa, wahusika hawa wa kiume hawakupata malezi yanayostahili kutoka kwa wazazi wao. Mwandishi anadhihirisha hili anaposema:

> Ngoswe alikuwa mwana kindakindaki, akaengwaengwa na kudekezwa kupita kiasi. Ngoswe alikuwa na marafiki wa kitajiri aliotabaradi nao. Wengine walikuwa na uraibu wa dawa za kulevya. Aghalabu ndiye aliyezifahamu njia zote za kuzipata dawa hizo (uk. 122).

Kwa sababu ya kukosa malezi mazuri, wahusika hawa wanaingilia biashara haramu ya ulaguzi wa dawa za kulevya. Dawa hizo hatari husambazwa nchini kisiri. Mwandishi anasema:

> Ziliuzwa hadi kwenye mitaa duni na mawakala ambao walilipwa na Ngoswe na wenzake (uk. 123).

Aidha, Mangwasha anapokuwa katika ziara zake za kumsaka mumewe Ponda Mali, mtaani, anakutana na kundi la vijana ambao walivaa mararu. Kila dalili ilionyesha

kwamba hawajaona mlango wa darasa la shule. Kama inavyoelezwa, wengine walikuwa wakivuta vipande vya sigara vilivyotupwa na wapita njia, hadi eneo likaonekana kukosa maadili mema. Mwandishi kupitia kinywa cha Mangwasha anasema:

> Walikosa malezi bora ya wazazi wao ambao huenda ni walevi, waliopotelea humo mtaani Ponda Mali. (uk. 35).

Riwaya *Nguu za Jadi* inaonekana kuakisi hali halisi ya jamii ya sasa. Ulaguzi wa dawa za kulevya umekithiri katika jamii ya sasa na wengi wa wanaolagua dawa hizi ni wanaume. Msimamo wetu ni kuwa, hatua ichukuliwe kukomesha uuzaji wa dawa za kulevya ambazo zinaleta madhara mbalimbali kwa jinsia ya kiume ulimwenguni.

## 4.3 Namna Changamoto zinazomkabili Mhusika wa Kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake katika Riwaya Teule

Riwaya teule zimeonyesha kuwa, changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinamwathiri yeye binafsi na jamii yake. Changamoto zilizojadiliwa katika sehemu iliyotangulia, athari zake zimeonyeshwa katika sehemu ifuatayo.

### 4.3.1 Athari za Ukosefu wa Nafasi za Kazi

Utafiti huu umebaini kuwa, ukosefu wa nafasi za kazi katika jamii ya Wahafidhina unaleta athari ya umaskini kwa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri.* Athari hii inachangia wahusika hawa kushindwa kumudu maisha yao. Athari hii inadhihirika kupitia kinywa cha mja, anaposema:

> "Tunawanasihi akina mama kuwapigia kura viongozi ambao hata wanatiririkwa na machozi wanapoona ngozi zetu zilivyopauka na kujaa makunyazi kwa ulitima kumbe machozi yenyewe ni ya mamba" (uk. 22)

Aidha, umaskini unaotokana na changamoto za ukosefu wa nafasi za kazi, na kuwafanya wahusika wa kiume kutumiwa vibaya na viongozi kama vile kwenda kuwafanyia kampeni. Kupitia kinywa cha yule mwanaharakati aliyevaa shati lililoandikwa '*Hitman*' mgongoni, mwandishi anasema:

> Tunasombwa kama taka kwenda kuwafanyia kampeni. (uk. 22)

Kutokana na ukosefu wa nafasi za kazi kwa wahusika wa kiume, jamii pia inaadhirika kwa ulitima. Aidha, changamoto ya ukosefu wa nafasi za kazi zinasababisha mhusika wa kiume kukata tamaa na kuambulia uraibu wa pombe. Athari hii inaonekana kupitia kwa mhusika Shamsi ambaye amesoma mpaka chuo kikuu, lakini kwa sababu ya kukosa nafasi ya kazi anaingilia ulevi na kuwa mlevi wa kupindukia. Anapolewa, Shamsi anaonekana kuimba wimbo ambao unasema:

> Kwani hawakunipa nyenzo za kujiendeshea maisha? Kwani walitupuuzilia mbali tulipolilia kuhiniwa? Nafasi za kazi zilipotwaliwa na ndugu zao huku tukiambiwa kindanindani "Viganja huoshana, aso mwana aeleke jiwe! (uk. 133).

Kutokana na wimbo wa mhusika Shamsi, ni kweli kuwa changamoto hii ya ukosefu wa nafasi za kazi, imemwathiri kwa kukosa pesa ya kuendesha maisha yake. Jamii ya Shamsi nayo inaathirika kwa kukosa maendeleo ambayo angeyaleta Shamsi kama angekuwa ameajiriwa. Mwandishi anasema kuwa, kidogo anachopata anapeleka ulevini badala ya kuiauni jamii yake. Riwaya ya *Chozi la Heri* inaonekana kuakisi hali halisi ya jamii. Katika maisha ya sasa, wanaume wanapokosa nafasi za kazi hukata tamaa na kuingilia ulevi ili kujisahaulisha na mambo wanayopitia maishani. Jamii nyingi zimekosa maendeleo kama athari ya changamoto ya ukosefu wa nafasi za kazi.

Kwa upande wa riwaya ya *Nguu za Jadi*, vijana wengi wa kiume waliohitimu shahada za vyuo vikuu, wanahangaika mijini kutafuta kazi bila kufanikiwa. Hivyo basi vijana

hawa wanakosa matumaini na kuacha kutuma maombi ya kazi serikalini. Kwa sababu ya ukosefu wa ajira, vijana wa kiume wanaonekana kuzurura tu katika barabara za mji wasijue wafanyalo. Hata hivyo, vijana wengi waliokosa ajira ni jamii ya Waketwa. Inaelezwa kuwa, vijana hawa wa kiume wanashindwa kuyamudu maisha yao kwa sababu hawana ajira. Changamoto hii inaathiri maisha yao. Jamii nayo inaathirika kupitia changamoto hii kwa sababu wizi unaongezeka mijini. Vijana wa kiume wanapokosa ajira wanajihusisha na uhalifu kama vile kupora mali. Hali hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Wengine walizurura tu katika baraste za mji wasijue wafanyalo. Vibaka nao walikuwa wakisubiri fujo au ghasia fulani zizuke mjini ili wapate nafasi ya kunyang'anya watu mali zao au kupora maduka (uk. 48).

Kupitia changamoto ya ukosefu wa ajira, mustakabali wa mhusika wa kiume unaonekana kuathirika kama ambavyo mwandishi anatuonyesha kupitia kinywa cha Mangwasha:

> "Hawa watakuwa wanaume wenye kutunza jamaa zao kweli? Watategemewa na nani maishani?" (uk. 49).

Aidha, athari nyingine inayotokana na changamoto ya ukosefu wa ajira ni hali ngumu ya maisha ambapo mhusika wa kiume anashindwa kujiendeleza. Kutokana na ukosefu wa ajira, wahusika wa kiume wanaonekana kushindwa kujimudu na kuwajibikia familia zao. Mwandishi anasema:

> Mangwasha aliwaona vijana hao kama kizazi kinachopotea. Alijiuliza kama vijana hawa watakuwa baba wa aina gani. Je, wataweza kuzihimili familia zao iwapo hata wao wenyewe wanahitaji kuhimiliwa? Baadhi yao wangekuwa na familia zao kwani walikwishafikia umri wa kuoa. (uk. 137).

Umaskini na utumiaji mbaya wa dawa za kulevya kama athari ya changamoto hii unajidhihirisha mwandishi anaposema:

> Wengine walikuwa vijana ambao walihitimu vyema katika masomo. Lakini kwa sababu ya ukosefu wa ajira na ulitima mwingi miongoni mwa wazazi wao; wameishia majiani na mitaani, wakivuta bangi na kupora mali za watu. (uk. 137).

Kwa kurejelea dondoo hili, inabainika kwamba, changamoto ya ukosefu wa ajira inamfanya mhusika wa kiume kukosa njia za kujiendeleza kimaisha, nayo jamii inaathirika kwa kukosa maendeleo. Kushindwa kuoa kwa mwanaume kunaashiria kukosekana kwa kizazi kipya katika jamii, hivyo jamii inaathirika. Riwaya teule inaonekana kuakisi hali halisi ya maisha ya leo, ambapo vijana wengi huzurura mitaani kwa kukosa ajira. Kwa hivyo, ukosefu wa ajira ni jambo ambalo linaonekana katika jamii ya leo na madhara yake kwa wanaume na jamii ni yale ambayo yamebainika katika utafiti huu. Mapendekezo yetu ni kwamba, hatua ichukuliwe ili kuepukana na madhara ya ukosefu wa nafasi za kazi.

### 4.3.2 Athari za Usaliti kwa Mhusika wa Kiume

Kupitia riwaya ya *Chozi la Heri*, uhakiki unaonyesha kuwa, usaliti huleta madhara kwa mtu binafsi na jamii yake. Athari ya changamoto hii inadhihirishwa na Lunga anaposalitiwa na shirika la Maghala ya Fanaka. Inaelezwa kuwa, licha ya kujitolea kulifanyia kazi kwa bidii shirika hili, anafutwa kazi kwa sababu ya kupinga kitendo cha raia kuuziwa mahindi ya manjano kutoka ughaibuni. Baada ya usaliti huu, Lunga anaathirika kwa sababu anakosa pesa na maisha yake kubadilika, hali ambayo inamfanya mkewe Naomi kumtoroka na kumuachia watoto. Alionekana kumtumia mumewe ujumbe mfupi, ambao uliashiria mwanzo wa mkondo mpya wa maisha ya familia yake:

> “Nimeondoka. Acha nitambe na ulimwengu (uk. 81).

Aidha, usaliti wa Naomi kwa mumewe na watoto unawaletea madhara ya aina mbalimbali. Kwanza, Lunga anashindwa kustahimili changamoto hii ya upweke unaomsababishia kihoro na hatimaye anafariki kutokana na ugonjwa wa shinikizo la damu. Inaelezwa kuwa, kifo cha Lunga kinatokana na madhara ya usaliti wa mkewe. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Lunga aliingiwa na wahka ambao ulimsababishia kihoro na hatimaye uwele wa shinikizo la damu. Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao (uk. 82)

Hali kadhalika, watoto wa Lunga wanaonekana kuathirika na changamoto hii ya usaliti. Inaelezwa kuwa, baada ya baba yao mlezi kufariki wanapitia matatizo mengi zaidi. Dick na Mwaliko wanatoroshwa na kijakazi Sauna huku Umulkheri akibaki peke yake, akizunguka kuwatafuta huku na kule asifanikiwe kuwapata. Mwandishi anasema:

> Asubuhi moja Umu aliamka na kujipata yu pweke nyumbani mwao. Ndugu zake wawili Dick na Mwaliko, walikuwa wametoweka (uk. 82).

Kwa mujibu wa nukuu hii, inaonekana kusadifu hali halisi ya jamii ya sasa ambapo usaliti umekithiri.

Aidha, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, changamoto ya usaliti inasababisha kutoelewana kwa Mashauri na Sagilu. Inaelezwa kuwa, Mashauri anapofahamu kuwa baba yake ana uhusiano wa kimapenzi na Cheiya, hali hii inazua uhasama kati yao. Isitoshe, jambo hili linamtenganisha Mashauri na Cheiya. Athari ya changamoto hii inadhihirika kupitia kinywa cha Mashauri:

> “Kuanzia leo…Kuanzia leo mimi sikutambui kama mzazi wangu tena. Kama ni urithi wako, mpelekee Cheiya mkaishi naye. Don’t call me your son ever again. Unasikia?” Mashauri alifoka na kutoka pale mbio (uk. 122).

Kulingana na nukuu hii, inaeleweka kuwa, changamoto ya usaliti imemwathiri mhusika wa kiume kwa sababu inaleta uadui kati yake na wanafamilia. Aidha, kutengana kwa Cheiya na Mashauri kulitokana na changamoto ya usaliti. Tena, jamii inaathirika wakati wanafamilia hawana uhusiano mwema katika jamii yao. Usaliti ni jambo la kawaida katika jamii zetu na una madhara kama tuliyoyabaini katika utafiti huu.

### 4.3.3 Athari za Ulevi

Ulevi unaleta madhara ya maaafa katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Inaelezwa kuwa, Kipanga ananusurika kutokana na madhara ya pombe inayosemekana kuwa iliwaua watu sabini. Maneno haya yanaonyesha kuwa, changamoto ya ulevi inaleta vifo kwa wahusika wa kiume. Maafa haya yanaathiri jamii inayoachwa na watu wao. Mwandishi kupitia Selume anasema:

> Yeye alinusurika kifo kutokana na kangara iliyowaua watu sabini mwezi uliopita (uk. 143).

Aidha, kwa sababu ya ulevi, Shamsi anaonekana kutembea kuelekea nyumbani kwake usiku wa manane. Shamsi anapita akiimba usiku bila kujali kwamba wimbo wake unawasumbua waliolala. Hivyo tabia yake ya kilevi inaiathiri jamii yake. Mwandishi anasema:

> Haidhuru kuwa huenda wimbo huu unawaghasi waliolala. Atakalo mwimbaji huyu ni kuzitakasa hisia zake (uk. 129).

Vilevile, inadhihirika kuwa, tabia ya kilevi inamwathiri Shamsi na familia yake ambao wanaishi maisha ya kubahatisha tu. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Daraja kubwa limeutenga mtaa huu na mtaa wa Kazikeni ambako familia ya Shamsi na nyingine za aina yake zinakoishi. La! Haziishi, zinaambuila maisha ya kubahatisha tu. (uk. 138).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, athari zinazotokana na ulevi katika jamii halisi, zinafanana na zile ambazo zimetajwa.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi***,** athari mojawapo ya changamoto ya ulevi inajidhihirisha kupitia kwa mhusika Mrima anapoingilia ulevi na kusahau kutunza familia yake. Kutokana na ulevi wake, mkewe na watoto wanapitia matatizo mengi. Mwandishi anasema kuwa, watoto walimsumbua mama yao wakitaka kujua aliko baba yao. Mwandishi anasema:

> Mrima alianza kushiriki ulevi akawa anakesha katika vilabu vya pombe. Watoto walishinda kumsumbua mama yao. Walitaka kujua aliko baba yao (uk. 27).

Kwa kurejelea dondoo hili, familia ya Mrima iliathirika kutokana na ulevi wake. Aidha, changamoto hii ya ulevi ilimwathiri Mrima zaidi kwa sababu ilisababisha kufutwa kazi. Kama inavyoelezwa, Mrima alianza kuhepa kazi na kupotelea ulevini jambo ambalo lilimpeleka kupigwa kalamu. Mwandishi anasema:

> Mwishowe Mrima alikosa kufika kazini mara kwa mara. Alianza kuhepa kazi na kupotelea ulevini (uk. 27).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, ni kweli kuwa, ulevi kati ya wanaume umekithiri na athari zake zinafanana na zile ambazo zimebainika katika utafiti huu. Kulingana na mtafiti, athari za ulevi hazihesabiki. Hatua ichukuliwe kukabiliana na changamoto ya ulevi ili kuepukana na athari hizi.

### 4.3.4 Athari za Utelekezaji wa Mwanamume

Utelekezaji ni mojawapo ya changamoto katika riwaya teule, ambayo inaleta athari kwa mhusika wa kiume pamoja na jamii yake kwa njia mbalimbali. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, hakuna anayewakinga wala kuwatetea wahusika wa kiume, kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Hivyo basi, wahusika wa kiume wanateseka katika ndoa

kutokana na mapigo na dhiki za kisaikolojia. Isitoshe, maghulamu wanalawitiwa, jambo ambalo linaathiri jamii kwa jumla. Mwandishi anadhihirisha athari ya kutelekezwa kwa jinsia ya kiume kupitia kinywa cha Tetei:

> "Lakini ni wangapi wanaokumbuka kuwa hata maghulamu wanalawitiwa? Ni wangapi wanaowatetea mamia ya wanaume ambao wanateseka katika ndoa kutokana na mapigo na dhiki za kisaikolojia kutoka kwa wake zao? (uk. 17).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa, kutokana na changamoto ya utekelezaji, mhusika wa kiume katika riwaya teule anaathirika pamoja na jamii yake.

Halikadhalika, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume anaonekana kukosa matumaini katika maisha kwa sababu ya kutelekezwa. Mwandishi kupitia kinywa cha Mangwasha anadhihirisha hayo:

> "Lazima tujirudi tuone ni wapi tulipoanza kupotea njia. Lazima tuokoe kizazi hiki kinachopotea nyikani bila matumaini. Ole wako Matuo, utashika mti gani?" (uk. 138).

Hata hivyo, jamii ya Matuo inaathirika kwa kukosa wanaume wanaoweza kutengemewa siku za usoni. Hii ni kwa sababu, wanaume waliopo wamekosa matumaini katika maisha yao na kuingilia matumizi mabaya ya vileo, huku wengine wakishindwa kuyamudu maisha yao na familia zao. Mwandishi anasema kuwa, Mangwasha alikuwa akiwaonea huruma vijana hao, ambao aliwaona kama kizazi kilichopotea kama anavyosema:

> "Je, hawa wangeweza kuwa raia wa kuaminiwa kesho kweli?" (uk. 34)
> "Hawa watakuwa wanaume wenye kutunza jamaa zao kweli?" (uk. 49).

Nadharia ya uhalisia inadai ya kwamba, fasihi ieleze mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Katika jamii ya sasa, jinsia ya kiume inaathirika kutokana na changamoto ya kutelekezwa katika jamii. Katika jamii ya mtafiti, vijana wa kiume wameingilia

matumizi mabaya ya vileo na kuwa watu wasioweza kutengemewa maishani. Wamekosa mwelekeo katika maisha yao na kushindwa kuyamudu maisha yao wenyewe. Atieno (2019) anasema ya kwamba, kupuuzwa kwa jinsia ya kiume kumechangia hali yao ya upweke kwani hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike.

Katika nadharia ya Uhalisia mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii umetumika kuongoza utafiti huu. Utafiti unaonesha kuwa, Ngoswe na wenzake wamechorwa walivyo kulingana na jamii ya sasa. Mtoto anapodekezwa, akikua na kuwa mtu mzima, anafanya mambo ya kuwaumiza wazazi wake na jamii kwa jumla, ila wanashindwa kuvisahihisha kwa sababu wanakuwa wameishachelewa. Aidha, inadhihirika kuwa, jamii ya Matuo ina matukio yanayolingana na hali halisi iliyopo. Mara nyingi wenye pesa, yaani matajiri, huwalea watoto wao vibaya na kutumia pesa zao kununua haki. Mwandishi anasema kuwa, wakuu wa serikali hawakuwa na uwezo wa kumkamata wala kumshtaki Ngoswe, licha ya kuwa mlanguzi wa dawa hatari za kulevya kwa sababu ni mwanawe Mtemi. Kulingana na maoni ya mtafiti, kumtelekeza mwanamume ni jambo hatari na ni lazima jamii ijirudi ione ni wapi ilipoanza kupotea njia. Aidha kizazi hiki kiokolewe ili kupata raia wa kuaminika kesho, na wanaume wenye kutunza jamaa zao.

### 4.3.5 Athari za Mapigo na Dhiki za Kisaikolojia

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa, kuna wanaume ambao wanateseka katika ndoa zao kutokana na mapigo na dhiki za kisaikolojia wanazopata kutoka kwa wake zao. Utafiti umeonesha kuwa, mojawapo ya athari inayotokana na changamoto hii kwa wanaume ni majeraha wanayopata kutokana na udhalilishwaji huu. Kupitia mwanaharakati Tetei, mwandishi anasema:

> Je, ni nani asiyeshuhudia majeraha ya kudhalilisha wanayopagazwa wanaume mashavuni, na hasa mioyoni? (uk. 17).

Aidha, Naomi anapomtoroka mumewe na kumnyima haki za unyumba na kumwachia upweke anampagaza dhiki ya kisaikolojia. Dhiki hii ya kisaikolojia inamwathiri Lunga hadi anafariki kutokana na uwele wa shinikizo la damu. Mwandishi anasema:

> Kabla ya mwisho wa mwaka huo, Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao (uk. 82).

Inadhihirika kwamba, baada ya Lunga kufa, watoto wake wanabaki wakiteseka. Dick na Mwaliko wanatoroshwa na kijakazi Sauna ambapo, Dick anapelekwa kwa Buda anayemlazimisha kumsaidia kazi ya ulanguzi wa dawa za kulevya. Mwandishi anasema:

> Siku hiyo kiwewe kilikuwa kimemkumbatia kwani kazi ya kubeba dafina, kama walivyoita biashara haramu ambayo alikuwa kalazimishwa kufanya siku hizo, ilikuwa imewaingiza wengi kwenye nyavu na madema ya polisi, wakatiwa mbaroni (uk. 119).

Hivyo, kutokana na changamoto ya dhiki za kisaikolojia inayomkumba Lunga na kumsababishia kifo, watoto wake wanabaki kuteseka. Katika jamii halisi, wanaume hupitia changamoto za mapigo na dhiki za kisaikolojia ambapo athari zake huwa kama tulizozitaja hapo juu. Hivyo basi, fikira kuwa wanawake ndio hupitia dhiki na mapigo katika ndoa ni potovu.

### 4.3.6 Athari za Ukosefu wa Elimu

Ukosefu wa elimu bora unachangia ukosefu wa ajira miongoni mwa wahusika wa kiume. Ingawa wahusika wengi wa kiume kutoka jamii ya Waketwa na waliosoma na kuhitimu walikosa kazi, wengine walikuwa na changamoto ya kukosa elimu pia. Inaelezwa kuwa, waliokosa elimu walionekana kuzurura huku na kule, wengine

wakivuta sigara. Hivyo, athari mojawapo ya kukosa elimu inaonekana kuwa ni vijana wa kiume kuzurura ovyo ovyo mitaani na kuvuta sigara. Mwandishi anasema:

> Nyuma yake alifuatwa na kikundi cha vijana watundu waliomcheka na kusikiliza aliyoimba. Kila dalili ilionyesha kwamba hawajaona mlango wa darasa la shule. Walivaa mararu. Wengine walikuwa wakivuta vipande vya sigara vilivyotupwa na wapita njia (uk. 34).

Hata hivyo, inadhihirika kuwa, Wakule hata wale ambao hawakuhitimu ipasavyo walikuwa wanapewa nafasi za kazi kwa sababu ya ukabila. Mketwa aliyehitimu angenyimwa kazi na kupewa Mkule asiyehitimu. Mwandishi anasema kuwa, jeshi la nchi ilijaa vijana wa kiume kutoka katika jamii ya Wakule. Kutokana na hilo, changamoto ya ukosefu wa elimu ilianza kuathiri jamii hii. Mwandishi anasema:

> Marubani wengi wa kijeshi waliangusha ndege kila wakati kutokana na mafunzo duni ya urubani. Nao manahodha wa kijeshi wakapasua vyombo kwenye miamba kwa sababa ya kutindikiwa kitaaluma (uk. 44).

Kwa kurejelea dondoo hili, inadhihirika kwamba, ukosefu wa elimu katika jamii halisi unasababisha athari ambazo zimetajwa. Hivyo riwaya teule inaakisi hali halisi ya maisha ya sasa ambapo wanaume wengi wanaathirika kwa kukosa elimu. Mtafiti anaonelea kuwa, kuna haja ya mwanaume kupata elimu ili kuepukana na athari za changamoto hii.

### 4.3.7 Athari za Ukosefu wa Matumaini

Matokeo yanaonyesha kuwa, ukosefu wa matumaini unaleta madhara mbalimbali kwa mhusika wa kiume na jamii yake katika riwaya teule. Kwanza, vijana wa kiume waliokosa matumaini wanaonekana kuzururua ovyoovyo mjini, huku wakipoteza muda wao katika viambaza vya maduka. Vijana hawa wa kiume wanaonekana kuathirika na changamoto ya ukosefu wa matumaini kwa sababu hawafanyi lolote la kuwandeleza kimaisha. Isitoshe, jamii inaathirika kwa kuwa, vijana ambao wangekuwa wanafanya

kazi kuzalisha rasilimali za kuendeleza jamii wanazurura bila kufanya lolote, hivyo jamii inakosa maendeleo. Inaelezwa kuwa, kwa sababu ya kukosa matumaini kwa jinsia ya kiume, mizozano ya kifamilia inakithiri na wanandoa kuuana. Mwandishi anasema:

> Asasi ya familia ikaathirika sana pale mizozano ya kifamilia inapokithiri. Wanaume kwa wake wakawa makatili kiasi cha kuagamiza makinda yao. Mume akamgeukia mke na kumchinja naye mke akafanya vivyo hivyo. Mauaji ya kifamilia yakawa matukio ya kila siku (uk. 47).

Dondoo hili linadhihirisha wazi athari ya ukosefu wa matumaimi kwa mhusika wa kiume, ambaye amekosa mwelekeo. Inaonekana kuwa, ukosefu huu wa matumaini unasababisha maafa katika jamii yake. Riwaya ya *Nguu za Jadi* inaonyesha hali halisi ya jamii ya sasa. Vijana wengi wa kiume wanaathirika kutokana changamoto hii ya kukosa matumaini, na ambao wanaonekana kuzururua mitaani ovyoovyo wasijue la kufanya. Jamii ya sasa inaathirika kwa kukosa maendeleao ambayo yangeletwa na vijana hawa, ambao wamepotelea mitaani na ulevini kwa kukosa matumaini maishani. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, hatua ifaayo ichukuliwe ili kuepukana na athari hizi.

### 4.3.8 Athari za Utekaji Nyara

Ni jambo la kawaida kuwa mtu anapotekwa nyara huwa hana uhuru wa kutangamana na wenzake na kufanya mambo ayatakayo. Hivyo, mtu huyu ataathirika. Isitoshe, watu wa familia yake pamoja na wenzake hukosa amani kwa kutojua aliko, na kuhangaika kumtafuta huku na kule. Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, kutekwa nyara kwa Lonare pamoja na vinara wakuu wa chama chake cha kisiasa kunamwathitri kwa sababu anakosa nafasi ya kuchaguliwa kama Mtemi wa nchi ya Matuo. Mtemi Lesulia anaingia mamlakani bila kupingwa na yeyote. Mwandishi anasema:

> Hakuonekana mpaka baada ya uchaguzi. Wafuasi wake walitawanyika. Wakamtusi kwa kuwatelekeza katika dakika ya mwisho. Marafiki zake wa karibu walimwita msaliti. Wakasusia hata kupiga kura. Mtemi Lesulia akachaguliwa bila kupigwa! (uk. 10).

Mwandishi anaeleza kuwa, wafuasi na marafiki zake pamoja na jamii nzima ya Waketwa wanaathirika sana na utekaji nyara huu. Walionekana sasa kama kundi la kondoo lisilokuwa an mchungaji. Walionekana kufadhaika, kuhangaika na kumsaka ila hawakufanikiwa kumuona, wala hata kumsikia popote. Jambo hili lilifadhaisha nchi nzima. Mwandishi anasema ya kwamba, taharuki iliwavaa wakihofia usalama wa Lonare. Maskani yake Lonare sasa ikajaa umati wa watu, wengine wakiomboleza na wengine wakiangua vilio ni kana kwamba kifo kimezuru makazi yao. Isitoshe, vyombo vya habari vilisikika kutangaza kutoweka ghafla kwa Lonare. Kutokana na maelezo haya, changamoto hii iliyomkumba Lonare pamoja na vinara wakuu wa chama chake cha kisiasa, inaonekana kumwathiri pamoja na jamii yake. Mwandishi anasema:

> Wafuasi wake wakawa kama kondoo waliopoteza mchungaji. Wakaanza kutawanyika huku na huko. Mangwasha na Mbungulu wakaangua kilio walipopata habari za kupatikana kwa vitu vya Lonare (uk. 164).

Aidha, Lonare anaonekana kuathirika sana na utekaji nyara huu. Waliomteka nyara walimdhulumu na kuumiza mwili wake zaidi. Siku ile ya uchaguzi inapofika, Lonare anapatikana karibu na kizingiti cha mlango wa nyumba ya Mrima, kalala kifundifundi huku mwili wake ukiwa na majeraha mengi. Mwandishi anadhihirisha hili anaposema:

> Miguuni kadungwadungwa utadhani alitembea juu ya misumari. Miguu hiyo ilikuwa imefura mithili ya mtu aliyepiga milundi mwendo mrefu (uk. 170).

Kwa kurejelea nukuu hapo juu, ni kawaida kuwa, mmoja wa wanajamii anapopotea au kutekwa nyara, wanajamii wenzake huwa na huzuni na kumtafuta mpaka apatikane.

#### 4.3.9 Athari za Malezi Mabaya

Malezi mabaya ni changamoto ambayo inaleta madhara mengi kwa mhusika wa kiume na jamii yake katika riwaya teule. Mwandishi wa riwaya ya *Nguu za Jadi* anasema kuwa, kwa kutopata malezi yanayofaa, marafiki wa kitajiri wa Ngoswe wanaathirika. Inaelezwa kuwa, wanakataa shule na kuishi kama wafalme kwenye makasri ya wazazi wao huku wengine wakilangua dawa za kulevya. Mwandishi anasema:

> Ngoswe alikuwa na marafiki wa kitajiri aliotabaradi nao. Wengine wao walikuwa wamekataa shule, wakaishi kama wafalme kwenye makasri ya wazazi wao. Wengine walikuwa na uraibu wa dawa za kulevya (uk. 122).

Aidha, Ngoswe anaathirika na kujiingiza katika uraibu wa madawa ya kulevya na anasa mbalimbali, pamoja na kuendeleza biashara haramu nchini Matuo. Mwandishi anasema:

> Ngoswe aliwekeza fedha alizovuna katika biashara hiyo haramu kwenye majumba ya starehe na anasa (uk. 123).

Hali kadhalika, kutokana na malezi mabaya ya wahusika wa kiume nchini Matuo, jamii inaathirika. Mwandishi anaeleza kuwa, Ngoswe na wenzake walichuuza dawa hizo hatari katika shule na vyuo vikuu, jambo ambalo linasababisha watoto na vijana wengi nchini Matuo kuharibika na wengine kupoteza maisha yao. Inaelezwa kuwa, sumu hizo zilikuwa tisho kwa usalama na ustawi wa nchi. Mwandishi anasema:

> Zilichuuzwa kwa siri katika shule na vyuo nchini. Zikaharibu watoto na vijana wengi nchini. Wengine wakaishia kuwa mazumbe tu, yasiojifahamu. Wengine nao wakaacha shule, wakawa wazururaji tu mjini (uk. 123).

Kwa kurejelea dondoo hili, katika jamii halisi vijana wameingilia matumizi mabaya ya vileo, na wengine kuacha shule kutokana na malezi mabaya. Maoni ya mtafiti ni kwamba, watoto wa kiume wapewe malezi mazuri ili kuepukana na athari zilizotajwa hapo juu.

### 4.4 Hitimisho

Sura hii imegawanywa katika sehemu tano kuu, na inahusu uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu na pia kufanya mjadala. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa sura ya nne. Sehemu ya pili inahusu ubainishaji wa usawiri wa mhusika kwa kiume katika riwaya teule ambazo ni, *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Sehemu ya tatu inahusu ubainishaji wa changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule. Sehemu ya nne, inahusu ubainishaji wa namna changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake katika riwaya teule. Sehemu ya mwisho ni muhtasari wa sura ya nne.

# SURA YA TANO

# HITIMISO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti anatoa hitimisho  kwa kufafanua matokeo ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti huu. Halikadhalika, mtafiti anawasilisha majibu ya maswali na makisio yaliyomo katika sura ya kwanza kwa kuzingatia nadharia ya uhalisia. Mwisho, mapendekezo yametolewa kwa ajili ya watafiti wengine watakaofuata.

## 5.1 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Utafiti huu ulilenga kuyatimiza malengo matatu; lengo la kwanza ni kuchunguza jinsi mhusika wa kiume anavyosawiriwa katika riwaya hizo. Utafiti huu umebaini kuwa, riwaya ya *Chozi la Heri* Matei (2017) na *Nguu za Jadi* zimemsawiri mhusika wa kiume katika nyanja mbalimbali za maisha. Katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*, mhusika wa kiume amesawiriwa kama; aliyetelekezwa katika jamii, aliyekosa matumaini, aliyekosa nafasi katika jamii, mvumilivu, aliyelemewa na ulevi, mwenye bidii, kiongozi wa familia, mwenye mapenzi ya dhati kwa mkewe, kiumbe asiye na hisia na anayebaguliwa kwa misingi ya kiukoo. Hata hivyo, usawiri huu unakanganya kwa kuwa anaoneshwa akiwa na mapenzi ya dhati kwa mkewe huku pia akisawiriwa kwamba ni kiumbe asiye na hisia.

Waandishi wa riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi* wameonyesha mtazamo mpya kuhusu nafasi ya mwanaume katika jamii ya sasa. Hata hivyo, riwaya za *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi* zinatoa mwelekeo mpya wa uandishi, ambapo wahusika wa kiume

wanakutana na jamii iliyobadilika kiwakati, ambapo wao wenyewe wanatelekezwa na kukumbana na changamoto mbalimbali maishani mwao. Mwelekeo huu unalenga kuonyesha jinsi mabadiliko ya kijamii yanavyoathiri nafasi ya mwanamume, akiishi katika mazingira ya mvutano na changamoto zinazomhusisha na mabadiliko ya kijinsia na kijamii.

Lengo la pili lilikuwa kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule. Imekuwa hali ya mazoea kuona jinsia ya kike ikisawiriwa kwa kiasi kikubwa na kuonyeshwa namna inavyoonewa na kudhulumiwa katika tafiti tangulizi. Jinsia ya kiume huonekana kama iliyokamilifu na isiyokabiliwa na changamoto yoyote. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kinyume na mtazamo huo kwamba wahusika wa kiume wanakabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha. Baadhi ya changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya teule ni pamoja na: Ukosefu wa nafasi za kazi, kutelekezwa katika jamii, ukosefu wa matumaini, kutopewa nafasi katika jamii, kutumikishwa n.k. Imebainika kuwa, changamoto zinazoonyeshwa katika riwaya hizi zinasadifu uhalisia katika jamii, yaani ni uhalisia unaopatikana katika jamii ya sasa. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, mwanamume anahitaji kutetewa jinsi ambavyo mwanamke hutetewa na jamii.

Lengo la tatu lilikuwa kuonyesha jinsi changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume zinavyomwathiri binafsi na jamii yake. Utafiti umebaini kuwa, mhusika wa kiume anaathirika pamoja na jamii yake, kutokana na changamoto zinazomkabili katika riwaya husika. Imedhihirika kuwa, changamoto ya ukosefu wa nafasi za kazi inawafanya wahusika wa kiume kuwa maskini na kushindwa kuyamudu maisha yao pamoja na jamaa zao. Aidha, kukosa ajira kunawafanya wahusika wa kiume kuingilia matumizi mabaya ya dawa za kulevya ili kujisahaulisha na hali wanayoipitia. Hali

ilivyo ndani ya riwaya teule ndivyo inavyoonekana katika jamii halisi. Mustakabali wa mwanamume katika jamii ya mtafiti unaonekana kuathirika kwa sababu ya kukosa ajira. Baadhi ya wanaume wamekosa matumaini na kuzurura mijini huku wakisubiri ghasia fulani zizuke wapate nafasi ya kunyang'anya watu mali zao au kupora maduka, ambapo jamii inaathirika. Utafiti umebaini kuwa, kutelekezwa kwa mhusika wa kiume katika riwaya teule kunamfanya kukosa matumaini ya kuishi, ambapo mizozano ya kifamilia inakithiri na wanandoa kuuana.

Ulevi kama changamoto inayomkabili mhusika wa kiume, ina madhara kwake pamoja na jamii yake. Madhara hayo ni kama vile; kufutwa kazi, kifo, mizozano ya kifamilia na kadhalika. Halikadhalika, kutokana na malezi mabaya, vijana wengi wa kiume wanaharibika na wengine kupoteza maisha yao.

Imedhihirika kuwa, jinsia ya kiume imetelekezwa katika jamii, yaani hakuna dira mahususi ya kumwongoza mtoto wa kiume. Vilevile, maandiko yanayomfunza mtoto wa kiume jinsi ya kuishi na kutangamana na mazingira yake ni machache mno. Aidha, jamii imeshika mkono mtoto wa kike, ikapiga mbio na mtoto wa kike huku mtoto wa kiume akisahaulika. Isitoshe, kutokana na kutelekezwa huku, mhusika wa kiume anakumbwa na changamoto mbalimbali, ambazo zinamwathiri binafsi na jamii yake. Hali inavyoonyeshwa katika riwaya teule ndivyo ilivyo katika jamii halisi ambapo, madhara yanayotokana na changamoto zinazomkabili mwanamume katika jamii hayahesabiki. Tasnifu hii inatarajiwa itakuwa kichocheo cha watafiti wa baadaye wa fasihi kuchunguza masuala yanayohusiana na jinsia ya kiume ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikisahaulika katika tafiti na tahakiki. Halikadhalika, ni matumaini yetu kuwa kutokana na tasnifu hii, jamii itabaini changamoto mbalimbali zinazoikabili jinsia ya kiume na athari za changamoto hizo na itabuni mikakati ya kukabiliana nazo.

Utafiti huu umeangazia masuala ya jinsia ya kiume, jambo ambalo linahusu jamii kwa jumla. Watafiti wa fasihi watafaidi maarifa mapya kutokana na utafiti huu. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatawafaa wasomi na hata waandishi wa fasihi wanapofanya uhakiki wa kazi za fasihi na hata wanapoandika kazi za kifasihi. Vilevile, utafiti huu ni muhimu kwa wanafasihi kwa jumla, na wapenzi wa masuala ya kiuana. Halikadhalika, utafiti huu utakuwa kichocheo na rejea muhimu kwa watafiti wa baadaye kuchunguza masuala ya jinsia ya kiume.

Kuongeza uelewa wa taswira za kiume katika fasihi za Kiswahili: Utafiti umeonyesha namna wahusika wa kiume wanavyojengwa kifikra na kihisia katika riwaya hizo, na jinsi usawiri huo unavyoakisi au kuibua changamoto kwa mitazamo ya kijinsia ya jadi na ya kisasa.

Kutoa mchango katika tafiti za fasihi na jinsia: Uchambuzi umeongeza ujuzi juu ya jinsi wahusika wa kiume wanavyosawiriwa kisanaa na kiutamaduni katika fasihi, na hivyo kusaidia wasomaji na watafiti kuelewa zaidi mienendo ya kijinsia katika muktadha wa riwaya hizi.

Kusaidia kujenga mjadala kuhusu usawa wa kijinsia na mabadiliko ya mitazamo: Matokeo ya utafiti yanaweza kusaidia wasomaji, walimu, na watafiti kuzingatia kwa undani zaidi masuala ya jinsia, na hivyo kuchochea mijadala ya kijamii kuhusu usawa na haki za kijinsia kupitia fasihi.

## 5.2 Waathirika wa Mchango wa Utafiti Huu:

Watafiti na wanafunzi wa fasihi: Watapata maarifa mapya na mbinu za kuchambua wahusika wa kiume katika fasihi za Kiswahili.

Walimu na wasomaji: Utafiti huu utawasaidia kuelewa zaidi muktadha wa kijinsia katika kazi za fasihi na kuhamasisha mijadala ya kijinsia darasani na nje ya darasa.

Wanafunzi wa masuala ya jinsia: Watapata taswira za kina kuhusu jinsi jinsia inavyosawiriwa katika fasihi na jamii, na hivyo kuendeleza fikra za usawa.

Watunga sera na wanasiasa: Ingawa si lengo kuu, utafiti huu unaweza kuwa chanzo cha maelezo yanayochochea sera zinazolenga kuondoa ubaguzi wa kijinsia na kukuza usawa katika jamii.

Kwa ujumla, utafiti huu umechangia sana katika kufichua na kuelewa taswira za kiume katika riwaya za Kiswahili, na kuhimiza tafiti zaidi katika nyanja hii ili kuendeleza uelewa wa mitazamo ya kijinsia katika fasihi na jamii kwa ujumla

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya ya *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi*. Mawanda ya utafiti huu yalijifunga katika riwaya mbili. Kwa kuwa hakuna utafiti unaoweza kukamilisha kila jambo, mtafiti anapendekeza yafuatayo kwa watafiti wa baadaye: Kwanza, utafiti ufanywe kuhusu usawiri wa wahusika wa kiume katika tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile; ushairi, tamthilia na hadithi fupi. Halikadhalika, watafiti wa baadaye washughulikie suala la jinsia ya kiume katika tanzu za fasihi simulizi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Inapendekezwa

kwamba, watafiti wengine wachunguze suala la jinsia ya kiume kwa kuongozwa na nadharia nyingine za uhakiki wa fasihi.

## MAREJELEO


Atieno, J. (2019). “Utambulisho wa jinsia katika *Maumbile si Huja* na *Paradiso*.” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Arron, H. (1977). *Marxist Aesthetics*. Cornell University Press. London. *Encyclopaedia Britannica Vollume 9*.

BAKITA. (2017). *Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: BAKITA na TATAKI/TUKI.

Bayyo, F. (2020). “Usawiri wa jinsi ya kiume katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi.” Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa)

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods*. Oxford: Oxford University.

Fakih, J. (2017). “Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si Mbali Tena*.” Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Furlong, N. (2000). *Research Methods and Statistics*: *An Intergrated Approach,* New York: Hart colledge Publishers

Gilbert, A.H. (1962). *Literary criticism*. Plato to Dryden. Detroit: Wayne University press.

Kanwa, O. (2022). “Usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya zilizoandikwa na wanawake.” Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kothari, C.R., & Garg G. (2016). *Research Methodology; Methods and Techniques*; New Delhi. New Age International (p) limited Publishers.

Kimalu, P. K., & Marimba, K. (2014). *Research Methods, Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, TUKI, Dar es Salaam, Tanzania.

Kilonzo, K. (2015). “Ujitambuzi na utambulisho wa kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*.” Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kipyegon, E. (2013). “Nafasi na utambulisho wa mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani*.” Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kobia, J. M., & Mung’ahu, R. (2013). “Ubabedume katika ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Utenzi wa Fumo Liyongo.” Katika *Kioo cha Lugha Juz.* 11. Dar es Salaam: TUKI 14-29.

Lukacs, G. (1972). Studies in European Realism. The Universal Library GROSSET &DUNLAP, NEW YORK.

Maombe, O. (2011). “Ukombozi wa mwanamke katika riwaya za Habwe.” Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mavisi, R. (2018). “Usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya za Zainabu Burhani.” Makala katika *Kioo cha Lugha VOL.16*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Matei, A. (2017). *Chozi la Heri*. Nairobi, Kenya.

Mboya, L. (2018). “Dhuluma kama kichocheo cha mzinduko wa wanawake katika riwaya ya Kiswahili” *Journals of Social Sciences and Information Technology*, Chuo Kikuu cha Rongo.

Mnenuka, (2011). “Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano kutoka katika Nyimbo Teule” katika *Mulika Na*. 29&30. Dar es Salaam: TUKI.

Mohammed, K. (2018). “Kuchunguza usawiri wa mhusika mwanamme katika riwaya ya Kiswahili: *Joka La Mdimu* na *Watoto wa Mama N’tilie.*” Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Momanyi, C. (2021). *Nguu za Jadi*. Nairobi, Queenex Publishers Limited.

Mugenda, O. and Mugenda, A. (2003). *Research Methods*. *Quantitative and Qualitative Approaches*, Nairobi Act Press.

Mulokozi, M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Kauttu publisher: Dar es salaam.

Mutua, M.J. (2017). “Mitazamo ya waandishi wa kike na wa kiume kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili,” Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Pwani.

Mlacha, S. (1985) “Wahusika katika riwaya za Kiswahili (1970-1982)”, Katika Jarida la *Mulika, Toleo la* 17, Uk. 29-44, Dar es salaam, TUKI.

Mwita, B. (2021). “Usawiri wa wahusika wa jinsia ya kiume katika riwaya *Chozi la Heri*.” Moi University Journal, Chuo Kikuu Cha Mashariki mwa Afrika, Baraton.

Ndungo, C. M na Wafula, R.M (1993). *Nadharia ya Fasihi Simulizi (Kiswahili part III).* Nairobi University.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College: Rock Island.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Obure, M. (2012). "Dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini*." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Rymond, M. (2016). "Usawiri wa mwanamume katika methali za Kimeru nchini Kenya. "Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Pwani. (Haijachapishwa)

Samuel, N. (2018), "Ukandamizaji wa jamii unavyodhihirika katika uandishi wa Clara Momanyi na Sheila Ali Ryanga." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)

Sardana, N. Shekoohi, S. Cornett, E. M, & Kaye, A. D. (2023) "Qualitative and Quantitative research methods." In *Substance Use and Addiction Research* (pp. 65-69). Academic Press.

Saro, J. (2017). "Kuchunguza usawiri wa mwanamke katika riwaya: Mfano wa riwaya ya Utengano." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Sengo, T. 2009. *Fasihi za Kinchi*, Dar es salaam: The Trustees of Al Amin Education and Research Academy.

Sulemani, S. (2015). "Usawiri wa mwanamke katika muziki wa nyimbo za dansi: Mifano katika nyimbo za Mbaraka Mwinshehe." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa)

Taherdoost, H. (2021). "Data collection methods and tools for research; a step by step guide to choose data collection techniques for academic and business research projects."

*International Journal of Academic Research in Management (IJARM*), 10(1), 10-38.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wasike, W. (2020). "Mwanamke wa kisasa katika insha za Kiafrika magazetini; mtazamo wa Nadharia ya upalizi." Katika Mulika Na.38, Chuo Kikuu cha Kibaabi.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Fountation.

Wanjiku, M. (2018). "Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya za Said A. Mohamed: Utengano (1980) na Dunia Yao (2006)." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Wamitila, K. W (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi Phoenix publishers Ltd.

Yego, E. (2013). “Nafasi ya mwanamke jinsi inavyotetewa katika nyimbo za Taarabu za Zanzibar. “Tasnifu ya shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

**KIAMBATISHO I**

**MACHAKOS UNIVERSITY**

**OFFICE OF THE DEAN GRADUATE SCHOOL**

Telephone:254-(0)735247939, (0)723805929
Email: graduateschool@mksu.ac.ke
Website: www.machakosuniversity.ac.ke

P.O Box 136-90100
Machakos
**KENYA**

REF. MksU/ASA/GS/3/3

28th August, 2024

The Director,
National Commission for Science, Technology and Innovation
P.O Box 30623,
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam

**RE: KIEMA AGNES MWONGELI (C50-6901-2020)**

The above named is a masters student in the second year of study and has cleared coursework. The University has cleared her to conduct a research entitled: **"Usawiri wa Wahusika wa Kiume Katika Riwaya ya Chozi ya Heri na Nguu za Jadi."**

Kindly assist her with a Research Permit in order to undertake the research.

Thank you.

DEAN OF GRADUATE SCHOOL
28 AUG 2024
MACHAKOS UNIVERSITY

**PROF. KIMITI RICHARD PETER, PhD**
**DEAN GRADUATE SCHOOL**

KRP/sk

ISO 9001:2015 Certified ……………………………………*Co-creating Sustainable Futures*

## KIAMBATISHO II

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 465239

Date of Issue: 26/September/2024

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Miss.. Agnes Mwongeli Kiema of Machakos University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Machakos on the topic: USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIUME KATIKA RIWAYA YA CHOZI LA HERI NA NGUU ZA JADI for the period ending : 26/September/2025.**

License No: **NACOSTI/P/24/40176**

**465239**

Applicant Identification Number

Director General


NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

**KIAMBATISHO III**



**KIAMBATISHO IV**

